Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Sita – Tarehe 6 Novemba, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Massele Mabumba) Alikalia Kiti*

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes.

Na. 67

### Tatizo Kubwa la Maji – Mji Mdogo wa Omurushaka

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES)** aliuliza:-

Mji mdogo wa Omurushaka Wilayani Karagwe unapata maji kwa asilimia 0(0%), na Halmashauri ya Wilaya Karagwe haina uwezo wa kupeleka huduma ya maji

kwenye mji huo kwa sababu kiasi cha shilingi bilioni moja na nusu zinazotakiwa kupeleka maji kwenye mji huo haziwezi kupatikana toka kwenye Halmashauri:-

Je, Serikali iko tayari kwa upendeleo na huruma maalum kutenga fedha za dharura za kuwapatia maji wananchi wa Omurushaka na vitongoji vya Nyakahanga, Bugene na Kishao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba lipo tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma za maji safi na salama kwa wananchi wa Mji wa Omurushaka.

Aidha, juhudi mbalimbali zinafanywa na Serikali ili kuondokana na tatizo hilo la maji ambapo katika mwaka 2010/2011, Serikali ilitoa shilingi milioni 89 kwa ajili ya kuimarisha chanzo cha maji cha Charuhanga kwa kukipatia huduma ya umeme, kusafisha na kukarabati banio (*intake)* kwa kuondoa mchanga na tope, kujenga jengo la kuhifadhia mitambo ya maji na nyumba ya walinzi wa pampu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe katika mwaka 2012/2013 imepanga kukamilisha mradi huu kwa kufanya kazi zifuatazo:-

Kununua mtambo wa kusukuma maji na kuusimika kwenye chanzo cha maji Charuhanga ambapo shilingi milioni 150 zimetengwa kwa ajili ya kufunga umeme katika jengo la mitambo ya maji Charuhanga, kukarabati mabomba ya njia kuu kutoka sehemu ya kuchukulia maji hadi kwenye tanki la kuhifadhia maji Nyakashenyi – umbali wa mita 3,300, kukarabati tanki la kuhifadhia maji Nyakashenyi, kukarabati njia za kusambazia maji na kujenga vilula vya kuchotea maji katika mji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kwa kushirikiana na Wizara ya Maji iko katika mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri (*Consultant)* atakayefanya kazi ya upembuzi yanikifu wa mradi wa maji katika Mji huo. Aidha, taarifa ya tathmini ya Wataalam washauri watakaofanya kazi hiyo imeshawasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa majibu aliyotoa, lakini niseme kwamba ahadi ya kupeleka maji katika kijiji hiki cha Omurushaka ni ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2006 na kiasi kinachotakiwa ni shilingi 1,500,000/= kama swali linavyosema.

Sasa kwamba kwa kiasi cha shilingi 80,000,000/= iliyotolewa na Serikali na kwa majibu haya ya mchakato na Benki ya Dunia haoni kwamba itakuwa ni hadithi tu sasa miaka 6 imepita tangu Rais atoe ahadi hiyo maji hayatapatikana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu ambayo tunatoa hapa ni majibu ambayo tumeyafanyia kazi sana. Kuna mtu anaitwa Daudi Thomas inaonekana Mheshimiwa ana-*doubt* majibu tunayotoa hapa.

Nataka nieleze hapa tunavyozungumza sasa hivi katika chanzo cha Charuhanga tumefunga pampu pale na tumefunga mashine ya umeme pale, na hizi hela tunazosema shilingi 150,000,000/= hivi ni kwamba tunazisukuma ili ziende pale kwa ajili ya kupeleka mabomba kwa sababu eneo lenyewe pale hakuna suala la *graphite* maji unapampu kwa sababu maji yanapanda juu.

Nimezungumza na Walter ni *Engineer* wa maji, nimezungumza na Vitus, wamezungumza wote tumezungumza nao na tumekubaliana kwamba ikifika mwezi Juni maji yapatikane katika mji huu mdogo tunaozungumzia hapa.

Wakati huo huo hela zinazotakiwa katika mradi huu ni shilingi bilioni 1.6. Hela zinazotengwa kwa ajili ya Halmashauri ya Karagwe yote ni shilingi 500,040,000/=. Nimetafuta na nikaenda katika *special request* nione kama Karagwe imeomba hata maombi maalum haikuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri mbele yako kwamba ni kweli wenzetu nimekwenda Karagwe pale wana matatizo makubwa ya maji. Ni kweli kabisa kama wanavyosema Wabunge. Nataka nikuambie kuwa

hatutalala tutahakikisha kwamba maji haya yanapatikana hapo. Kinachotusumbua pale ni kwamba maji yanayonywewa pale kwenye mji ni maji ya visima vidogo, visima vya asili ndiyo maji yanatoka pale.

Sasa nimemwambia Mkurugenzi na nimemwambia yule *Engineer* wa maji lazima wahakikishe kwamba wana-*treat* yale maji kwa sababu wananchi wakinywa hayo maji wanayokunywa watapata homa za matumbo, wataharisha damu na *typhoid* na vitu vingine na Serikali hii iko hapa kuhakikisha kwamba matatizo hayo yanaondoka pale. Kwa hiyo, nataka nimwambie Ndugu yangu Rweikiza mimi nimekuja pale Bukoba mara nne nalijua tatizo hili tutaliondoa na wala usiwe na wasiwasi na *World Bank* kama tulivyozungumza wamesema watapeleka pale kumsaidia ili tatizo liweze kuondoka pale. (*Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni kubwa nchi nzima na kuna malalamiko katika baadhi ya maeneo kwamba Kampuni za Maji zinagawa maji kwa upendeleo. Mfano mzuri ni Kampuni ya *Kili Water* pale Rombo.

Baadhi ya matajiri wenye pesa na wenye mamlaka wanapewa maji, lakini wananchi wanaowazunguka hao hao matajiri hawapati maji kwa sababu ya upendeleo unaofanywa na mafundi wa Kampuni ya *Kili Water*.

Je, Serikali iko tayari kwenda kuichunguza Kampuni ya *Kili Water* ili kuangalia ni nini kinachofanya wawape matajiri na wawanyime wananchi wa kawaida? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri mbele yako kwamba ndio nasikia tatizo hili la upendeleo. Nikitoka hapa nitapiga simu mkoani nataka waende kule wakaangalie hiki ambacho Mheshimiwa anasema hapa na mimi nitawasiliana na Mheshimiwa kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Tunaendelea, Maswali yako mengi tunaingia kwa Mheshimiwa Halima James Mdee.

Na. 68

**Changamoto Zinazozikabili Shule za Umma Nchini**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Shule za Umma zinakabiliwa na changamoto, nyingi ikiwa ni pamoja na upungufu wa walimu, madawati, vitabu, vifaa vya TEHAMA na Maabara:-

Je, Serikali ina mikakati gani mahsusi na ya muda mfupi na mrefu kukabiliana na changamoto hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) unaotekeleza hadi mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM), Serikali ina mikakati mbalimbali kuboresha elimu ya Msingi na Sekondari ili kuondokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ifuatayo:-

(i) Kukarabati na kukamilisha shule za Sekondari 1,200 kwa kiwango cha kuwa na miundombinu yote muhimu ikiwemo maabara, maktaba, vyoo, umeme na maji. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 zimetengwa jumla ya shillingi bilioni 56.3 kwa ajili ya shule 264. Nyaraka za zabuni zimeshaandaliwa na kupelekwa katika Halmashauri zote nchini tayari kwa utekelezaji wa mradi huo.

(ii) Kila mwaka kutenga na kupeleka fedha katika Halmashauri kwa ajili ya miundombinu mbalimbali ikiwemo maabara, madarasa, ununuzi wa maabara hamishika (*Mobile Laboratory*), madawati na kukarabati shule zenye miundombinu chakavu zikiwemo shule zote za sekondari Kongwe.

(iii) Kutoa Ruzuku ya Uendeshaji *(Capitation Grant)* kwa shule zote za Serikali nchini. Asilimia 50 ya fedha hii kwa shule za Sekondari na asilimia 40 kwa Shule za Msingi kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vitabu na vifaa vya TEHAMA. Aidha, Serikali

kupitia Shirika la Kimataifa la Msaada la Marekani *(USAID)* imesambaza vitabu 1,970,530 vya masomo ya Kemia, Biolojia, Fizikia na Hisabati katika shule 1,500 za Sekondari nchini.

Pia, Serikali itatumia asilimia 75 sawa na shilingi bilioni 54.2 ya fedha za fidia ya ununuzi wa rada kununua vitabu vya kiada kwa shule za msingi.

(iv) Kuendelea kujenga na kupanua miundombinu ya shule za Sekondari na ifikapo mwaka 2015; shule 528 zitakamilishwa kuwa na miundombinu muhimu kama ambavyo nimeitaja pale juu kujenga na kukamilisha maabara za masomo ya Sayansi 2,500, Hosteli 100 zenye uwezo wa wanafunzi 48 kila moja, nyumba za walimu 1,800 katika shule 900 zilizo maeneo ya vijijini na majengo ya utawala 1,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mipango ya Bajeti za Halmashauri, Serikali inatenga fedha kwa kuboresha miundombinu ya shule mbalimbali kulingana na vipaumbele vya Halmashauri yenyewe.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi bilioni 74 kwa shule za Sekondari na bilioni 33 kwa shule za Msingi zimetengwa kwa ajili ya madawati, ujenzi wa maabara, vyoo, nyumba za walimu, madarasa na hosteli. Pia asilimia 25 sawa na shilingi bilioni 18.1 ya fedha za fidia ya rada zitatumika kununua madawati kwa shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha upatikanaji wa walimu wa kutosha, Serikali kwa kushirikiana na sekta

binafsi imeongeza udahili katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu pamoja na kujenga vyuo vipya. Wanafunzi wanaojiunga na kozi za ualimu wameendelea kupatiwa kipaumbele katika Bodi ya Mikopo.

Serikali itaendelea kuajiri walimu wanaohitimu na kufaulu na kuwapanga katika Halmashauri zote nchini kwa kuzingatia upungufu na ifikapo mwaka 2014 upungufu wa walimu utakuwa tumekwishaupunguza kwa asilimia zaidi ya 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mradi wa Mpango wa Majaribio wa Ufundishaji wa Masomo ya Kompyuta katika shule za sekondari 126. Mpango unahusisha ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza kwa njia ya kompyuta.

Awamu ya kwanza ya mradi inahusisha shule 50 kuanzia Julai 2011-2013. Shule 21 na Halmashauri husika zimepatiwa vifaa vya kufundishia ikiwa ni pamoja na *Lap top* 11, Projekta, *Scanner, Photocopier* Vipaza sauti pamoja na *flash disk*. Lengo la mradi huu ni kuona mafanikio yanajitokeza ili kuweza kufikia shule zote nchini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali lake moja kati ya vitu alivyovizungumzia ni (*Capitation Grants)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sote tunajua na Serikali inajua kwamba tunasema utapeleka fedha kule chini, lakini ukweli ni kwamba fedha zinakwenda kidogo sana. Mwaka

jana Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mulugo alisema Serikali itahakikisha kila mtoto wa shule ya Msingi atapata shilingi 15,000/=, kila mtoto wa shule ya Sekondari atapata shilingi 25,000/=.

Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka jana unaonesha katika shilingi bilioni 50 zilizotengwa kwa ajili ya *Capitation Grants* shilingi bilioni 10 ndio zilizoenda shuleni.

Matokeo yake ni kwamba mzigo wa kuziendesha hizi shule kule chini wanaachiwa wazazi. Sasa mimi nilitaka Serikali ituambie juzi alijibu Waziri wa Elimu hapa kisiasa kwamba kuna Kamati za Shule, lakini hatuwezi kuziachia Kamati za Shule ziendeshe kila kitu wakati kuna jukumu la msingi la Serikali. Swali langu?

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Swali langu kwa Serikali ni kipi kiwango cha chini cha mzazi kuchangia na ni kipi kiwango cha juu cha mzazi kuchangia uendeshaji wa shule zetu.

Pili, uandikishaji wa wanafunzi umeanza nimepigiwa simu asubuhi kutoka jimboni kwangu kwamba mwanafunzi kama hana fedha za kujiandikisha zinazo *range* kuanzia shilingi 20,000/= mpaka 70,000/= kutegemeana na shule haandikishwi.

Sasa nataka Serikali itoe tamko leo kwa mwanafunzi ambaye anakwenda kujiandikisha lakini hana uwezo wa kutoa hiyo fedha *cash* afanyeje? Liwe tamko kweli na sio

tamko la kisiasa wakati huko chini uhalisia ni hali tofauti. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza anahitaji kujua ni kiwango kipi cha chini na cha juu ambacho mwananchi anatakiwa kuchangia kwa maendeleo ya shule yake.

Nataka nimweleze Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwamba shule hizi zote za msingi na Sekondari nchini ni shule za wananchi. Tuna shule za Msingi katika kila kijiji na inawezekana pia katika kila kitongoji kikubwa chenye idadi kubwa ya wananchi wanahitaji shule na tunazo shule za sekondari katika Kata zetu zote nchini kwa sasa.

Kama ziko ambazo hazina shule ni Kata chache sana. Shule hizi kwa kuwa ni za wananchi bado zinafanywa uendelezaji wake pamoja na Serikali kwa upamoja wake na ndiyo kwa sababu tunapotoa majibu ya msingi hapa tunaeleza ni kiwango gani cha fedha Ofisi ya Waziri TAMISEMI imepeleka katika Halmashauri zetu kwa ajili ya maendeleo.

Lakini fedha hii haitoshi kukamilisha mahitaji yote ya maendeleo ya shule husika na kwa maana hiyo sasa Kamati za Shule kwenye maeneo yao, Mabaraza ya Madiwani kwenye maeneo yao wanakaa kutenga Bajeti husika ili kuboresha maendeleo ya shule husika iwe ni shule ya msingi au Sekondari kwa Maendeleo yake na kwa maana hiyo hatuna kiwango cha chini cha uchangiaji wala

cha juu ambacho tumekiweka inategemea na mahitaji ya uendelezaji wa shule husika na mipango waliojiwekea wananchi wenyewe kwenye maendeleo yenyewe ili shule iweze kupata maendeleo. Lakini bado Serikali tunapeleka fedha kama ambavyo tunazitamka kwa ajili ya uendelezaji kwenye majengo lakini pia hata vifaa vya ufundishaji.

Suala la pili, Mheshimiwa Mbunge amepata taarifa kutoka kwa wananchi wake kwamba wanafunzi wanaoandikishwa Darasa la Kwanza wanatakiwa kulipia. Nataka nitamke na hii narudia, nimeshatamka mara nyingi hakuna gharama yoyote anayotoa mzazi ya kumpeleka kumwandikisha mtoto kwenda shule darasa la kwanza. (*Makofi)*

Elimu ya Msingi nchini ni bure, elimu ya Sekondari nchini uchangiaji ni wa shilingi 20,000/= kwa mwaka zile za kutwa na zile za bweni ni wa shilingi 70,000/= Kama kunatokea michango katika shule yoyote ile iwe ya Msingi au Sekondari lazima itakuwa imeamriwa na Kamati yenyewe ya shule kulingana na mahitaji ya shule husika.

Hakuna mchango wowote ambao mzazi anapaswa kulipia kama tozo ya kumwandikisha mtoto kwenda kuanza darasa la kwanza. Popote pale ambako inaonekana jambo hili lipo tumeshawaagiza Wakurugenzi na Maafisa Elimu, Mwalimu Mkuu anaendesha michango ya kumwandikisha mtoto shuleni kwa ajili ya kumwandikisha achukuliwe hatua mara moja na mtusaidie kubaini ni wapi tatizo hilo lipo ili tuweze kulichukulia hatua na tumeshawaelekeza Maafisa Elimu, Wakurugenzi naomba

Watanzania wajue kwamba hawapaswi kulipa fedha kwa ajili ya kumwandikisha mtoto kwenda shuleni.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo. Idadi ya watoto wadogo wanaomaliza darasa la saba nchini mwetu kwa mwaka ni wastani wa watoto milioni moja na laki moja.

Shule za Sekondari za Serikali kwa maana ya shule za Kata na hata shule za watu binafsi zinauwezo wa kuchukua watoto wasiozidi laki tano kwa mwaka. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba sisi kama taifa kila mwaka tunazalisha zaidi ya watoto laki sita wenye umri wa miaka kati ya kumi na tatu na kumi na nne wanaishia darasa la saba na hakuna mpango wowote wa kitaifa dhidi ya kundi hili.

Waziri kwa niaba ya Serikali atalieleza nini Bunge, kuna mkakati gani wa kiserikali la kuhakikisha kwamba kundi hili kubwa la watoto ambao tunazalisha kwa mwaka wasiopungua laki sita linawekewa utaratibu maalum wa aidha wa mafunzo ya baadaye au mafunzo mengine yoyote yale ambayo yanaweza yakawapatia utaalam fulani kwa sababu umri wao kwanza ni mdogo elimu yao ni ndogo na Sheria ya Mikataba katika nchi yetu inaruhusu watoto kuajiriwa kwa zaidi ya miaka 18 na hawa wana miaka kumi na nne, taifa na Serikali inasema nini kuhusu jambo hili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalitambua sana tatizo hilo na Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, imejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba inashughulikia kwa mafanikio tatizo la kuwaelimisha vijana wetu nchi nzima.

Sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha sera mpya. Sera ya mafunzo ya ufundi, sera ya elimu ya ufundi na mafunzo stadi na kui-*revise* sera ya elimu ambayo itahakikisha kwamba mifumo hii muhimu ya elimu, elimu ya kawaida na elimu ya ufundi inachanganywa kuhakikisha kwamba vijana wote wanapata nafasi ya kusoma.

Hawa ambao hawaingii kidato cha kwanza wanaenda kwenye mkondo wa ufundi na wale ambao wanaendelea tumejenga shule nyingi zaidi na hawa watakao kuwa na ufundi wakienda mbele wanaweza pia kuja kukutana na wale wengine katika ngazi za vyuo na ngazi za vyuo vikuu kwa sababu tumeunganisha mifumo hiyo miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalifahamu na tutalishughulikia kikamilifu. (*Makofi*)

**MHE. MODESTUS D. KILUFI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nataka kujua ni jitihada gani za makusudi sasa zinafanyika na Serikali kuhakikisha kwamba shule za Kata nazo zinapewa umuhimu kama ambavyo zilivyo shule nyingine kwa sababu shule hizi hazina umeme, nyingi hazina maabara hazina lakini kwenye mashindano ya mtihani unaotungwa ni uleule.

Sasa je, hatuoni kwamba hizi shule zinafanyiwa visivyo kulingana na hali halisi ya taaluma inayotolewa katika nchi hii. Nini jitihada ya Serikali sasa kuona kwamba huduma hizo inazifikia hizo shule kwa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba na elimu hiyo inaboreshwa kwenye shule zetu za kata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ukweli kwamba tunazo shule za Kata kwenye maeneo yote na ukweli kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba shule zote hizi watoto wanaosoma katika shule hizo wanapata elimu ya kutosha ikiwemo na ile ya masomo ya Sayansi.

Serikali imeendelea kuwa na mkakati endelevu ambao utawezesha watoto hawa kusoma masomo ya Sayansi kwa kujenga miundumbonu ya majengo ya Maabara ili waweze kusoma masomo hayo ya Sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Maabara tayari Serikali kupitia ofisi ya Waziri Mkuu tumeshapeleka fedha katika Halmashauri zote na nakala niliwaletea hapa za ununuzi wa vifaa vya Maabara tunaita *Mobile Laboratory* kwa lengo la kuanza kusoma masomo ya Sayansi na *Mobile Laboratory* inatosheleza kusoma masomo yote ya Sayansi yakiwemo ya *Chemistry*, *Physics* na *Biology* kuanzia sasa na fedha ambayo tumeipeleka katika maeneo yote ni bilioni tatu na tayari tumeshaisambaza nchini na Halmashauri zote wamepokea fedha kwa ajili ya kununua *Mobile Laboratory*.

Zinapopatikana *Mobile Laboratory,* Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wale wataalam na wauzaji wa vifaa vile walikuja hapa waka-*display* na Mheshimiwa Waziri Mkuu alituongoza kwenda kukagua. Kwa hiyo, tuna uhakika kwamba *Mobile Laboratory* zinapatikana sasa Halmashauri ziagize.

Lakini kama hiyo haitoshi tumetenga milioni 600/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ili tuzisambaze pia kwenye Halmashauri zote tuweze kuongeza *Mobile Laboratory* ziende kwenye shule za Kata ili tuweze kuwafundisha watoto hawa masomo haya ya Sayansi.

Na. 69

**Kuzuia Uchimbaji Dawa Wakati wa Safari**

**MHE. JOYCE J. MUKYA** aliuliza:-

Mwezi Agosti, 2012 Serikali ilitangza kuzuia utaratibu wa abiria kuchimba dawa njiani wakati wanaposafiri na mabasi ya abiria:-

(a) Je, ni Sheria gani ilitumika kutoa tamko hilo?

(b) Je, Serikali imeweka miundombinu gani mbadala kuwezesha huduma hiyo muhimu kuwa safi?

(c) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima haki ya msingi baadhi ya abiria ambao kutokana na maradhi ya kisukari, homa za matumbo na wajawazito hulazimika kupata huduma hiyo mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce John Mnyika (Mbunge, Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* inayo wajibu wa kusimamia na kulinda mazingira yakiwemo ya barabara ili kuzuia yasiharibiwe kwa kuchafuliwa na watumiaji au watoa huduma za usafiri hapa nchini. Hivyo, tamko la kuzuia abiria kuchimba dawa wanapokuwa safarini lilitolewa kwa kuzingatia Sheria ya *SUMATRA* Na. 9 ya mwaka 2001 vifungu vya 5(f) na 6(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na msingi huo wa kisheria, misingi yetu ya ustaarabu na malezi bora hairuhusu shughuli zinazotakiwa kufanyika kwa faragha zifanywe hadharani tena bila tahadhari ya kwamba kuna akina mama, akina baba, vijana na hata watoto wadogo ambao wengi wao inakuwa mara ya kwanza kuona wazee wakifanya vitu vyao hadharani.

Hivyo basi kuchimba dawa kwa halaiki ni kitendo cha aibu kubwa na cha kudhalilisha utu wetu na kinatoa picha mbaya sana kwa wageni wanaotembelea nchi yetu. Ipo vilevile hatari ya kuvamiwa na majambazi na hata kushambuliwa na wanyama wakali. Kung’atwa na wadudu au nyoka ukiwa katika shughuli hiyo ya uchimbaji dawa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya utafiti katika njia mbalimbali za barabara ziendazo mikoani na kubaini kuwepo kwa maeneo mazuri na rasmi yaliyojengwa na Halmashauri za Miji, Mikoa, Wilaya pamoja na watu binafsi ambazo abiria wanaweza kupata huduma za vyoo katika hali ya usalama na kwa heshima pindi wanapokuwa safarini.

Aidha katika baadhi ya maeneo ambapo huduma za vyoo hazipatikani kwa urahisi kwa wasafiri, Halmashauri husika kwa kushirikiana na watu binafsi zimeanza kujenga vyoo kwa ajili ya abiria.

Mfano katika eneo la njia panda ya Kilosa, awali lilikuwa linatumika kuchimba dawa pakiwa na pori lakini hivi sasa kumejengwa vyoo vya kisasa. Serikali imechukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha madereva na makondakta wa mabasi ya mikoani. Kuwatangazia abiria vituo vyenye huduma za vyoo pindi wanapokuwa safarini?

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imezingatia makundi yote ya wasafiri kwa kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria ikiwa ni pamoja na kuwawekea miundombinu itakayosaidia kulinda usalama wa afya zao pindi wanapokuwa safarini na kuhakikisha huduma za vyoo zinapatikana kiurahisi wakiwa safarini.

**MHE. JOYCE J. MUKYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Je, Sheria hii ni kwa ajili ya magari ya abiria tu au ni kwa ajili ya magari binafsi pia kwa sababu hata tumeona magari mengine binafsi ambayo yanasafiri mwengo mrefu wakichimba dawa wakiwemo viongozi mbalimbali?

Swali la pili, pamoja na Serikali kuweka miundombinu mbalimbali humo njiani lakini hamwoni kuna umuhimu wa mabasi kuwa na vyoo vya ndani?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii haibagui kwamba uchimbaji dawa au uharibifu wa mazingira ni kwa wasafiri wa mabasi peke yao. Hata watu binafsi wanaosafiri huku njiani kisheria hawapaswi kufanya hizo shughuli za uchimbaji dawa.

Kwa hiyo, yeyote anayefanya hivyo anatuvunjia Sheria na nitoe rai kupitia Bunge lako Tukufu kwamba wananchi wasifanye hizo shughuli hadharani. Unaweza kuwa wewe Mheshimiwa unachimba dawa barabara linapita basi wapo wakwe zako humo ndani, ni aibu.

Kwa hiyo, niombe kutumia Bunge lako Tukufu kuwaomba viongozi na wananchi kwa ujumla wanaosafiri kwa magari yao binafsi wasifanye hayo mambo. Ziko sehemu nyingi ambazo wanaweza kujistiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili mabasi kuwa na vyoo. Ingependeza sana kama mabasi yote yangekuwa na vyoo vya ndani lakini bahati mbaya watengenezaji wengi wa mabasi hawaweki vyoo katika magari hayo. Kwa hiyo, ndiyo maana kuna hiyo *option* ya kutumia sehemu maalum zilizotengenezwa kwa ajili ya kuchimba choo. Basi kama linachoo ni zuri zaidi kwa ajili ya huduma hiyo ya kuchimba dawa.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ndani ya treni kuna vyoo lakini abiria wanapokwenda kujisaidia ule uchafu wote unadondoka chini moja kwa moja.

Hakuna *container* au vyombo vya kupokea ule uchafu ili baadaye uweze kuhifadhiwa mahali salama. Sasa je, kuna utaratibu gani wa kufanya marekebisho wa jambo kama hili?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mabehewa ya abira yanayotumika sasa hivi mengi yalinunuliwa miaka 25, 30, 40 iliyopita. Kwa hiyo, yalitengenezwa katika namna ambayo mtu akienda kuchimba dawa ule uchafu unadondoka kwenye reli.

Serikali imekwishaliona hili na mabehewa yote ambayo yameagizwa sasa, kwanza tumedhamiria kuondokana na mabehewa yanayoitwa daraja la tatu lakini tutahakikisha kwamba yatakuwa na vyoo ambavyo baadaye mtu akifanya hiyo shughuli ule uchafu haudondoki chini kwenye reli isipokuwa utaondolewa baada ya treni kufika mwisho au katika vituo vya katikati ya safari.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile naulizia wasafiri wa meli, *Lake Tanganyika, Lake Victoria, Lake Nyasa* kwenye hizi meli zetu mtu akijisaidia moja kwa moja kinyesi kinakwenda ziwani na wananchi wetu ndiyo wanakunywa maji hayo hayo na kila kitu. Kuna taratibu gani kuzuia hizo meli au kinyesi kisidondoke moja kwa moja kwenye maziwa? Kipindupindu kimezidi kule kwetu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye suala la treni, meli hizi anazozisema, Meli ya *MV. Liemba* ni ya mwaka 1905, Victoria ya mwaka 1961 ni meli ambazo zimejengwa siku nyingi na kwa hiyo teknolojia ya kukusanya uchafu wakati watu wanajisaidia nadhani haikuwepo wakati huo. Tutajenga meli za kisasa sasa hivi. Nadhani haya yote yatazingatiwa.

Lakini kwa kweli huduma hiyo inavyopatikana kwa sasa katika meli hizo bahati mbaya sana iko namna hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi swali namba 70 linaulizwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

Na. 70

**Kudhibiti Uvuvi Haramu Unaofanywa na Meli za Nje**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Mwaka 2009 ilikamatwa meli ya *MV. TAWARIQ 1* iliyokuwa ikifanya uvuvi haramu katika kina kirefu cha Bahari ya Hindi Ukanda wa Tanzania na kuharibu mazingira ya ukanda huo.

Je, ni hatua gani zimechukuliwa katika kudhibiti uvuvi haramu unaofanywa na meli za nje katika Bahari yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kupambana na uvuvi haramu. Hatua hizi ni pamoja na:-

(1) Kusimika, kutumia na kuimarisha vifaa vya kuangalia na kufuatilia mwenendo wa uvuvi baharini *(Vessel Monitoring System – VMS)* ambapo kifaa hicho kimewezesha kufanya doria za uhakika na kupunguza gharama zake kwa asilimia 40 – 45;

(2) Kukusanya taarifa muhimu za meli zinazovua katika maji yetu;

(3) Kutoa mafunzo ya aina mbalimbali kwa watumishi ili kuongeza uwezo wao na kuleta ufanisi;

(4) Kuendesha doria za majini na anga;

(5) Kukamata meli na zana haramu kushtaki na kusimamia kesi za uvuvi haramu; na

(6) Kutoa hukumu iliyoambatana na adhabu kali kwa wahalifu husika ikiwemo kifungo na faini.

Mfano mzuri ni wa meli ya *Tawariq 1* ambapo watuhumiwa walipewa adhabu iliyoambatana na utaifishaji wa meli yenyewe, zana za uvuvi na mazao ya uvuvi yaliyovumiliwa katika uvuvi huo haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshirikiana na mataifa jirani na Taasisi na Jumuiya za Kimataifa kama vile nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* katika kupeana taarifa za vyombo vinavyoonekana katika nchi husika ili kulinda rasilimali zetu kwa pamoja na kupambana na uvuvi haramu.

Aidha, Mashirika kama vile *Indian Ocean Tuna Commission (IOTC)* husaidia katika kupata taarifa za kuwezesha kubaini vyombo vinavyojihusisha na uvuvi harama *(Illegal Unregulated Unreported Fishing-IUU).* Vilevile kupitia *program* ya *Smartfish,* Serikali inanufaika kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za usimamizi na udhibiti wa uvuvi haramu.

Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu *(DSFA*) imeandaa Mpango Mkakati wa kuendeleza na kusimamia shughuli za uvuvi katika Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya hatua zilizochukuliwa na Serikali uvuvi haramu umepungua na idadi ya vyombo vinavyoomba kupatiwa leseni na kuvua kihalali imeongezeka. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, jumla ya vyombo 113 viliomba na kupatiwa leseni ya kufanya uvuvi katika ukanda wa uchumi wa Tanzania chini ya Sheria na Kanuni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi hizi uvuvi haramu katika bahari yetu umedhibitiwa kwa kiwango kikubwa na Serikali itaendeleza juhudi zake na hatimaye kumaliza kabisa tatizo la uwepo wa uvuvi haramu.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wadogo wadogo ambao ni maskini sana wakati mwingine hutumia vifaa duni visivyoruhusiwa si kwa mapenzi yao bali ukosefu wa mitaji ya kuweza kufanya uvuvi wa ufanisi wanakuwa hawana.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwapa vifaa mbadala pale inapotokea wanakamatwa na vifaa hivyo haramu ili waweze kukidhi mahitaji yao iwe kwa njia ya mkopo au kuwasaidia weweze kuendelea na maisha yao kama kawaida?

Swali la pili, tumekuwa tukishuhudia uchomaji wa vifaa mbalimbali vinavyokamatwa vikijihusisha na uvuvi haramu vya wavuvi wadogo wadogo.

Je, Serikali haioni kwamba ilikuwa ni sahihi kuzichoma meli kubwa pia ili iwe fundisho kwa wale wote wanaodhania kuja kuiba rasilimali zetu kama wanavyochoma vifaa vya wavuvi wadogowadogo pindi wanapovikamata ili wavuvi wadogo wadogo nao wajue kwamba kama meli inachomwa je, mitumbwi itakuaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya MheshimiwaKhatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Moja, ni kweli kuwa wavuvi wadogo wadogo wanatumia vifaa duni na kumekuwapo na mkakati ambao ni wa Kitaifa moja itambulike kuwa kwanza vifaa hivi vinapigwa marufuku ili kuhakikisha kuwa uvuvi unaendelea kuwa ni sekta inayoendelea, ni sekta ambayo hatutamaliza samaki kwenye maji.

Lakini mkakati huu umekuwa ni kuwaomba wajiunge katika makundi madogo madogo ambayo yanakopesheka iwe ni *SACCOS* au wapate jina lolote lakini kwa njia hii Benki zinaweza kuwakopesha na *colatrol* likabaki kuwa ni kundi lililotambulika na kusajiliwa kwa taratibu za Kiserikali.

Mbili, uchomaji wa vifaa ni ili nyavu hizo zisirudi baharini na kuendelea na uvunjivu wa Sheria lakini uchomaji wa meli kubwa kwa kweli kwa kuwa sisi ni nchi inayoendelea na inayohitaji kila aina ya rasilimali mali hizi hasa nikichukua mfano wa hiyo meli kuwa imetaifishwa ili tuweze kuitumia.

Moja kwanza ni kuimarisha doria mle lakini pia kutumia kama nyenzo tunazohitaji kwa ajili ya kuendeleza sekta hii. Kwa sababu kama tunahitaji bado kila aina ya rasilimali ninadhani siyo busara kuchoma kitu ambacho kinaonekana kuwa kina thamani ya mabilioni ya dola kwa hiyo hizi hazichomwi badala yake wale wavuvi haramu hawabaki na mali hizo, mali hizo zinachukuliwa kitaifa ili ziendeleze na kudumisha sekta hii ya uvuvi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninashukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninapenda kumwuliza Naibu Waziri.

Je, anayo habari kuwa pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa bado meli za kigeni zinaendelea kuiba samaki wetu katika mwambao wa bahari baina ya Kenya na Tanzania katika maeneo ya Kaskazini Pemba, anajua hivyo? Kama anajua ni hatua gani wanazochukua?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa kama ifuatavyo:-

La kwanza, Mamlaka ya Uvuvi Bahari Kuu yenye Makao Makuu yake Zanzibar kama nilivyosekma katika majibu yangu ya swali la msingi hawa wameweka mfumo unajulikana kama DVMS maana yake ni *Versal Monitoring System* na mfumo huu umewawezesha watu wa Mamlaka yetu ya Uvuvi, moja kwanza kutambua kila meli inapoingia kwenye maji yetu kwamba imeingilia wapi na pili wapo wanavua au wanafanya shughuli zipi maana wanaweza wakatambua kuwa mwendo wa meli ni wa kasi kiasi gani wanafanya shughuli zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama na meli yenyewe ina mfumo ama wa VMS ama *Argos system* inawezekana kutambua pia na kuona kuwa ni nini kinachofanyika.

Kwa hiyo, hiyo taarifa inakusanywa na mara nyingi kwa upande wa doria hizi nilizogusia doria zinafanywa mara kwa mara Mamlaka yetu ikishirikiana na KMKM lakini pia *Navy* pamoja na polisi wetu kwa upande wa majini pia.

Na. 71

## Kukomesha Vitendo vya Uvuvi Haramu

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kufuatia kukithiri kwa vitendo vya uvuvi haramu wa kutumia sumu na mambomu katika ukanda wa Bahari ya huku Lindi na Mtwara 1998 Serikali iliahidi kununua *(Speed Boat)* ili kuendeleza kuthibiti uvuvi huo na pia kutunza mazingira ya bahari.

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuleta *speed boat* hizo kwa ajili ya doria kwa ukanda wa Kusinini?

(b) Je, Serikali haijasaidia kuwapa zana mbadala za uvuvi wale wote waliokamatwa na kuacha uvuvi haramu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum,, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2007-2010, Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine and Coastal Environmental Management Project (MACEMP)* ilininua boti 12 ziendazo kasi *(Speed Boats)* na kuzigawa katika Mikoa ya Mtwara (3), Lindi (7) na kituo cha Doria cha Mtwara (2).

Boti hizi zimewezesha Halmashauri za Lindi, Mtwara na Hifadhi ya Bahari ya *Mnazi Bay (MBREMP)* kufanya doria majini dhidi ya uvuvi haramu katika maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mradi wa *MACEMP* Kwa kushirikian na *TASAF,*ilitoa fursa kwa jamii za mwambao wa Bahari ya Hindi kuibua Miradi midogo ya kiuchumi kwa lengo la kuboresha maisha yao na kuweka mifumo ya ikolojia ambayo ni endelevu. Lengo la miradi hiyo ni kuwaendeleza wananchi kupata zana bora za uvuvi na kufanya shughuli mbadala zikiwemo zile za ufugaji wa samaki, nyuki na kuku.

Chini ya utaratibu huo, *MACEMP* ilifadhili jumla ya miradi midogo 157 yenye thamani ya shilingi 2,198,275,008/= katika Mikoa ya Lindi (100) na Mtwara (57). Kiasi hicho cha fedha kimenufaisha wananchi 3,121 wakiwemo wanawake ni 1,318 na wanaume 1,803. Jamii zilizohusika na uibuaji miradi ni pamoja na baadhi ya wananchi waliowahi kukamatwa kutokana na vitendo vya uvuvi haramu.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri lakini nina swali moja na nusu kwa majibu haya kwa nini ninasema nusu ninaanza na nusu. Tufanye tathimini kama Mtwara na Lindi waliwahi kupokea *Speed Boat* 7 Lindi na 3 Mtwara nusu imeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya *MANCEMP* haikuwafikia walengwa hasa wale waliokamatwa kwa uvuvi haramu wa kutumia mabomu. Hivyo wale wavuvi haramu wa kutumia mabomu bado wapo na hawana kazi yoyote hawana zana mbadala baadhi yao wamethubutu kurudia tena uvuvi haramu wa kutumia mabomu.

Kwa hiyo, mimi ninataka kumwuliza Naibu Waziri. Je, Serikali inafahamu kuwa kula samaki wanaovuliwa na sumu na mabomu kuna madhara kwa binadamu?

Serikali ina kauli gani kwa wananchi wa Mtwara na Lindi kuhusu kukomesha kabisa uvuvi haramu wa kutumia mabomu, kwasababu una madhara na watu wanaumwa matumbo kwa ajili ya sumu na mabomu? Ninaomba tupate kauli ya Serikali ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja na nusu alilouliza Mheshimiwa Fatma Mikidadi. Moja kwanza niseme kuwa mnamo tarehe 17 na 18 mwezi wa kumi mimi mwenyewe nilitembelea Lindi na baadae nikapita Kilwa na nimeona Baadhi ya boti hizi zilizotolewa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama ana wasiwasi nimwondoe wasiwasi kuwa kwa uhakika boti hizi kama nilivyosema 12 zimenunuliwa kwa ajili ya Mtwara na Lindi, hilo nusu swali nitakuwa nimeshajibu kwa hiyo niende kwenye swali lake la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya sumu na mabomu ni kitu kinacho hatarisha afya ya walaji wa samaki lakini pia inahatarisha mazingira. Maana haya mabomu yanapolipuliwa yanaharibu matumbawe pamoja na maeneo ambayo kwa kawaida samaki wanazaliana. Kinachofanyika ni kuendelea kutoa elimu kwa umma moja kwanza watu wafahamu na wasusie wasile samaki hawa waliovuliwa kwa njia hii maana ni hatari kwa afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, mikakati ipo na ndiyo maana tuna vikosi vya doria na kwa sasa majadiliano yameanza moja kwa kuona namna ya kuchukua hatua.

Kwa mfano uvuvi unaotumia mabomu badala ya kuona bomu ama vitu vinavyolipuliwa vinahusiana na uvuvi haramu vionekane pia kwamba ni silaha haramu, maana katika maeneo mengine yanaua pia na unakuta wanaotumia na wenyewe wengine wamekuwa vilema kwasababu ya vidole kukatwa na vifaa hivi vinavyolipuliwa.

Lakini kwa ukanda wa Kusini nisisitize kuwa jitihada tunaziongeza zaidi kwa sababu mambo ya gesi mara nyingine mambomu haya wanayotumia kuvua kiharamu zinalipuliwa karibu na maeneoa ambayo kwa kweli ni hatarishi maana kunakuwepo na gesi na mafuta pia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa sekta hii ya uvuvi kuanzia Mtwara Mikindani kwenye Bahari ya Hindi mpaka Tanga ambao una urefu wa kilomita 1,424 na kwa kuwa, ni sehemu mojawapo ya kukuza pato la wananchi wetu na kule Lindi

na Mtwara wanaofaidika na mradi huu ni wananchi 3,121 kwa takwimu za Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa wavuvi hawa wanavua samaki kwenye *deep sea* siyo kwenye *shalow water* wanaenda kwenye *deep sea* na *deep sea* ni hatari sana kwa uhai wa mwanadamu.

Je, Wizara yake ina kitengo maalum cha kutoa elimu kwa ajili ya kuokoa uhai wa Watanzania pindi maji yanavyokuja kwa kasi yaani *speed* ya maji *high tide* inapotokea hivyo maisha yanakuwa magumu kwa wavuvi wetu, wanaangamia uhai wao unaondoka kwa kukosa elimu.

Je Wizara ina kitengo hicho na kama haina kitengo siyo vyema wakawa wanatoa elimu ya kutosha na vifaa vya kutosha ili tuokoe maisha ya binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi niliyoitoa ni ya watu walionufaika na mradi huu wa *MANCEMP.* Kwa hiyo, kuna wengine wengi ambao hawapo kwenye hii idadi ya 3,000 maana kwa uhakika watu wanaotegemea uvuvi ni wengi sana kuliko hawa 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa 3000 ni wale tu walionufaika kwa mradi huu na ni kwa Mikoa tu ya Lindi na Mtwara maana wako zaidi ya 8000 walionufaika katika Halmasahuri zingine 14 ukiacha maeneo ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali alilouliza ndilo hili lina fahamika Wizarani tuna kitengo ambachi taaluma wanayo ya kutosha na wamekuwa wakijibidisha kufanya kazi hizi lakini kwa uhakika bado wanakwamishwa na uhaba wa vifaa na uduni wa vifaa wanavyotumia.

Kwa hiyo, katika mikakati tuliyo nayo Kiwizara na Kisekta hili ni eneo mojawapo ambalo linajengewa uwezo kwa kipindi cha miaka 5 na tutaomba mtuunge mkono Waheshimiwa Wabunge ili hii sekta iweze kupata mapinduzi na sisi Kitaifa tutanufaika zaidi na rasiliamali hii ambayo ni ya manufaa sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mara nyingi sana tunalalamika na uvuvi haramu na kwa kuwa miradi ya kuwasaidia hawa wavuvi waondokane na uvuvi haramu ni michache sana, na kwa kuwa *MANCEMP* na *TASAF* uliyoitaja ambayo yote ni miradi ya Kitaifa lakini hatujaona ilivyosaidia katika visiwa wa Unguja na Pemba.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari mimi na yeye twende Jimboni kwangu Mkanyageni tukatizame *MANCEMP* gani na *TASAF* gani iliyosaidia wavuvi wadogo wadogo katika Jimbo la Mkanyageni?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kusema kuwa taratibu za Katiba yetu Sheria zilizopo na Kanuni uvuvi ndani ya maji yetu siyo suala la Muungano. Kwa hiyo, kwa upande wa uvuvi kama ndani ya Bahari Kuu Mamlaka yetu kama Wizara yanaishia Pwani ya Dar es salaam na Tanga.

Kwa ushirikiano wa Waziri mwenzetu wa upande mwingine lakini pia labda kwa kutumia mfano wa mfuko wa *TASAF* inawezekana kuangalia na labda taratibu zitazamwe lakini ninadhani ni vizuri Mheshimiwa pia na yeye anafahamu nina uhakika kuwa kwa upande wa mandate nchi yetu kwa uvuvi siwezi kwenda Jimboni kwake nikatazama, maana hili linaangukia katika Mamlka husika kwa upande mwingine. *(Makofi)*

Na. 72

**Kutekelezwa kwa Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA)** aliuliza:-

Pamoja na Halmashauri nyingi kutimiza vigezo vya kupata vibali vya ukandarasi kwa ajili ya miradi ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, bado miradi hiyo inaonekana haitekelezeki:-

Je, kwa nini miradi hiyo imetumia fedha nyingi katika hatua za awali za upembuzi yakinifu na baada ya hapo inashindwa kutekelezeka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji *(WSDP)* inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Fedha za program zilianza kutumika mwaka 2007/2008 katika ujenzi wa miradi ya maji yenye kuleta matokeo ya haraka.

Miradi hii imeleta mafanikio kwa kujenga vituo 9,546 vya maji na wananchi wapatao 2,386,500 wanaoishi vijijini wanapata huduma ya maji. Kwa upande wa Halmashauri ya Songea, Miradi mitano ya maji ya mtiririko ilikarabatiwa na visima 31 vilichimbwa na kufungwa pampu za mkono.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi hufanyika ili kuainisha mahitaji halisi ya maji, kubaini ubora na kiasi cha maji kilichopo, kujua gharama za miradi pamoja na miundombinu ya maji kwenye maeneo ambayo hakuna maji ya kutosha au maji yaliyopo kukosa ubora.

Kitaalam, hakuna mradi unaojengwa bila kupitia hatua ya upembuzi yakinifu kwa lengo la kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu. Katika utekelezaji wa *WSDP,* wastani wa gharama za kusanifu mradi katika kijiji kimoja ni shilingi milioni 50 na kuchimba ni kisima kimoja ni shilingi 20 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 31 Oktoba, 2012 Halmashauri 103 zimepata vibali vyote vya kuanza ujenzi wa miundombinu na maji kupitia *WSDP* kati ya hizo Halmashauri 77 zinatekeleza ujenzi wa Miundombinu ya maji katika vijiji 211.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wote kushirikiana na Halmashauri zenu ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo kwani ni jukumu la Halmashauri husika kusimamia utekelezaji wake baada ya kupata vibali vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatumia milioni 318.39 katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji vya Maweso, Masigira, Likuyufusi na Liweta.

Hata hivyo, kutokana na ongezeko la kiwango kikomo katika awamu ya kwanza ya *program,* Halmashauri ya Songea imetengewa shilingi bilioni 1.154 ikiwa ni ongezeko la shilingi millioni 536.85 ikilinganishwa na kiwango au kikomo cha awali. Fedha hizo za nyongeza zitatumika kutekeleza miradi katika vijiji vya Mkongotema na Magingo.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuongeza swali la nyongeza, kwanza niipongeze sana Serikali kwa hatua ambayo imefikiwa lakini kwa kuwa muda wa wananchi kutathimini Serikali hii iliyopo madarakani unakaribia kwa maana ya mwaka, 2015.

Je, Serikali imeweka mikakati gani kuhakikisha kuwa miradi ya maji ya *Becken 100* inakamilika mapema kabla ya mwaka 2014?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kuipongeza Serikali, pongezi zake tunazichukua. Lakini tunayo mikakati, tunao mpango wa

miaka 15 ambao umegawa katika miaka ya vipindi vitatu vitatu vya miaka mitano na ambao tayari umeshaanza kutekelezwa. Katika mpango ule, inaonesha kwamba kufikia mwaka 2015 hali ya upatikanaji wa maji katika Vijiji itakuwa imefikia asilimia 65. Sasa hivi tunaamini kwamba kufikia mwaka 2013/2014 Vijiji 10 vitakuwa vimetekelezwa. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi imeonesha idadi ya Halmashauri ambazo zimepata kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naendelea kuwaomba Wabunge ni kuwa karibu na Halmashauri ili ziharakishe kutoa zile taarifa kwenye Wizara na hivyo Halmashauri zote zipate vibali tuingie kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa vijiji vingine 10.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa gharama halisi ya miradi ya maji iliyothaminiwa katika Halmashauri ya Namtumbo ya awamu ya kwanza, mgawo wa fedha za kutekeleza mradi huo hatujapata kama *design report* ilivyotafsiriwa, mgawo unatolewa kwa utaratibu maalum baada ya gharama halisi ya miradi yetu ya maji. Hivyo itasababisha miradi yetu ya awamu ya kwanza kuchelewa kutekelezwa.

Je, Serikali inaweza kugawa fedha hizo za kikomo kulingana na gharama halisi ya kitalaam?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Vita Kawawa kwa sababu Halmashauri yetu ya Namtumbo ni moja ya Halmashauri 103 zilizotajwa ambazo tayari zimeanza utekelezaji wa miradi hii ya maji vijiji 10. Fedha hizi zipo tayari kwenye Halmashauri na ili fedha ziweze kulipwa, inategemea kazi inayofanyika na yule Mkandarasi. Kila inapofikia hatua Fulani, yule Mkandarasi kuna Kamati ya Halmashauri ambayo inakwenda kujiridhisha na utekelezaji wake ndipo zile fedha zinaanza kulipwa. Kwa hiyo, kasi ya utekelezaji wa miradi hii itaongeza kasi ya kupeleka fedha katika ngazi ya Halmashauri kwa maana ya kulipa na katika ngazi ya Wizara kwa maana ya kupeleka kwenye Wizara baada ya kujiridhisha na utendaji uliopo kwenye miradi husika.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni dhahiri kwamba hata katika Halmashauri ambazo zilishapata kibali cha kuendelea kuchimba, ni kwamba wamechimba visima lakini hakuna maji. Hii ni ushahidi kwamba waliopewa kazi ya kufanya upembuzi yakinifu walipewa watu ambao walikuwa hawana uwezo wa kufanya hiyo kazi ambao ni moja ya ufisadi pia ambao unaendelea kwenye Serikali yetu.

Napenda kujua kwamba: Je, katika maeneo ambayo yamechimbwa visima na maji hayakupatikana, Serikali ina mpango gani wa ku-*compensate* hayo maeneo ili kama watapeleka pesa vichimbwe tena kwa sababu wao ndiyo walifanya kosa la kwanza la kuwapa watu ambao hawana

uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu, wakafanya upembuzi hewa, watu wanakwenda kuchimba maeneo ambayo hakuna maji? Serikali ina mpango gani wa kupeleka pesa ya fidia kwenye maeneo yote na kwenye Majimbo yote ambayo watu walichimba visima na maji hayajapatikana mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Jibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Ni kweli maeneo mengi yalichimbwa visima na havikupata maji. Lakini nilishaeleza hapa Bunge kwenye Bunge lako Tukufu kwamba katika miradi ile ya vijiji kumi ilikuwa ni miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za wafadhili na hivyo tulikubaliana kwenye taratibu za manunuzi kwamba, kunakuwa na usanifu, wanapatikana watalaam wale, na kunakuwa na usimamizi, anapita Mtalaam Mshauri. Katika eneo hili watalaam wengi hawakuwa na uwezo huo, na hawakuweza kushirikisha zile taarifa zilizopo kwenye Ofisi za Mabonde ya Maji ambako kuna Ma-*hydrologist* na *Geologists* ambao wana utalaam wa kujua ni maeneo gani yana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limetokea. La msingi ni kwamba hakutakuwa na fidia yoyote. Tutakachofanya kama Wizara, yale maeneo ambayo hayakupatikana maji sasa, kwa kutumia watalaam sahihi kama nilivyoeleza jana kwenye swali la msingi kwamba Halmashauri zichukue taarifa kwenye Ofisi za Mabonde na Watalaam wa Ofisi za Mabonde wafanye *survey* ya maeneo muhimu ambayo yanaweza kuwa na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama yale maeneo yatakuwa hayana maji tena, Wizara itaangalia vyanzo vingine ambavyo inaweza kuwa pengine ni mabwawa, inaweza kuwa pengine ni uvunaji wa maji ya mvua na maeneo mengine. Lakini bado Serikali itahakikisha kwamba wale wananchi wanapata chanzo kingine cha kupata maji. *(Makofi)*

Na. 73

**Ahadi ya Maji kwa Vijiji 10 - Bukoba**

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Serikali kwa kutambua umuhimu wa maji kwa watu wake, iliahidi kusambaza maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini kwa kuanzia na vijiji kumi ambavyo ni Bituntu, Kibirizi, Itongo, Lukindo, Katale, Kibona, Mashule, Kitahya, Ibwera na Kyamulaile, lakini ahadi hiyo bado haijatekelezwa: Je, ni lini vijiji hivyo vitapatiwa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabango Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa awamu za vipindi vya miaka mitano katika Halmashauri zote nchini kuanzia mwaka 2007 hadi 2025. Kwa kuanzia, kila Halmashauri

ilichagua vijiji 10 vya kipaumbele. Hadi tarehe 31 Oktoba, 2012, Halmashauri 103 zimepata vibali vyote kuanzia ujenzi wa miundombinu ya maji. Halmashauri 19 zimepata vibali vya kutangaza zabuni za ujenzi na Halamsahauri nane zimepata wataalamu washauri wa kusanifu miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini imekamilika usanifu wa miradi katika vijiji 10 walivyochagua kama kipaumbele vyao ambavyo ni Bintuntu, Kibirizi, Itongo, Lukindo, Katale, Kibona, Mashule, Kitahya, Ibwera na Kyamulaile. Katika awamu ya kwanza ya programu, Halmashauri itatekeleza miradi katika vijiji vinne vya Mashule, Kyamulaile, Kitahya na Kibona. Mkandarasi wa ujenzi kwa ajili ya Kijiji cha Mashule alianza ujenzi tarehe 18 Juni, 2012 na anatarajia kukamilisha kazi ya ujenzi wa mradi tarehe 8 Desemba, 2012. Hadi sasa, utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 60. Aidha, Halmashauri inafanya makubaliano na mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kijiji cha Kyamulaile ili mkataba usainiwe na kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri inaendelea na taratibu za kutangaza zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi katika vijiji vya Kitahya na Kibona. Vijiji hivyo ni vya nyongeza baada ya Halmashauri kuongezewa kiwango cha kikomo katika awamu ya kwanza ya programu. Ujenzi wa miradi katika vijiji sita vilivyobaki utafanyika katika awamu ya pili ya programu.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa ni asilimia 54 tu ya wakazi wa Bukoba Vijijini wanapata maji safi, na hii inasababisha wanawake na watoto kutumia muda mrefu wakitafuta maji muda ambao ungetumika kwenye shughuli nyingine za maendeleo; napenda Serikali inieleze: Je, wana mipango gani kuwapatia maji wananchi ambao wapo kwenye vijiji vingine ambavyo haviko katika mradi wa vijiji 10?

(b) Katika miaka ya 70 na themanini, tulikuwa na vijiji vinapata maji salama na safi na miundombinu mpaka leo ipo, lakini inahitaji ukarabati mkubwa. Kwa mfano, kulikuwa na *pumping schemes* na *gravit scheme* katika sehemu za Maruku, Kanyangareko, Katoma Gera, Izimbya, Rugazi, Nyakato na Igombe: Je, Serikali inawaahidi nini sasa hao wananchi? Naibu Waziri upo tayari sasa kuja Mkoa wa Kagera Bukoba ufanye tathmini ikiwezekama tuambatane ili kusudi hii miradi iweze kukarabatiwa na watu waweze kupata maji safi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza kwa ufuatiliaji wa karibu wa miradi ya maji katika Mkoa wa Kagera.

Swali la kwanza kwamba tuna mikakati gani ya kupeleka maji kwenye vijiji vingine zaidi ya vijiji vile kumi, nimesema kwamba tunao mpango wa miaka 15 ambao upo katika vipindi vitatu vya miaka mitano mitano na kwa awamu ya kwanza tunatarajia mwaka 2015 tutafikisha maji vijijini kwa asilimia 65. Maana yake 65 haina maana ya vijiji vile kumi tu, vitakuwa vimeongezeka na vingine. Kuanzia

mwaka 2015 tutaanza kuongeza vijiji zaidi ili kufikia kiwango kikubwa kwenye usambazaji maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, ukarabati wa miundombinu, Wizara yangu itaendelea kutenga fedha jinsi inavyopatikana kuhusu ukarabati wa miundombinu, lakini niziombe Halmashauri baada ya kufanya ziara, tumegundua kwamba Halmashauri haziweki mipango ya maji kwenye shughuli za maendeleo kama wanavyoweka kwenye kilimo, elimu na mambo mengine. Wapange kwenye bajeti zao kwa ajili ya miradi ya maji ili isaidiane na juhudi zinazofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwenda kutembelea, tuko tayari, tutaambatana naye kwenda kuangalia hali halisi ya maji. *(Makofi)*

**MHE. SUZAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, suala la maji ni tatizo kubwa katika Mji Mdogo wa Ifakara na walishaandika andiko kuomba hela ya upembuzi kwenye chanzo cha Kiburubutu karibu Shilingi milioni 500.

Wananchi wa Ifakara wanataka kujua, ni lini Serikali itatoa hiyo hela ili kufanya upembuzi yakinifu kwenye hicho chanzo cha maji na baadaye kupeleka hela za upatikanaji wa maji kwenye Mji Mdogo wa Ifakara, na Mheshimiwa Mwanri anaijua sana hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi, ni lini mtapeleka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu swali hili amelikumbushia hata Bunge lililopita, tunaendelea kulichukua. Tukipanga bajeti tutaingiza hizo fedha ili kuweza kusaidia usanifu wa huo mradi wa maji katika sehemu husika. *(Makofi)*

Na. 74

**Serikali Kuwekeza katika Michezo**

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH** aliuliza:-

Michezo ni sekta muhimu nchini na inaweza kuleta faida nyingi kama vile kuongeza mapato ya Taifa, kuitangaza nchi yetu na kutoa ajira kwa vijana wengi:-

Je, Serikali itawekeza lini katika michezo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba michezo ni sekta muhimu katika jamii mahali popote duniani katika Nyanja za uchumi, afya, jamii na hata kisiasa. Kwa kutambua umuhimu huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianza kuwekeza katika michezo tangu ilivyojipatia uhuru. Kwanza, Serikali iliunda Wizara

iliyokuwa na dhamana ya kuendeleza michezo mwaka 1962 na mwaka 1967 kupitia Bunge lako Tukufu ikatengeneza Sheria ya Baraza la Michezo ya Taifa na kuifanyia marekebisho mwaka 1971.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa michezo, Serikali ilichukua hatua na viwanja vingi vya michezo vilijengwa kila Mkoa. Kuanzia mwaka 1990 mpaka mwaka 2012 Serikali ilianza kuwekeza katika mafunzo ya watalaam wa michezo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na Vyuo vingine vya vya Ualimu. Mradi huu ulifadhiliwa na Serikali ya Finland na umefanikisha kuzalisha walimu wa michezo zaidi ya 400.

Aidha, Serikali imewekeza katika ujenzi wa eneo changamani la michezo lililopo Dar es Salaam ambalo mpaka sasa Serikali inaendelea kutafuta wawekezaji na wafadhili wa kukamilisha ujenzi wa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuwekeza katika michezo kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu ili kuwezesha pato la Taifa na ajira kwa vijana kukua zaidi.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inajua umuhimu wa sekta hii ya michezo, na kwa kuwa sekta hii bado haijapewa

kipaumbele, ni lini Watanzania wategemee faida kutokana na sekta hii ya michezo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema ni kwamba, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, Serikali inathamini juu ya kuendeleza michezo na tulianza na miundombinu, lakini pia tuna programu mbalimbali za kuibua vipaji vya vijana kuanzia miaka sita mpaka 12 na upo mradi wa *FIFA* ambao utaanza mwakani utakaowashirikisha vijana katika sekondari zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba Serikali imejiandaa na ninawaomba Wabunge na wadau mbalimbali tushirikiane katika kuwekeza katika michezo ili tuweze kuendeleza michezo zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba mniwie radhi, maswali ni mengi. Naomba niendelee na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 75

## Bidhaa Chakavu za Elektroniki

**MHE. WARIDE BAKAR JABU** aliuliza:-

Bidhaa chakavu za kielektroniki ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kudhibiti bidhaa hizo kutoka nje ili Tanzania isifanywe jalala la kutupia bidhaa za aina hiyo?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuangamiza vifaa chakavu vya aina hiyo ambavyo sasa vimezagaa kila sehemu ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jabu, lenye sehemu (a) na (b), napenda kwanza nikubaliane naye kwamba bidhaa chakavu ikiwemo zile za kieletroniki zinazotumika katika teknolojia ya mawasiliano, visipohifadhiwa vizuri vinaweza kuhatarisha afya za binadamu na mazingira. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kwenye vifaa hivi kuna kemikali nyingi ambazo ni hatari kwa viumbe hai na mazingira. Hata hivyo, ukiwekwa utaratibu mzuri, upo uwezekano wa kemikali hizo kutolewa kwenye vifaa hivyo na kuvitumia kutengeneza bidhaa nyingine, yaani *recycling*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Sera ya Taifa ya Mazingira *(National Environment Policy)* ya mwaka 1997 inatambua changamoto za bidhaa ngumu zilizo chakavu *(solid waste)* na imetoa matamko mbalimbali kukabiliana nayo. Aidha, Sheria ya Menejimenti ya Mazingira *(The Environment Management Act)* Na. 20 ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake za bidhaa ngumu, yaani *Environmental Solid Waste Management Regulation of* 2009 na *The Environmental Management Hazardous Waste Control and Management Regulations* 2009, zinaeleza kwa ujumla kuhusu udhibiti wa bidhaa hizo chini ya Baraza la Utunzaji wa Mazingira *(NEMC)*.

Kwa kutambua kwamba suala hili pia linahusu Sekta ya Mawasiliano, Wizara yetu kuanzia mwezi Mei mwaka huu 2012 imeanza kuihuisha Sera ya Taifa ya Teknolojia Habari na Mawasiliano *(TEHAMA)* ili kulipangia mkakati maalum katika sekta. Siyo tu kudhibiti pekee, bali kuweka mpango maalum wa kuzitumia upya bidhaa zilizokwisha muda wake *(recycling of e-waste products)* na kuziuza baada ya kufanyiwa uzalishaji upya.

Mkakati huu utasaidia sana kutengeneza ajira kwa wananchi wengi na hivyo kuongeza kipato kwa wajasiriamali hapa nchini na Taifa kwa ujumla. Hivyo napenda kuchukua fursa hii pia kuwasihi Waheshimiwa Wabunge kutoa mchango wao katika utungaji wa sera mpya ya *TEHAMA* na pia kushiriki vilivyo katika utekelezaji wake.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuangamiza bidhaa zilizozagaa hapa nchini, Serikali itaendelea kutumia Sheria ya Menejimenti iliyopo na kwa kufuata miongozo ya

Kitaifa na ya Kimataifa katika kuhifadhi na kuangamiza bidhaa hizo. Pamoja na uwepo wa Sheria ya Mazingira, napenda kuzisihi Halmashauri zote nchini ambazo Wabunge ni Wajumbe wa Mabaraza hayo kuweka mkakati maalum na utaratibu kulingana na miongozo ya mazingira ya kuangamiza bidhaa hizo chakavu. Ni matarajio yangu kwamba pindi zera mpya ya *TEHAMA* itakapokuwa tayari sekta ya *TEHAMA* itatoa ushirikiano wa kutosha kwa sekta ya mazingira ili kulipatia ufumbuzi tatizo la menejimenti ya vifaa chakavu hapa nchini kwa maendeleo ya Taifa letu.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa vifaa hivi vya elektroniki visivyohifadhiwa vizuri vinaweza kuleta madhara kwa afya ya binaadamu na mazingira; nataka kujua: Je, Serikali ina mpango gani au mkakati gani wa kununua mtambo wa kuangamiza bidhaa hizi za elektroniki?

(b) Lakini pili, napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri: Je, Serikali ina mpango gani wa kuelimisha wananchi kuhusiana na madhara yatokanayo na bidhaa hizi za elektroniki? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jabu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inatumia utaratibu uliowekwa kwenye Sheria ya Mazingira kuangamiza bidhaa hizi, ambayo kwa sehemu kubwa ni kufukia bidhaa hizi katika utaratibu ambao utahifadhi vyanzo na mkondo wa maji.

Kama tunavyofahamu kwamba chini ya ardhi ndipo ambapo vyanzo vingi vya maji vinapatikana, lakini tunalichukua wazo la kupata mtambo kwa ajili ya kuangamiza bidhaa hizi na tunapenda kuzihimiza sekta binafsi vile vile ziwekeze katika shughuli hii. Lakini cha kwanza kabla ya mtambo ni kutenganisha kwa sababu katika hizi bidhaa zipo sehemu nyingi, kwa mfano plastiki, lakini vile vile ziko kemikali. Kwa hiyo, ni kuzitenganisha kwanza kwa sababu zile plastiki kwa mfano kwenye *TV* zinaweza kutumika kwa ajili ya kutengeneza vitu vingine. Kwa hiyo, wazo hilo tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Kuhusu kuelimisha Umma, tunaendelea na tumeweka mipango kwa kushirikiana na *NEMC* kuhusu suala zima la utunzaji wa mazingira, lakini vile vile kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Nchini kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya bidhaa hizi na zipo hatua mbalimbali ambazo tunachukua. Kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge kila mmoja akienda nyumbani kwake akiangalia idadi ya *charger* alizonazo katika *solid waste*, *waste* nyingi kuliko zote ni *charger* na tukikusanya *charger* zote hapa tulizowahi kuzitumia, zinafika malori matatu au zaidi.

Kwa hiyo, utaratibu uliowekwa sasa hivi tangu mwaka 2010 ni kuhakikisha kwamba simu za aina zote zinazotengenezwa zinatumia *charger* ya aina moja ili kusiwe na haja ya kila unaponunua simu, basi uwe na *charger* mpya ili kuongeza sasa ma-*charger* ambayo yanaongeza tatizo hili la hii *waste*.

Na. 76

**Tatizo la Wanyama Waharibifu**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI** aliuliza:-

Wanyamapori waharibifu hususan Nyati katika Kata ya Nyaluhande limekuwa ni tatizo sugu la muda mrefu ambapo kila mwaka mazao ya wananchi huharibiwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kumaliza tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii inatambua tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba. Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hilo, Wizara ina mpango wa muda mfupi na muda mrefu ili kuhakikisha

inapunguza kwa kiwango kikubwa cha tatizo la wanyamapori waharibifu katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kata ya Nyaluhande kama ifuatavyo:-

(i) Kuendesha doria za msako na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kushirikiana na Halmashauri zetu za Wilaya;

(ii) Kutambua shoroba na mapito ya wanyamapori ili wananchi wahamasishwe kutofanya shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo;

(iii) Kuendelea kutoa Mafunzo ya Uaskari wa Wanyamapori kwa wananchi wa Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ili kushiriki katika doria za msako wa wanyamapori wakali na waharibifu;

(iv) Kuendelea kufanya utafiti wa kutumia mbinu mbadala za kufukuza wanyamapori wakali na waharibifu; na

(v) Kuhamisha Halmashauri za Wilaya kuandaa Mipango Bora ya Matumizi endelevu ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inampongeza sana Mheshimiwa Kamani katika jitihada zake na ushirikiano katika kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa salama dhidi ya tishio la wanyamapori hatari. Aidha, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote na wadau wengine wa maliasili wawahamasishe wananchi wazingatie Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi iliyopo katika maeneo yao kwa kuishi na kuweka makazi mbali na kwa mujibu wa mipango

hiyo ili kupunguza au kuepukana na athari za wanyamapori waharibifu.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilipenda kufahamu tu kwa sababu kwa kuwa fidia au kifuta jasho ambacho kinatolewa kwa wananchi baada ya mazao yao kuharibiwa, utaratibu wake unachukua muda mrefu sana na hivyo kupoteza thamani:-

(a) Serikali ina mpango gani wa kuweka mfumo ambao utarahisisha upatikanaji wa fidia hizo ili wananchi ambao wameshaharibiwa mazao yao kule Nyaluhande kwenye Kata ya Ngasamo, Lamadi, Lutubila na Mkura waweze kupata stahili zao? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa wanyama ambao wanasumbua katika Kata hii ya Nyaluhande ambao ni nyati, wanatoka katika Hifadhi ya Msitu wa Sayaka ambayo kimsingi, iko mbali sana na Hifadhi yoyote ya wanyamapori; sasa na Hifadhi ya Msitu ni ya mimea, sio kwa ajili ya wanyama, Serikali itakuwa tayari sasa kuruhusu wananchi wawawinde wale wanyama wote, wale nyati ili wananchi wawe salama na mazao yabaki salama? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwanza, fidia itaendelea kulipwa kama ambavyo imeendelea kulipwa kwa mujibu wa kanuni

zilizopo chini ya Idara yetu ya Wanyamapori. Ninachokubaliana na Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, Serikali itaangalia kila kinachowezekana ili hizi fidia ziwe zinatolewa kwa wakati na tuangalie vipingamizi vya kiutendaji ambavyo vimekuwa vikichelewesha fidia hii ambayo ipo kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa kanuni.

Pili, wanyama hawa waharibifu kama wanatoka katika msitu wa jirani ama kama wanatoka katika maeneo yetu ya Hifadhi za Mapori ya Akiba, ni muhimu sana watu wakafahamu kwamba uwindaji wa wanyamapori ni lazima na sharti uendane na sheria zilizopo za wanyamapori chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na hivyo ili kuepukana na madhara yanayotokana na wanyama waharibifu.

Kama alivyosema Mheshimiwa Kamani, nakubaliana naye kabisa kwamba tuna maeneo ambayo wananchi wamedhurika kutokana na athari zinazotokana na wanyama waharibifu, Serikali inafanya kila uwezekano wa kuhakikisha kwamba kwanza tunafanya misako ya hawa wanyama na nimesema kwamba tunatafuta njia nyingine mbadala za kisayansi zaidi ambazo zinaweza kutusaidia kuwafukuza hawa wanyama wasiwadhuru wananchi na pale ambako madhara yanatokea, Wizara yangu iko tayari kwa kushirikiana na Mamlaka zinazohusika kutoa fidia kwa haraka iwezekanavyo.

Na. 77

## Fursa za Ajira kwa Vijana Mkoa wa Arusha katika Mbuga za Wanyama

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Licha ya Mkoa wa Arusha kuongoza kwa kuwa na mbuga nyingi za wanyama Tanzania, lakini vijana wengi wa Mkoa huo hawana ajira.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijana wa Mkoa huo wanapatiwa fursa ya ajira katika Hifadhi hizo ili kuinua uchumi wa vijana na Taifa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za ajira katika Hifadhi za Taifa zinatolewa kwa usawa kabisa kwa vijana wote nchini wenye sifa na ujuzi wa kufanya kazi husika kwa mujibu wa taratibu za Ajira za Mashirika na Taasisi za Umma. Aidha, vijana wa Mkoa wa Arusha wanazo fursa za kufanya kazi katika Sekta ya Utalii zinazotokana na sekta binafsi na kuweza kujipatia kipato kwa ajili yao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/2012, jumla ya watalii 867,994 walitembelea nchini Tanzania, ambako kati yao, watalii 52,641 walipanda Mlima Kilimajaro. Katika kipindi hicho, utalii uliingiza nchini Dola za Kimarekani bilioni 1.32 na kuwezeshesha upatikanaji wa ajira unaokadiriwa kufikia ajira milioni 1.1, hizi ikiwa ni ajira za kudumu na ajira za muda mfupi na ni sawa na asilimia 11 ya ajira zote zilizopatikana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inawahamasisha vijana wote nchini, ikiwa ni pamoja na vijana wa Mkoa wa Arusha, watumie fursa zilizopo kupata taaluma zitakazowawezesha kupata sifa za kuajiriwa katika Sekta ya Utalii nchini. Fursa hizo ni pamoja na kujiunga na Vyuo mbalimbali vilivyoko hapa nchini kama Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka, Chuo cha Taifa cha Utalii, Vyuo mbalimbali vya *VETA*, Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi; na Vyuo Vikuu mbalimbali nchini vinavyotoa Stashahada na Shahada katika tasnia ya Utalii hapa nchini.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa vijana wengi wa Mkoa wa Arusha wamepitia katika mafunzo ya JKT na Mgambo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira kama za Askari wa Wanyamapori katika Hifadhi zetu? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Mkoa wa Arusha una maeneo mengi sana ya wazi, kwa nini Serikali isitenge maeneo maalum

kwa ajili ya vijana na akina mama wanaojishughulisha na biashara za utalii ili waweze kufanya biashara zao vizuri na kujipatia kipato kwa wingi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

(a) Moja, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Magige kwamba nchi yetu inahitaji kuajiri Maaskari wengi sana wa wanyamapori na Tanzania inapitia msukosuko mkubwa wa tishio la ujangili nchini katika maeneo mengi ya mapori yetu ya akiba na hata ndani ya maeneo ya hifadhi za Taifa na Wizara yangu tayari inaendelea kushirikiana na Mamlaka nyingine zinazohusiana ili tuweze kupata kibali cha kuongeza ajira kwa vijana ambao wamemaliza mafunzo husika na tutalifikiria hili wazo la vijana ambao wamemaliza mafunzo ya JKT kama sehemu ya watu ambao tutawafikiri katika kuwaajiri katika tasnia hii ya Uaskari wa Wanyamapori.

(b) Tunawasisitiza vijana wote wa Mkoa wa Arusha na vijana wote nchini wachukue fursa za ubunifu mahali ambako kuna maeneo ya wazi mahali ambako wangeweza kuja na mapendekezo ni jinsi gani wanaweza kushiriki kuchukua fursa zilizopo katika utalii kama ni kuanzisha kikundi cha kuuza vinyago kama ni kuanzisha vikundi vya kupeleka mazao mbalimbali ya kilimo katika mahoteli mbalimbali yaliyoko nchini katika Hifadhi na kwingineko. Serikali iko tayari kabisa kushirikiana nao.

Tungependa kuona ubunifu wao na hawa ni kwa vijana wa Arusha na vijana popote waliko nchini.

Na. 78

## Kupeleka Boti ya Doria Kipili

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Kumekuwa na vitendo vingi vya uharamia mwambao mwa Ziwa Tanganyika hususan katika Vijiji vya Wilaya ya Nkasi:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka boti ya kisasa eneo la Kipili kwa ajili ya doria katika vijiji vya Wilaya ya Nkasi?

(b) Je, ni lini Mkutano wa ujirani mwema kati ya Wilaya ya Nkasi na Wilaya ya Moba *-DRC* utafanyika kuzungumzia suala zima la uharamia kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi katika mpango wake wa maboresho limepanga kutafuta boti ya kisasa itakayofanya kazi kwa ufanisi zaidi katika eneo la

Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Aidha, kwa sasa Jeshi la Polisi lina boti moja na pia Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina boti moja aina ya *Fibre* ambayo hutumiwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya doria Ziwani.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikutano ya Ujirani Mwema kati ya Wilaya ya Nkasi na Wilaya za mpakani mwa nchi za Burundi na Zambia hufanyika mara kwa mara. Ushirikiano huu umesaidia sana kupunguza uhalifu katika maeneo mbalimbali ya Ziwa Tanganyika. Kwa upande wa Tanzania na nchi ya *DRC*, mikutano ya namna hii haijafanyika, ingawa hatua za makusudi zinafanywa na Serikali ili kufanikisha mkutano baina ya Wilaya ya Moba *(DRC)* na Wilaya ya Nkasi (Tanzania).

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Majibu aliyoyatoa Naibu Waziri hayakufanyiwa utafiti. Kituo cha Polisi Marine kinahudumia toka Karema Wilaya ya Mpanda mpaka Kasanga Wilaya ya Sumbawanga, karibu Vijiji 60 na baadhi ya Visiwa.

Mheshimiwa Waziri ameelezea kuhusu boti ya *Fibre.* Hiyo boti ya Fibre mimi ndio Mbunge wa Wilaya ya Nkasi, wana mtumbwi wa *Fibre* lakini *engine* zote Halmashauri ya Nkasi ni mbovu na hata siku moja hawajafanyia doria hizo boti. Hizo boti zinafanya doria kwa ajili ya wavuvi kuangalia nyavu salama au nyavu makokoro. Makokoro siyo kwa ajili ya doria kukamata majambazi. Majambazi yanatoka *DRC - Congo* kuja kudhuru watu wetu. Swali:-

(a) Nani alimpa hilo jibu ambalo sio la uhakika?

(b) Lini mara ya mwisho aliwasaidia hata Polisi Marine Kipili lita hata moja ya mafuta ili waweze kuazima hata *engine* au boti yoyote kwa mtu wa raia mwema ili kupambana na majambazi. Lini mara ya mwisho uliwapelekea hata lita moja ya mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Keissy, kama ifuatavyo:-

(a) Jibu la swali hili nimelitayarisha mwenyewe.

(b) La pili ni kwamba ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Keissy kwamba Boti ambayo ipo ya *Fibre, mashine* yake imeharibika, ni mbovu. Lakini naomba nimthibitishie kwamba ni sahihi kusema kwamba Polisi walikuwa nayo boti ambayo imeharibika na *engine* yake ndiyo inatumika kufanya *joint operations* kwa kutumia boti hiyo. Boti kubwa ambayo ipo ambalo tatizo lake kubwa ni mafuta, imekaa pale *stand by* ili wale ambao wanafanya *patrol* wakitoa taarifa ndiyo iweze kufuatiliwa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajajibu alipeleka lini mafuta hata lita moja mara ya mwisho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy naomba ukae chini. Tunaendelea na swali namba 79, Mheshimiwa Hebert James Mntangi atauliza.

Na. 79

**Ujenzi wa Nyumba za Askari- Muheza**

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE (K.n.y. MHE. HERBERT J. MNTANGI)** aliuliza:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Kituo cha Polisi Muheza na wafanyakazi zitajengwa katika eneo hilo?

(b) Je, ni lini ukarabati wa Kituo kidogo cha Polisi Amani utafanyika na kuwapatia vifaa vya usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hebert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mpango wa kujenga nyumba ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya *(OCD),* Mkuu wa Kituo *(OCS)* pamoja na nyumba za kuishi Askari Polisi Muheza. Nia hii ni nzuri, bado inakwamishwa na upungufu wa rasilimali fedha. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Jeshi la Polisi halijatenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba. Hata hivyo, mradi huu wa Muheza

utategemea upatikanaji wa fedha katika wa bajeti ijayo ya mwaka 2013/2014.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Amani kwa sasa kipo kwenye jengo ambalo ni mali ya Shirika la Mamlaka ya Chai Amani. Serikali haina mpango wa kukifanyia ukarabati mkubwa Kituo hiki kwa vile siyo mali ya Polisi na badala yake tumeazimia kujenga Kituo kipya mara fedha itakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kumwomba Mheshimiwa Mntangi kuwahamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa Kituo hicho. Aidha, nitumie fursa hii pia kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuwahamasisha wananchi kujenga Vituo vya Polisi kwenye maeneo yao kama inavyofanyika katika ujenzi wa Shule, Zahanati na Vituo vya Afya hapa nchini.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa pale Muheza, wafanyakazi wake wote wanaishi katika maeneo ya nyumba ambayo awali zilikuwa mali za Shirika la Reli la Afrika Mashariki, ambazo sasa zinamilikiwa na Shirika la Reli la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yetu ni kwamba, wabadilishe Hati sasa, kwa sababu, Shirika la Reli pale halina kabisa wafanyakazi. Je, utaratibu huu na mapendekezo ya kubadilisha Hati ili wayamiliki yale na kuweza kufanyia ukarabati nyumba zile, umefikia wapi? Kwa sababu, nimeshawahi kutoa mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu Kituo cha Amani. Ni kweli, Kituo cha Amani kilijengwa na wamiliki wa mashamba, lakini walijenga ili wakikabidhi Serikalini, na hawahitaji kuwa na Kituo kwa sababu, kazi ya ulinzi iko mikononi mwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, haioni kama ipo haja, badala ya kujenga kituo kingine au kuchukua muda mrefu, kuomba wakabidhiwe Kituo hicho na wafanyie ukarabati wao wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa ushauri ambao nataka nimhakikishie kwamba, tutaufuatilia kwa upande wa reli na kwa upande wa Chae.

Rai ni nzuri na mimi mwenyewe nitachukua hatua ya kwenda kuonana nao ili kuona uwezekano wa kubadilishana majengo haya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, Swali la Nyongeza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,... *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Aah, samahani. Mheshimiwa Sakaya, samahani!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kituo cha Wilaya Mpya

ya Kaliuwa kina hali mbaya sana; ni kidogo, hakina huduma na pia Askari wake wote akiwemo *OCD,* wanaishi *Guest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapanua kile Kituo cha Wilaya Mpya ya Kaliuwa na pia kujenga nyumba za watumishi akiwemo *OCD* ambaye anaishi *Guest* mpaka hivi ninavyoongea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Vituo na Nyumba za Askari ni kubwa na kutegemeana na bajeti ni kazi ambayo haitawezekana katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, inafanya mazungumzo na wadau mbalimbali ili kuweza kupata ufumbuzi katika miundombinu hii kwa kutumia mitindo ya *PPP,* na kadhalika. Hata mkopo, bado mawasiliano yanaendelea na Taasisi mbalimbali. Tuna matumiani kwamba, tukimaliza mazungumzo haya *positively,* tutakuwa na uwezo wa kutimiza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kabla hatujatimiza, pamoja na bajeti ndogo tuliyonayo, ninasisitiza Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane kuhamasisha wananchi, ili tusaidiane. Hii ndiyo Polisi Jamii tunayozungumza.

Na. 80

## Muda Unaotumika Kupata Mkopo wa Benki

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED** aliuliza:-

Je, kwa kawaida kama taratibu zote zimekamilika, mwombaji wa mkopo kwenye Benki za Biashara, hutakiwa kupata mkopo wake baada ya muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa wateja kupata mikopo baada ya taratibu zote kukamilika unatofautiana kati ya benki na benki kutegemeana na sera na taratibu za utoaji mikopo za Benki husika. Kwa mfano, kwa mkopo wa biashara, Sera ya *CRDB* inatamka kuwa ni siku 21; Benki M *Tanzania Limited* inatamka kuwa ni siku saba; *NBC* siku 30; *NMB* siku 14; na *Bank of Africa* siku 30. Mkopo binafsi mara nyingi hutolewa ndani ya siku saba au wiki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni *NMB* ambayo hukamilisha mkopo binafsi ndani ya saa 24. Hata hivyo, muda uliowekwa kisera kwa kila Benki unaweza kupungua au kuongezeka kulingana na mazingira yaliyopo kati ya mwombaji na benki husika, aina ya biashara na uthibitisho wa nyaraka zinazohitajika kama vile dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali, tunatarajia kuona kwamba msukumo wa nguvu ya soko utayasukuma mabenki kuimarisha sera na taratibu zao za kutoa mikopo na hivyo kuwawezesha wateja wao kupata mikopo kwa wakati.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa takwimu alizozitoa Mheshimiwa Waziri zinazungumzia zaidi mikopo binafsi, kwani, hata Serikali inapokopa katika mabenki, hakuna hata benki moja imethubutu kuipa hata Serikali, acha mtu binafsi, muda usiopungua miezi saba au nane.

Je, uko tayari kwenda kufanya utafiti wa kina kujua kwamba kweli hizi siku walizozitaja kwamba kweli mteja anaweza kupata mkopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mikopo hii aliyoitaja Mheshimiwa Waziri ambayo inapatikana kwa siku saba au nane, ni mikopo ambayo haina *risk* kubwa. Yaani Benki haina tatizo la kupata udhamini. Kwa mfano, mfanyakazi anajidhamini kwenye mshahara wake na mteja wake anamdhamini na ndiyo sababu Benki zinatoa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, benki hiyo hiyo inatoza riba kubwa sana kwa wafanyakazi na hata hapa kwa Wabunge wanaokopa. Je, ni sababu zipi za msingi, wakati hakuna *risk* yoyote ya kukopa, benki zikaendelea kuchukua riba kubwa kwa wakopeshwaji

ambao hakuna *risk* yoyote kwa benki? Kuna sababu, yoyote ya msingi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nafikiri siyo maswali mawili, ni matatu. Ni kwamba takwimu nilizozitoa ni takwimu ambazo nimezipata kwa mabenki husika moja kwa moja kwa kuongea nao baada ya kwenda kuwaona. Wamenihakikishia kuwa hizo ndiyo *time* ambazo wanatumia kushughulikia mkopo ambao umekamilisha kila kitu mpaka kupata mkopo. Zile siku saba ndiyo za mikopo binafsi. Mwezi mmoja au siku saba nyingine kama kwa Benki *M,* ni mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba naweza nikafuatilia zaidi kwa kina. Nafahamu vilevile kuwa, kuna mikopo mingine inachukua muda mrefu zaidi. Lakini hiyo ni michache kuliko ile ambayo ni ya kawaida, ambayo inachukua muda mfupi ambao nimeutaja mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya mkopo wenyewe ndiyo husababisha ni kwa nini ichukue muda mrefu. Kuna mikopo ambayo, kwa mfano mtu anataka kukopa *machinery,* kuna masuala ya ufuatiliaji, kuhakiki mambo mbalimbali ya *importation* na vitu kama hivyo. Kuna masuala vilevile ya kuangalia *terms* mbalimbali za dhamana ambazo zinawekwa. Kuna kufuatilia hizo dhamana kama kweli zipo, kama zinafaa na kuzitathmini, na kadhalika. Kwa hiyo, inaweza ikasababisha mkopo ukachukua muda mrefu. Lakini kwa kawaida, viwango vilivyotajwa ni vile vya mkopo ambao hauna matatizo mengi kama Mheshimiwa Mbunge, alivyotaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mikopo ya binafsi au mikopo ambayo inadhaminiwa na Mwajiri au inayowekewa dhamana za mteja mwenyewe, ni kweli kuwa haina *risk* kubwa. Lakini kuna gharama vilevile za kibenki ambazo zinaendelea kutumika katika ku-*process* mikopo hiyo. Ni lengo la Serikali kwa kweli kuhakikisha kuwa kadiri tunavyokwenda, mikopo inazidi kuwa na riba ndogo zaidi ili watu wengi zaidi waweze kufikiwa na hizo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni suala ambalo tunaendelea kulifanyia kazi. Kwa sasa hivi, hivyo ndivyo viwango ambavyo vipo. Napenda kufikia hapo.

Na. 81

**Halmashauri Kukopa Katika Miradi ya Maendeleo**

**MHE. ISMAIL A. RAGE** aliuliza:-

(a) Je, ni utaratibu upi unaotumika Kisheria kwa Halmashauri kukopa katika Miradi ya Maendeleo?

(b) Je, mpaka sasa Serikali, imedhamini Halmashauri gani na Halmashauri zipi zimefaidika na mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa ujumla, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kudhamini mikopo zinasimamiwa na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Na. 30 ya Mwaka 1974 na iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Mwaka 1974 na Marekebisho yake ya Mwaka 2004, Kifungu Na. 13, kinampa mamlaka Waziri wa Fedha kutoa dhamana kwenye Halmashauri za Serikali za Mitaa kwa niaba ya Serikali, baada ya kushauriwa na Kamati ya Taifa inayosimamia madeni na vilevile baada ya kujiridhisha kwamba, mkopo unaokopwa ni kwa maslahi ya Taifa na kwamba, Halmashauri, ina uwezo wa kurejesha mkopo na riba kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imetoa dhamana kwa Halmashauri mbili tu ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, iliyokopa Shilingi bilioni 10 kutoka kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, *NSSF.* Fedha hizi zilitumika kugharamia mradi wa Jengo la Wafanyabiashara, maarufu kwa jina la *Machinga Complex.*

Pili, ilikuwa ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya, iliyokopa Shilingi bilioni 13 kutoka Benki ya *CRDB.* Fedha hizi zilitumika kugharamia mradi wa ujenzi wa soko la Mwanjelwa.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, atakubaliana na mimi kwamba hii Sheria Na. 30 ya mwaka 1974 na marekebisho madogo ya mwaka 2004, imepitwa na wakati? Kwa sababu, sasa hivi Halmashauri zote ziko

chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kwa nini zisidhaminiwe na Ofisi ya Waziri Mkuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa mmeshawahi kudhamini mikopo ya Mbeya kwa *CRDB,* kwa nini msiruhusu benki ambazo zinaelewa miradi ambayo haihitaji udhamini wa aina yoyote zikatoa mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *CRDB* wako tayari kutoa mikopo kwa ajili ya upimaji wa viwanja kwa sababu ni mikopo inayolipika haraka sana. Je, Wizara iko tayari sasa kuruhusu Halmashauri ziweze kupata mikopo katika Benki hizo bila kupata Kibali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama Sheria hii imepitwa na wakati, ingawa vilevile haizui kujadili kama inahitaji kurekebishwa. Hilo nitawaachia wanaohusika na masuala ya kupitia Sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwa nini tusiruhusu, au kwa sababu, Halmashauri ziko chini ya Waziri Mkuu, ni kwa nini Ofisi ya Waziri Mkuu isidhamini? Masuala yote yanayohusiana na fedha Kisheria na Kikatiba, yako chini ya Wizara ya Wizara ya Fedha. Kwa hali hiyo, inabidi Wizara ya Fedha ndiyo idhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni kwa nini tusiruhusu Benki kama *CRDB* kutoa mikopo kwa ajili ya upimaji wa viwanja ilhali yenyewe ipo radhi kufanya hivyo; napenda kusema kwamba, Benki ya *CRDB* au benki nyingine yoyote inaruhusiwa kutoa mikopo, lakini kinachofahamika ni kuwa,

Benki yenyewe ya *CRDB* na Benki nyingine, ndizo zinazokuja Serikalini kuomba *guarantee* kabla hazijatoa mikopo kwa Halmashauri. Lakini kama Benki iko radhi kutoa huo mkopo kwa *risk* yake yenyewe, mimi siamini kama sisi tutakuwa na kipingamizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Muda wa Maswali umekwisha. Nawaomba radhi sana kwamba, kila mmoja ameleta kipeperushi hapa kuomba aongee. Sasa inakuwa taabu kidogo, naombeni radhi sana.

Waheshimiwa, nina matangazo yafuatayo:-

Kwanza, tuna wageni kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Tunaye Ndugu Ludovick Utoh - Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Karibu sana Bungeni na hongera kwa kazi nzuri kwa Taifa, unazozifanya. *(Makofi)*

Pia tuna Dkt. Patrick Makungu, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo. Tunao Wanakwaya 36 kutoka Kwaya ya Mtakatifu Gaspa, Dodoma. Popote mlipo msimame! Karibuni kwenye Bunge lenu. *(Makofi)*

Tunao pia Wachungaji 26 kutoka Chuo cha Biblia Dodoma. Popote walipo wasimame! Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga ambao ni Wanafunzi 11 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe na Jordan, Morogoro. Popote walipo wasimame! Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni wa Mheshimiwa Richard Ndassa, ambao ni Walimu saba wa Shule ya Sekondari Mantale, wakiongozwa na Ndugu Deogratius Paul - Mwalimu Mkuu. Popote walipo wasimame! Hawajafika? Haya! *(Makofi)*

Matangazo ya Kazi. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hii kwamba, leo tarehe 6 Novemba, 2012 saa 7.00 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa, B. Mnasisitizwa mfike kwa wakati.

Pia Mheshimiwa Andrew Chenge - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hii kwamba, leo, tarehe 6 Novemba, 2012 saa 7.00 mchana, watakutana Ukumbi wa Pius Msekwa.

Wale wengine ni Msekwa B. Hao ni Msekwa ule mkubwa. Mnasisitizwa mfike kwa wakati.

Mwisho wa Matangazo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba Mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68 (7). Kwenye Orodha ya Shughuli za leo, kuna Hoja za Serikali. Hizi Hoja za Serikali, zinalitaka Bunge lijadili na kuridhia Mikataba miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ile ibara ya 63 (3) ambayo inatoa mamlaka na madaraka kwa Bunge kujadili, kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninavyoomba mwongozo wako, hakuna hata Mbunge mmoja katika Bunge lako Tukufu ambaye ana Mkataba hata mmoja kati ya mikataba hii miwili ambayo tunataka kuijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu niingie kwenye Bunge la Tisa, imekuwa ni kawaida ya Serikali yetu kuwashtukiza Wabunge na kuendesha mtindo wa papo kwa papo juu ya Bunge kujadili na kuridhia Mikataba. Mikataba hii tunaiingiza nchini, kwenye Jumuiya za Kimataifa, ni mikataba ambayo inabidi Bunge kwa niaba ya wananchi waione hiyo Mikataba mapema, waipitie ili wajenge misingi ya kujadili ili waridhie vitu ambavyo vina maslahi na tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako kama inaruhusiwa Bunge hili lenye heshima katika nchi za Afrika na *SADC* kama kweli linaweza likajadili Mikataba hii muda mfupi ujao wakati Mikataba hii hatujaitia machoni. Nilikuwa naomba mwongozo wako kama inaruhusiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nimepokea ombi la mwongozo. Naomba niwasiliane na wenzangu mezani ili niweze kutoa mwongozo wangu kama hoja hii inaweza kufanyika kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, naomba niipokee, nitatoa maelekezo baada ya muda mfupi. Kwa hiyo, naomba tuendelee. Katibu, Agenda inayofuata!

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba Mpya wa Umoja wa Posta Afrika *(The Convention of the Pan African Postal Union (PAPU) of 2009)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya kuridhia Mkataba.

**WABUNGE FULANI:** *Aaaah!*

**WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya kuridhia Mkataba umoja wa Posta Afrika wa mwaka 2009. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani. Kutokana na hali ambayo Mheshimiwa Kangi ameielezea hapa kwa kuomba mwongozo wangu, nilisema nifanye mawasiliano kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tumruhusu Mheshimiwa Waziri asome mbele yetu lakini pia Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia wasome watupatie hali halisi ilivyo, wakati huo tutakuwa tumeshagawiwa vitabu hivi, mimi nitaliahirisha Bunge mwende kujisomea, baadaye mtakuja kuendelea na michango mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri naomba uendelee.

**WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya kuridhia mkataba wa Umoja wa Posta Afrika *(Instrument of Pan African Postal Union - PAPU)* wa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kwa maelekezo na michango mbalimbali wanayoitoa kutuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Ushirikiano wao wa karibu umetuwezesha maandalizi ya Azimio hili la kuridhia Mkataba huu wa *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu mapendekezo ya kuridhia ya Mkataba uliokusudiwa ambao naliomba Bunge lako Tukufu liweze kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Posta Afrika *(Pan African Postal Union – PAPU)* kwenye Makao yake Jijini Arusha ulianzishwa rasmi tarehe 18 Januari, 1980 kupitia uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama waliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika *(Organization of Africa Unit – OAU)* ambao kwa sasa unaitwa Umoja wa Afrika *(African Union – AU).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi haya ya *OAU* yalilenga kuifanya Sekta ya Posta kuwa chachu ya maendeleo hasa kwa kuzingatia kuwa huduma za posta zina mchango mkubwa katika kuunganisha watu wa kusaidia uendeshaji wa bidhaa, uchumi na masuala mbalimbali ya kijamii. Kujenga uwezo wa kitaalam kwa nchi wanachama pamoja na kusimamia maendeleo ya huduma za posta katika bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Posta imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali zitokanazo na maendeleo makubwa ya kiteknolojia katika Sekta ya Mawasiliano, utandawazi pamoja na soko huria ambayo athari yake imekuwa kubwa kwa Sekta ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mabadiliko hayo, mwezi Juni, 2009 Mkutano Mkuu wa *PAPU* uliofanyika Cairo – Misri, uliamua kuwafanyia marekebisho mikataba ya awali

ili kukubaliana na changamoto zilizopo, lengo likiwa ni kuiwezesha Sekta ya Posta kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa nchi wanachama wa Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama mwanachama na mwenyeji wa umoja huu ni vyema iridhie Mkataba huu mapema na kushawishi nchi nyingine ziharakishe kuridhia ili Mkataba uweze kutambulika kisheria na kuanza kufanya kazi. Kuridhia Mkataba huu mapema kutaongeza heshima ambayo Tanzania imepewa ya kuwa mwenyeji wa *PAPU* ambapo inapata manufaa mengi yanayotokana na kuwa mwenyeji wa umoja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui katika ibara za Mkataba wa Umoja wa Posta Africa zilizofanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo:-

Ibara ya kwanza mpaka ya tano zinahusu kuundwa kwa umoja, Wajumbe wa Umoja, madhumuni ya kuanzishwa kwa Umoja Makao Makuu ya Umoja na lugha zitakazotumika. Ibara ya sita mpaka 12 zinahusu muundo wa Umoja. Hii ni pamoja na vyombo vya Umoja ambavyo ni Mkutano Mkuu Baraza la Utawala Sekretarieti Kuu pamoja na Kamati za utawala na ufundi.

Ibara ya 13 mpaka 15 inahusu mapato na matumizi ya fedha za umoja. Ibara ya 16 mpaka 17 zinaelezea hati zinazowezesha Umoja kutekeleza Umoja wake ambazo ni Katiba, Mkataba, Kanuni na Taratibu. Ibara ya 18 mpaka 24 zinaeleza majukumu ya kisheria na uhusiano wa Kimataifa.

Ibara ya 25 mpaka 26 zinahusu haki, majukumu na kustawi kwa wananchama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kuridhia mkataba mpya wa Umoja wa Posta Afrika ni pamoja na mambo yafuatayo:-

Kwanza, mafunzo kwa wataalam wa masuala ya Posta yanayotolewa na Umoja ili kuongeza ubora wa utoaji huduma za Posta;

Pili, kushirikiana na nchi nyingine katika tafiti na ubadilishanaji wa taarifa mbalimbali za tafiti zinazohusu miradi au uanzishwaji wa huduma mbalimbali za Posta; na

Tatu, kufaidika na misaada ya kitaalam na kiufundi kutoka Umoja wa Posta ya Afrika, Umoja wa Posta duniani na mashirika mengine duniani yanayojihusisha na uendelezaji wa huduma za Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mikataba ya kimataifa ya aina hii inapasa kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya maelezo hayo, naomba kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Umoja wa Posta Afrika umeanzishwa kwa lengo la kujenga uwezo wa kitaalam kuongoza na kusimamia maendeleo ya huduma za maendeleo katika Bara la Afrika;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Mkutano wa Mkuu wa Umoja wa Posta uliofanyika mwezi Juni, 2009 Mjini Cairo Misri kulifanyika na kufanyika marekebisho katika Mkataba wa Awali ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika Sekta ya Posta ili kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii;

NA KWA KUWA Tanzania kama nchi mwanachama bado haijaridhia Mkataba mpya wa Umoja wa Posta ingawa imeendelea kutimiza masharti mengine ya wanachama ikiwemo kulipa ada ya Uanachama na kushiriki katika Mikutano ya Umoja huo;

NA KWA KUWA nchi zote za wanachama zilizosaini Mkataba mpya zinatakiwa kuridhia kulingana na utaratibu wa nchi zao na hadi hivi sasa idadi ya nchi zilizoridhia Mkataba huu ni tano ambapo Mkataba huu utaanza kufanya kazi endapo asilimia 51 ya uanachama wa Umoja watakuwa wameridhia Mkataba;

NA KWA KUWA Tanzania ni mwenyeji wa Umoja huu, uko umuhimu wa kuridhia Mkataba huu na kushawishi nchi nyingine kuridhia ili Mkataba uweze kutambulika kisheria na kuanza kufanya kazi, ikizingatiwa kuwa kutoridhia Mkataba kutahatarisha heshima ambayo Tanzania imepewa ya kuwa mwenyeji wa *PAPU,* kwani fursa hiyo inaweza kunyang'anywa na kupewa nchi nyingine zinazohitaji nafasi hiyo na hivyo kupoteza manufaa yanayotokana na kuwa mwenyeji wa Umoja wa Posta Afrika;

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba huu kutaiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kushirikiana na nchi nyingine za Bara la Afrika katika kubuni sera na mikakati madhubuti ya kuendeleza Sekta ya Posta kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi;

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba huu ni kutekeleza sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 inayoeleza kuhusu kuendeleza ushirikiano wa Kimataifa katika Sekta ya Posta;

NA KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina jukumu la kuridhia Mkataba kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, naomba kunukuu;

"Kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, Bunge laweza kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake yanahitaji kuridhiwa." Mwisho wa kunukuu.

NA KWA KUWA, madhumuni ya Azimio hili ni kuliomba Bunge lako Tukufu kukubali mapendekezo ya kuridhia Mkataba wa *PAPU* kwa mujibu wa ibara ya 29 ya mkataba huu ili nchi yetu iweze kunufaika katika kubadilishana wataalam, mafunzo, ufundi na tafiti mbalimbali zitakazoongeza tija pamoja na kuendeleza kupata manufaa yanayotokana na umoja huu kuwa na Makao Makuu yake hapa nchini;

NA KWA KUWA, Tanzania kama mwenyeji tayari imetoa jengo la ofisi za muda na hivi sasa imetoa eneo kwa ajili ya Makao Makuu na mchakato wa ujenzi wa ofisi za kudumu za Makao Makuu za Umoja unaendelea, fursa ambayo Taifa linaweza kuipoteza kwa kushindwa kuridhia Mkataba huu wa Umoja wa Posta Afrika;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo lenye mamlaka ya kuridhia Mkataba huu na baada ya kuridhiwa hati ya kuridhia itaandaliwa na kuwasilishwa kwa muhifadhi ambaye ni Katibu Mtendaji wa Umoja wa Posta Afrika kama ilivyoonyeshwa katika ibara ya 17(1)(2) ya Mkataba huu;

HIVYO BASI, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika *(Instruments of Pan African Postal Union)* ili Tanzania iweze kushirikiana na nchi nyingine za umoja huu katika kukuza maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa, sasa naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Nakushukuru sana. Namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na kuchambua Mkataba huu. Mheshimiwa Mwenyekiti au mwakilishi wake!

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii kuweza kusoma mbele ya Bunge lako Tukufu.

Lakini vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Busanda, kwa imani kubwa waliyonayo kwangu, lakini vilevile kwa ushirikiano mkubwa walionao kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi. Sasa basi, nisome maoni ya Kamati kama yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Posta Afrika wa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawaopongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kazi nzuri walioifanya ya kuchambua Azimio hili kwa kina na kunipa heshima ya kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu.

Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Anna Kilango - Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe ni Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Juma Sululu Juma, Mheshimiwa Rita Elinesfa Kabati, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogelesi, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila,

Mheshimiwa Raya Ibrahim Hamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar Mbunge, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Prof. Juma Athumani Kapuya, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Munde Tambwe, Mheshimiwa Sara Msafiri Ali, Mheshimiwa Eng. Athuman Mfutakamba na mimi mwenyewe Mheshiumiwa Lolecia Jeremiah Maselle Bukwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa iwapo Bunge lako Tukufu litaridhia Azimio hili, nchi yetu itapata manufaa yafuatayo:-

Kwanza, Tanzania ni Makao Makuu ya Umoja huu na imeshatoa eneo la kujenga ofisi za kudumu za Umoja Jijini Arusha kama ilivyoelezwa kwenye ibara ya nne ya Mkataba. Iwapo Bunge litaridhia Azimio hili, Tanzania itanufaika na kuwa mwenyeji wa Umoja huo.

Pili, kushirikiana na nchi nyingine kukabiliana na changamoto zinazokabili mashirika ya Posta kutokana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Tatu, kunufaika katika kubadilishana utaalamu, mafunzo, ufundi na tafiti mbalimbali zitakazoongeza tija kwenye Shirika letu la Posta.

Nne, kushamirisha sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 inayoeleza kuhusu kuendeleza ushirikiano wa Kimataifa katika Sekta ya Posta.

Tano, kwa kuwa nchi yetu inaendelea kulipa ada kwa ajili ya kuwa mwanachama wa Umoja huu, kuridhia Azimio hili kutahalalisha sababu ya malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo kutoka Serikalini kuhusu Azimio hili, Kamati ilijadili na kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(1) Kwa kuwa miongoni mwa malengo ya Umoja huu ni kukuza raslimali watu kwa kutoa mafunzo, Kamati inashauri kuwa kuwe na mpango mahsusi wa kuandaa Watanzania ili kunufaika na mafunzo haya.

(2) Kwa kuwa nchi yetu ndiyo Makao Makuu ya Umoja huu, uandaliwe mkakati mahususi kuona namna itakavyonufaika ikiwemo kupata ajira na masoko kwa bidhaa zitakazokuwa zinatumika na Umoja huu katika Ofisi zake Jijini Arusha.

(3) Ibara ya 15 ya Mkataba inaitaka nchi mwenyeji kutoa fedha kwa Umoja huo kadri itakavyowezekana ambazo zitarejeshwa na Umoja huo baadaye. Kamati inashauri kuwa, ni vyema ibara hii iangaliwe upya, kwani inawezekana kiasi kitakachokuwa kinahitajika wakati huu kikawa kikubwa zaidi kuzidi uwezo wa nchi yetu kifedha.

Aidha, haielezi Umoja huu utalazimika kurejesha fedha ndani ya muda gani ili nchi yetu isiingie hasara kwa fedha za walipa kodi wetu.

Ibara ya 25(i) inazitaka nchi wanachama kuheshimu Mkataba huu, maana yake ikiwa ni pamoja na ulazima wa nchi wenyeji kuupatia fedha Umoja huu ili irejeshwe baadaye.

(4) Iwekwe ibara itakayoeleza hatua zitakazochukuliwa iwapo Umoja huo utasaidia kuirejeshea nchi wenyeji fedha zilizotolewa na nchi husika kwa ajili ya matumizi ya Umoja huo.

(5) Ibara ya 26(3) inaeleza hasara itakazopata nchi itakayoshindwa kulipa ada zake kwa miaka miwili mfululizo ikiwemo kukosa haki ya kupiga na kupigiwa kura pamoja na kukosa misaada ya kiufundi kutoka kwenye Umoja huo.

Kamati inatoa ushauri kuwa Serikali itoe kipaumbele kwenye malipo ya ada za Umoja huu ili kutopoteza haki zake ikiwa ni pamoja na kuepuka aibu ikizingatiwa kuwa nchi yetu ndiyo Makao Makuu ya Umoja huo.

(6) Kwa kuwa Serikali imeeleza kuwa imetoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Umoja huo, na ibara ya 27 inaeleza uwezekano wa nchi kufukuzwa uanachama. Kamati inashauri Mkataba uweke wazi iwapo mwanachana aliyefukuzwa ni nchi mwenyeji kama ilivyo Tanzania kwa sasa, hatma ya ofisi zilizojengwa itakuwaje? Na iwapo ofisi za Umoja huo zitaendelea kuwepo kwenye nchi ambayo uanachama wake umesitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa - Naibu Waziri - Mheshimiwa January Yussuph Makamba, Katibu Mkuu wa Wizara hii - Dkt. Florence Turuka na Wataalamu wa Wizara hiyo kwa ushirikiano wao na kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri walioutoa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Azimio hili kwa manufaa ya nchi yetu.

Aidha, nampongeza Katibu wa Kamati - Ndugu Angumbwike Lameck Ng'hwavi kwa kazi nzuri ya kuandaa taarifa hii kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, Kamati kwa ujumla wake haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa azimio hili na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia ili kuendeleza ushirikiano wa nchi za Afrika katika masuala ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni haya ya Kamati, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kwa maoni ya Kamati. Namwita sasa Mheshimiwa Serukamba. Hamia kwenye *microphone* nyingine.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Kangi Lugola na wewe kutoa maamuzi yako, nilitaka kuliomba Bunge, kilichokuja mbele yetu ni Azimio na siyo Muswada wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sababu ya kuanzishwa Kamati za Kisekta ni kufanya kazi kwa ajili ya Bunge. Kamati yetu ya Bunge ya Miundombinu imepitia Maazimio yote mawili. Baada ya Serikali kuja mbele yetu tulisoma *page* kwa *page* tukaridhika na ndiyo maana tukakubali jambo hili lije Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliombe Bunge lako liendelee na baadaye tuweze kupitisha maazimio haya ili twende mbele. Naomba tuendelee kujadili na yule ambaye ana maoni ayalete kwenye kujadili na maoni hayo tutaona kama hajajiandaa, hatuwezi kuahirisha Bunge kwa sababu kuna mtu hajajiandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote, hoja ilipotolewa kwa kupitia mwongozo Na. 68(7) na Mheshimiwa Kangi Lugola na kuona sehemu kubwa ya Wabunge wamepiga makofi kwa maana ya kumuunga mkono kwamba hawajaona kitu, sasa naomba naendelea kuelezea kwamba baadaye meza ililetewa maelezo kwa maandishi na Wajumbe wa Kamati ambao walipitia mkataba huu, ambao Bunge linatakiwa kuuridhia; mimi niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tusipende kutoa kauli za jumla jumla wakati hatujui kinachoendelea.

Mheshimiwa Lugola alikuwa anashawishi Bunge hili likubali kwamba Wabunge wote kitu hiki ni kipya kwao, kumbe siyo kweli! *(Makofi)*

Wanasema, kama kitu hukijui, ni bora unyamaze kuliko kupotosha Bunge Tukufu kama hili ionekane sasa linakwenda kuridhia kitu ambacho halikijui kumbe Kamati yake kwa niaba ya Bunge zima imefanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kujadili Mkataba huu, baadaye wale ambao watakuwa hawajasoma waendelee kujiandaa wakati wenzao wanachangia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ile kauli kwamba nitasitisha shughuli hizi, ninaziahirisha, tutaendelea kujadili kwa sababu Kamati yetu imepitia kifungu kwa kifungu na kuukabidhi Ofisi ya Spika. Kwa hiyo, naomba tuendelee kujadili. Sasa namwita

Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu suala hili, asome maoni ya Kambi ya Upinzani.

Naomba tuendelee!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kusimama hapa leo. Lakini pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuisoma hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika, yaani *Pan African Postal Union - PAPU* ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kuanza kusoma hotuba hii, niungane na wananchi wangu wa Arumeru Mashariki na niwapongeze sana wale wananchi wa kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo *Usa River* ambao juzi siku ya Jumapili wamefanya mapinduzi makubwa kwa ushindi mkubwa wa kimbunga na hatimaye wakaamua kuikabidhi *CHADEMA* kuiongoza Mamlaka ya Mji Mdogo *Usa River* kwa kutupatia viti sita kati ya viti tisa vilivyokuwa vinaongozwa na Chama cha Mapinduzi na niwaambie tu kwamba wametupa Jimbo, wametupa mamlaka ya Mji mdogo sasa, bado Halmashauri mwaka 2015 na hatimaye nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Afrika mnamo mwaka 1980 Sekta ya Posta nchini imeendelea kudidimia na kudhoofu katika utoaji huduma kwa jamii na kuchochea maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na sababu zilizoelezwa na nchi

wanachama juu ya kudhoofika kwa huduma za Posta ikiwa ni changamoto zitokanazo na maendeleo ya kiteknolojia katika Sekta ya Mawasiliano, Utandawazi na Soko Huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu zilizoainishwa na nchi wanachama, ni dhahiri huwapa ugumu wa kupingana na maendeleo ya kiteknolojia kwa dunia ya sasa zaidi ikiwa na matokeo chanya kwa jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge ni hatua zipi zilizochukuliwa na Umoja huu baada ya Mkutano Mkuu uliofanyika mwezi Juni, 2009 Cairo, nchini Misri katika kufanya maboresho na kuhakiki Sekta ya Posta, kuona inaendelea kuimarika na kutoa huduma zenye kuongeza kasi ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Waziri mbele ya Kamati ilikiri kwamba Serikali imetoa jengo la ofisi za muda na kuendelea na mchakato wa ujenzi wa jengo la kisasa litakalotumika kama Makao Makuu ya Umoja na Mkataba. Inaonyesha jinsi Umoja utakavyowezeshwa katika majukumu yake ikiwa ni pamoja na kugharamia shughuli mbalimbali za Umoja. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata ufafanuzi katika mambo yafuatavyo:-

Moja, kwanza, ni kiasi gani nchi wanachama zimechangia katika jengo lililotolewa na Serikali na ujenzi unaendelea wa jengo jipya la kisasa?

Pili, ni makubaliano gani yaliyofanyika katika Mkataba na nchi wanachama katika kugharamia ujenzi wa Ofisi za Umoja ikizingatiwa ni moja ya maeneo ya msingi kabisa katika uendeshwaji wa majukumu ya Umoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta nchini limezorota katika utoaji huduma za Posta kwa kiasi cha kutokuwa na kasi nzuri ya kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii na kulitoa shirika hili hapo lilipofika, siyo tu kwa kujiunga na Umoja wa Posta Afrika bali ni zaidi kwa kuona changamoto tulizonazo na ni wapi soko lake limejielekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ina nia ya dhati ya kuboresha huduma za Posta, ni wakati muafaka wa kuliwezesha Shirika hilo liweze kutoa huduma kwa jamii yenye uhakika. Itakumbukwa na kufahamika kwamba huduma za Posta kwa sasa zimechukuliwa na Makampuni ya Usafirishaji wa abiria kutokana na huduma kutoa huduma kwa haraka zaidi kuliko Shirika la Posta. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchambua umuhimu wa Shirika la Posta na kufanya mabadiliko ya haraka ili liweze kutoa huduma zenye uhakika kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Posta wa Afrika, unahitaji asilimia 51 ya nchi wanachama zilizosaini uanzishwaji wa Umoja kuuridhia ili kuweza kutumika. Hadi kufikia sasa, ni nchi tano tu zilizokwisharidhia ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa Kongo, Kenya, Misri, Malawi na Tunisia. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua, ni sababu zipi zilizofanya Mkataba huu kuchelewa? Ni Mkakati upi uliopo katika nchi wanachama kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa kwa haraka? Ni hatua gani zitachukuliwa hususan kwa nchi yetu pale Umoja huu unapoendelea kusuasua na Shirika letu la Posta likiendelea kuzorota?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Joshua Nassari kwa uwasilishaji wa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mkataba huu.

Sasa tumeshapokea taarifa kutoka Serikalini, Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mkataba huu. Napenda sasa tuendelee kuchangia na nitawataja ambao wataanza kuchangia sasa hivi. Tutaanza na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde. Mheshimiwa Rajab Mbarouk na Mheshimiwa Leticia Nyerere wajiandae. Tutachangia kwa pamoja. Mheshimiwa Godfrey W. Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia, lakini naomba nisikitike sana namna ambavyo Kiti kimeliyumbisha Bunge leo hasa baada ya hoja ya Mheshimiwa Kangi Lugola, na Kiti kikakubali hoja ile na wewe mwenyewe Mwenyekiti ukasema Bunge litaahirishwa. Naamini Wabunge wengi wakachukua kauli yako na wengi wakatoka nje kwa sababu ulisema utaahirisha Bunge. Lakini inakuja Mwenyekiti wa Kamati anatoa maelezo tena, ukakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme na Watanzania waone kwamba mnaliyumbisha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nikubaliane na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati kwamba ilikuwa ni dhahiri kwa sababu hayo siyo mageni sana, yalishafanywa huko nyuma, kulikuwa hakuna sababu ya wewe Mwenyekiti kutamka kwamba litaahitishwa.

Kwa hiyo, naomba wakati mwingine pamoja na kwamba hatuhoji mamlaka ya Kiti, lakini Kiti kikiliyumbisha Bunge hatuwezi kwenda kwa utaratibu huo. Naomba wakati mwingine lisijitokeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kwa ufupi mambo yafuatavyo:-

Kwanza, naomba tena nisikitike kwamba maazimio haya yanachelewa sana kuletwa Bungeni. Azimio la mwaka 1999 la Umoja wa Mawasiliano, lakini Azimio la Posta la mwaka 2009 yanaletwa Bungeni leo. Kipindi kilichopita ni kirefu, wakati huo tunaelezwa tumeendelea kutimiza masharti yote ambayo yako kwenye Mikataba hiyo au Maazimio hayo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niiombe Serikali kwamba wakati mwingine iwe inatueleza sababu kwa nini inachukua muda mrefu namna hiyo kuleta maazimio haya Bungeni wakati vyombo vinavyohusika vilishakaa muda mrefu na kuazimia kwamba tuyaridhie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Umoja wa Posta walikaa mwaka 2009 wakafanya mabadiliko katika vifungu mbalimbali vya Mkataba. Pamoja na kwamba Makao Makuu yapo Tanzania Arusha, nchi tano tayari zimesharidhia, lakini bado Tanzania ambayo ndiyo Makao Makuu hayajaridhia na bado Waziri wanatuambia tufanye mapema kuridhia wakati tayari tulikuwa tumeshachelewa kuridhia. Mimi ningetegemea Tanzania ingekuwa ni nchi ya kwanza kuridhia ,*then* ingekuwa na maana zaidi. Unaposema kwamba turidhie mapema ili nchi nyingine ziweze kuridhia, naomba wakati mwingine hili pia lisijitokeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini natambua kwamba Kiswahili kilisharidhiwa kutumika au kuwa moja ya lugha za Umoja wa Afrika, lakini taarifa na Mkataba huu ambao ninao na ambao tumesambaziwa hivi punde umeandikwa kwa Kiingereza. Ni dhahiri kwamba kwamba inawezekana tukalalamikia Kiingereza, lakini kwa sababu Kiswahili kilisharidhiwa kuwa moja ya lugha ya Umoja wa Afrika, nilitegemea kwamba hata huu Umoja wa Mawasiliano na Umoja wa Posta Mikataba yake ingekuwa imetafsiriwa au imeandikwa kwa Kiswahili, ili basi iwe na tija zaidi kwa Watanzania wanapoijadili kuliko kuja kwa namna ambavyo imeandikwa sasa. Nategemea baadaye Wizara zote zitakazokuja na maazimio ya namna hii, basi Mikataba yake iwe imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulisemea, nataka nijue: Sasa hivi Shirika la Posta lina hali mbaya sana, lakini tunaelezwa kwamba tuko kwenye Umoja wa Posta katika nchi zetu za Afrika.

Sasa nataka Serikali inieleze Posta imefaidika nini kuwa kwenye umoja huu wa Afrika? Posta imefaidika nini kuwa kwenye Umoja huu wa Afrika na wakati huo tunaelezwa kwamba tumeendelea kulipa ada na kutimiza masharti mengine? Nilitegemea kwamba wakati Posta ni mwanachama katika umoja huu tungeendelea kuona faida ambazo ni za wazi kabisa ambazo shirika hili limeendelea kufaidika nazo.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze faida ambazo Tanzania imeendelea kuzipata.

Jambo lingine ambalo nilikuwa najiuliza, hatujaridhia mikataba hii lakini tunaendelea kulipa ada. Hivi tunaendelea kulipa ada kwa idhini ya chombo gani? Kwa sababu mkataba wenyewe haujaridhiwa na Bunge, lakini tunaendelea kutimiza masharti mengine pamoja na kulipa hizo ada. Sasa labda Serikali inieleze tunalipa ada hizo kwa kibali cha chombo gani maana najua Bunge ndiyo linapaswa liendelee kutoa kibali cha fedha zote ambazo zinalipwa kwenye taasisi mbalimbali za Umoja wa Afrika, pengine na jumuiya nyingine za kimataifa. Lakini hapa hatujaridhia maazimio haya. Serikali imeendelea kulipa michango, ninaomba kujua ada hizo zimeidhinishwa na chombo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mawasiliano ningependa pia tupate faida za moja kwa moja ambazo vyombo hivi au Umoja wa Mawasiliano tumeendelea kufaidika sisi kama nchi. Maana tusije tukawa tunaridhia tu. Pamoja na kwamba tumeandika kwenye taarifa ya Waziri, ukiisoma inasema tu kwamba kuna kufaidika kwa jumla, lakini hajatueleza tumefaidika katika eneo hili, eneo hili na eneo hili. Kama ni wataalam kutoka maeneo mengine, ambao wamekuja kwetu au wataalamu kutoka huko wamekwenda maeneo mengine katika Afrika, sijaliona moja kwa moja. Labda naomba Waziri atueleze, tumefaidika nini moja kwa moja pamoja na kuwa kwenye Umoja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maelezo mengi zaidi ya kwamba naunga mkono maazimio yote ambayo yameletwa hapa mbele, lakini niendelee tu kushauri kwamba wakati mwingine maazimio haya yasichukue muda mrefu zaidi ya miaka miwili, mitatu, wakati tunatakiwa tuwe tumeridhia mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 inachukua muda mrefu sana. Naiomba Serikali kwamba, Wabunge wawe wanapata taarifa ambazo ni za mapema zaidi. Basi ziwe zinakuja mapema zaidi na zitakuwa zinakuwa na maana zaidi kuliko ambavyo zinakuja kwa kuchelewa sasa.

Baada ya kusema hayo, naomba tu niseme naunga mkono maazimio hayo mawili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nakushukuru, lakini Mheshimiwa Zambi maelezo yako ya kwamba kiti Kimeyumbisha Bunge, siyo kweli. Waheshimiwa Wabunge mmeshangilia Mwongozo wa Mheshimiwa Lugola kwamba hamjaona chochote. Mimi kama Kiongozi hapa ni kuwatendea haki ninyi muwe mna utayari wa kuchangia hoja hii. Lakini kwamba mimi nimeyumbisha Bunge, hunitendei haki Mheshimiwa Zambi. Siyo kweli, isipokuwa ninyi muwe waangalifu. Mnashangilia kitu ambacho hamkijui! Tuwe na uhakika nini tunashangilia. Mnamshangilia Mheshimiwa Kangi Lugola, ambaye alikuwa anapotosha Bunge, mkamuunga mkono. Maana yake nini?

**MJUMBE FULANI:** Haina haja!

**MWENYEKITI:** Naomba unyamaze! *(Kicheko)*

Kwa hiyo, katika hili Kiti hakijayumbisha mtu yeyote. Naomba tuendelee na Mheshimiwa David Silinde.

*(Hapa Mbunge fulani alisimama bila idhini ya Mwenyekiti)*

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini. Mheshimiwa Silinde! Namwita sasa Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka niwe mmoja kati ya wachangiaji kuhusu suala zima la Posta. Nilitegemea kwamba *Protocols* hizi tutaweza kuzichangia kwa pamoja na wengi walijitayarisha hivyo, lakini bahati mbaya zimeletwa mbalimbali. Siyo vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba sasa hivi dunia imekuwa ni kijiji, suala la mawasiliano limeweza kutanuka. Lakini vilevile tukiangalia sera ya nchi yetu kuhusiana na suala la Posta inasema kuimarisha mahusiano ya kikanda. Kwa kweli kwa mujibu wa *Protocol* hii ambayo Waziri kaiwasilisha hapa kama watunga sheria, kama Wawakilishi wa wananchi, kwa kweli lipo hitaji kubwa la kukubali kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea mbele zaidi, nafikiri vilevile ni vyema ku-*declare interest* kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa katika nchi yetu au dunia kwa ujumla, utendaji wa Posta umeshuka kutokana na ukuaji wa mawasiliano. Sasa hivi suala la upelekaji wa barua baina ya mtu na mtu umepungua. Kilichobaki ni suala la upelekaji wa vifurushi. Ili tuweze kuendana katika suala zima la Kimataifa, kwa kweli kuridhia kwetu Mkataba huu ndiko ambako kutatupelekea biashara hii iweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nataka niwaombe Wizara na halafu Shirika lenyewe la Posta, kwa kweli hali ya Posta zetu ni mbaya, mbaya, mbaya kabisa na Sasa hivi tunataka kuridhia tena Mikataba hii ya Kimataifa. Inabidi kwanza turudi tujiangalie upya tusikimbilie tu moja kwa moja. Kwa hiyo, naiomba Wizara ifanye juhudi za makusudi kwanza kuimarisha hizi Posta zetu pamoja na Watendaji wake.

Sasa hivi tuna suala zima la anuani za Posta ambazo vilevile zitaturahisishia katika upatikanaji mzuri wa vitambulisho vya Taifa. Lakini zaidi ya hapo, sasa hivi tunakwenda katika masuala ya *GPS*. Kwa hiyo, hili suala la anuani za Posta inabidi Wizara iliangalie kwa mapana yake, ili twende nalo kwa haraka. Pale tutakapoamua au mtu atakapoamua mwenyewe kutumia *GPS* iwe imeshaunganishwa moja kwa moja na inakuwa rahisi kuweza kupata kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie suala la *EMS*. Hawa wenzetu wa Posta wamebweteka sana. Tunawaomba sana wenzetu wa Posta, tunataka kuingia sasa hivi katika Mikataba ya Kimataifa. Kuna haja ya kuweza kurekebisha *platform* yao katika suala zima la mambo ya *EMS*. Lakini vilevile sasa hivi wenzetu wa Posta mmeanzisha hizi *internet cafe.* Tunaomba hizi zisiwe kama zile za vijiweni, ziendane na haya ambayo tunayaridhia ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pale Chakechake katika Kituo cha Posta kwa kweli unaona aibu jinsi kikompyuta kimoja kimewekwa pale, vimeza vyenyewe vibovu, wamefunga na pazia. Sasa sisi wenyewe kwanza hebu tujirekebisheni jamani, halafu ndiyo tena tukiingia huku tuwe tumejitayarisha. Tunaomba sana wenzetu wa Posta katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie moja kwa moja katika Mkataba wenyewe. Nakwenda katika *article number five* ambayo inasema: "*The official language of the Union are Arabic, English, French, Portuguese and Swahili, while the working language shall be English and French*." Najua kwamba Wizara wala Posta wenyewe hawana uwezo tena wa kuibadilisha hii, ni kuridhia tu. Lakini ninyi mnakwenda katika hii mikutano, tunaomba mwende pamoja na mapendekezo ambayo tutayatoa kama Wabunge au kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mkapendekeze ya kwamba, hii *working language* iwe ni zile lugha zote ambazo zimekubaliwa na *AU*, siyo watuchagulie lugha namna hii kwamba ni *English and French*. Mbali na kwamba *official languages* imekubalika, Swahili imo, lakini tunataka hii *working language* nayo iweze kuendana na lugha ambazo zinatumika na *AU* ambapo Kiswahili kimo ndani yake. Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nataka niende katika *article number fifteen* ambayo inasema *Advance of Funds to the Union. The government of the host-country shall to the fullest extent possible advance funds to the Union for its smooth operations, pending their re-imbursement.*

Je, Serikali mmejitayarishaje katika hili? Tunaingia katika Mkataba wa Kimataifa, Makao Makuu yako Arusha, mtakuwa tayari kutoa *advance* kwa ajili ya kuendesha shughuli za Ofisi hii? Tusije tukakubali kitu halafu tukatakiwa tuendeshe chombo, tukaanza kusema ooh, kasungura kadogo. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, mmejitayarishaje katika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kidogo katika *registration of the conference, article number one*. Hii inasema kwamba atakayeongoza, *the government of each member state shall represent at the conference by a delegation led by the Minister responsible*. Waziri ndiye atakayeongoza ile *delegation* ambayo itakwenda katika vikao.

Katika vikao vyote vya Kimataifa kunakuwa na maamuzi ya kinchi. Maamuzi ya kinchi *(authority)* yanakuwa yanatolewa na Rais ya kwamba utasaini hili, utakubali hili, utaiingiza nchi hapa, au vile vile inatolewa na Waziri wa Mambo ya Nje.

Katika Mkataba huu, hii *power* haikuoneshwa nani atakuwa na *power* kamili ya kuweza kuridhia yale masuala makubwa ya Kitaifa au Mikataba ile ya Kimataifa au kuridhia jambo ambalo nchi yetu itabidi ilikubali katika ule Mkutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa kilichoelezwa hapa ni kwamba ni Waziri tu anayehusika na suala hili ndiye ambaye ataongoza ile *delegation*. Nafikiri haya, kama Wizara myachukue na mtakapokwenda huko myapendekeze ili vipengele kama hivyo viweze kuingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Rajab, nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Leticia Nyerere na Mheshimiwa Ezekia Wenje ajiandae.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mawazo yangu kuhusu hili azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kusema kwamba kuna haja ya kupitisha huu Mkataba. Kama ulivyoona na kushuhudia mwenyewe, tungekuwa tumeridhia huu Mkataba miaka mingi, leo hii Wabunge tusingeanza kusema kwamba hatuna taarifa kuhusu Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema hivyo? Hili azimio limekuwa kwenye mtandao wa Bunge wiki nzima sasa. Lakini hatujautumia mtandao na ndiyo maana leo tunadhani ndiyo kwanza azimio hili linawekwa hapa Mezani, wakati limekuwa likizagaa pale kwa takribani wiki nzima. Kuna haja kweli ya kuridhia hili azimio? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo faida niliyoisema, kuna faida nyingi za kuridhia hili azimio. Faida nyingine ni hiyo ya mawasiliano kama nilivyosema, lakini siyo mawasiliano tu ya ndani, vilevile mawasiliano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba, sasa hivi duniani kote kuna tatizo la ugaidi. Endapo sisi tutaamua kujitenga na kukataa kuwasiliana na wenzetu, nchi nyingine ambazo ni takribani 45 ambazo ziko kwenye Mkataba huu, kwa kweli sioni Taifa letu litakuwa linaelekea wapi kiusalama hasa ukizingatia kwamba vitendo vya ugaidi vimepamba moto. Kwa hiyo, mimi naona pia hii ni sababu moja kubwa kabisa ambayo tutake tusitake inabidi turidhie Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio hili pia au sheria itakayotungwa kutokana na hili azimio itatusaidia kupata anuani za makazi, na kama unavyofahamu, anuani za makazi ni muhimu sana kwa dunia ya leo. Faida moja kubwa ya kwanza ambayo wote tutaishuhudia, wale ambao wamewahi kuishi nje ya nchi hii, unapopatwa na dharura na una anuani ya makazi, unapiga simu ya dharura, huhitaji kutoa maelezo yanayoonesha uko *address* gani.

Unapopiga simu tayari wahusika wenyewe watatambua uko kwenye anuani gani na baada ya kupiga hiyo simu ya dharura wataingia baada ya dakika chache tu kuja kunusuru maisha yako.

Kwa hiyo, Watanzania tunahitaji kuuridhia huu Mkataba ili angalau tuwe na uhakika na hali ya usalama wetu na uhakika wa kuweza kuwa na kimbilio endapo unakutwa na dharura au hatari ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida nyingine ya kuridhia Mkataba huu ambayo ni faida ya kibiashara. Tunapofanya biashara kwa kutumia *new technology,* yaani mtandao, hakika wafanyabiashara wengi watanufaika. Hata wale ambao wananunua hizo biashara watanufaika ukizingatia kwamba hatutahitaji kwenda Kariakoo kwenye msongamano kuweza kufanya manunuzi, badala yake unaweza ukachukua *catalogue* ukachagua kitu chako ukaagiza ukiwa nyumbani kwako na wale watu ambao wanakuuzia biashara hiyo watakuwa na uwezo wa kukuletea hizo bidhaa nyumbani kwako bila bughudha yoyote. *(Makofi)*

Vilevile katika kusonga mbele kibiashara, unapokuwa una mawasiliano ya Kimataifa ni rahisi kupata mbinu za kibiashara za Kimataifa badala ya wewe kukaa kwenye *kiosk* chako watu ambao unawauzia bidhaa yako ni walewale wa siku zilezile, hupati *ideas* nyingine mpya zozote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapokuwa katika hali ya mashirikiano ya Kimataifa, ni lazima tutapata mwamko zaidi, ni lazima tutapata upeo mkubwa zaidi. Ndiyo maana hata katika suala la ajira, tunashindwa kuwapatia ajira vijana wetu walio wengi hasa katika mbuga za wanyama, ukizingatia kwamba hawana ule uelewa wa Kimataifa. Serikali haichukui jitihada za ziada kuwawezesha vijana wetu kupata ule uelewa. Wazungu wanasema, "*international exposure.*" Ni muhimu katika shughuli yoyote ile!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Azimio hili limekuja kwetu pamoja na kwamba limechelewa kidogo. Lakini endapo tutalitumia vizuri, hakika nchi yetu itasonga mbele kwa mambo mengi tu, ukizingatia kwamba kila kitu sasa hivi kinafanyika chini ya teknolojia ya kisasa. Ukiamua wewe kuwa Kijiji, umejitenga kutoka kwenye Kijiji ambacho ndiyo dunia ya leo ambayo iko kwenye utandawazi, kweli utaendelea kufanya mambo ya zamani na utaachwa na wenzio mbali tu na utakuwa umepitwa na wakati kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nisingependa kuchukua muda mrefu sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge turidhie huu Mkataba, kwani ni muhimu sana. Kama mlivyoshuhudia wenyewe, tunauhitaji huu Mkataba ili tuweze hata kufuatilia maelezo au taarifa tunazopewa kwenye mtandao wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Leticia Nyerere. Sasa namwita Mheshimiwa Ezekia Wenje, na Mheshimiwa Eng. Athuman Mfutakamba pamoja na Mheshimiwa Felix wajiandae. Mheshimiwa Wenje endelea kwanza.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa hii ili niweze kuchangia kwenye huu Mkataba wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kusoma hii *African Telecommunication Union,* hii *Constitution and Convention of the African Telecommunication Union (ATU)* ya mwaka 1999. Huu Mkataba ulitengenezwa mwaka 1999, leo ndio tunaletewa mwaka 2012, ni zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ambacho napenda kujua kwa mtindo huu wa kufanya kazi ya Mkataba unasainiwa miaka 10 imepita halafu ndio tunaletewa kuja kuridhia kwa sababu ndani ya miaka 10 kuna mambo mengi yanatokea. Ukiangalia hata yale mazingira ya soko la *Telecommunications* baada ya miaka 10 au ndani ya miaka 10 limebadilika sana. Sasa kama Mkataba uliwekwa kwa mazingira ya miaka 10 iliyopita halafu inaletwa kuridhiwa baada ya miaka 10 tena ijayo hii inafanya tunakuwa *reluctant players* kwenye mambo muhimu kama haya. Sasa *next time* kama Serikali iko *serious* inapokuwepo na Mikataba kama hii, bora tukaifanyia kazi mapema wakati wa mazingira ya Mkataba huo ulipotengenezwa yaani turidhie kipindi ambacho mazingira yanaendana na kile kitu tunacholetewa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, nimeangalia Ibara ya 8(2) ya Mkataba huu inayosema kwamba lugha rasmi zitakazotumika kwenye huu Umoja ni Kiingereza pamoja na Kifaransa na kwenye hiyo Ibara wanasema kwamba kama kuna nchi yoyote itakayotaka labda lugha yake itumike basi iwe tayari kugharimikia fedha za watu watakaokuwa wanatafsiri na kila kitu. Sasa kwa kuwa juzi tu hapa tumepitisha huu Mkataba wa Kiswahili na naendelea kusisitiza kwamba kama tunao uwezo kwa sababu hiyo Ibara ya 8(2) inatoa fursa ya nchi wanachama kutoa mapendekezo yao, mimi napenda kuhimiza nchi yetu hata kama tutalazimika kugharimikia, lakini tuweze kupeleka Kiswahili iwe moja ya lugha kati ya hizo lugha mbili, Kiswahili iwe lugha ya tatu itakayotumika hapo, hata kama tutalazimika kugharamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nimeona kwenye huu Mkataba ni kwamba Tanzania wadau kwenye sekta ya *Telecommunications* ambao wanahusika sana na huu Mkataba nimeona wameainishwa Shirika la *TTCL* pamoja na *ZANTEL*. Sasa Tanzania kama unajua kuna wadau wengi wako *VODACOM, AIRTEL*, sasa napenda kujua hawa *actors* wengine katika sekta ya *Telecom* kama *VODACOM, AIRTEL* wao watahusishwa vipi katika...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Wenje kuna taarifa unapewa. Naam Mheshimiwa Rajab!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayezungumza sasa hivi anazungumzia Mkataba ambao haujawasilishwa. Sisi tumezungumza Posta, lakini naona tunaanza kuzungumzia mambo ya *Telecommunication*. Naomba kutoa taarifa hiyo tu.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi ni kwamba tukimaliza kujadili Azimio hili la Mkataba Mpya wa Umoja wa Posta, Mheshimiwa Waziri atakuja kusoma Azimio hili linalohusiana na mambo ya *Teleclommunications* kwa pamoja tutakuja kuridhia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Wenje hiyo ndiyo taarifa naomba uendelee.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Order Paper* ya asubuhi iliandika kwamba tunakuja kujadili Azimio la *Telecom* pamoja na hili la Posta. Sasa mimi nilikuwa najiandaa kuja kuchangia *Telecom* kwa mujibu wa *Order Paper* iliyowasilishwa humu ndani asubuhi. Sasa kama mmekubaliana tofauti basi naomba nije nichangie kwenye hiyo *Telecom.*

**MWENYEKITI:** Sawa nakushukuru. Mheshimiwa Felix Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia machache kwenye Mkataba wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu wa Posta ni muhimu kwa nchi yetu kwa sababu hatuwezi tukajitenga, lakini ningependa kupata ufafanuzi kwenye baadhi ya mambo. Kwanza, ni kuhusu Serikali kwa sababu nchi yetu tunafuata *dualism system* ya kupitisha Mikataba ya Kimataifa ambapo Serikali mnaanza kwenye majadiliano huko mnasaini na ndiyo mnatuletea sisi tufanye *ratification.*

Sasa nataka nijue kwa nini mlikubali kusaini Mkataba huu wakati wameandika kwamba *working language* itakuwa ni *English*, je, mlihoji kuhusu lugha yetu ya Kiswahili wakati mnafanya majadiliano kabla ya kuleta Bungeni ili tuuridhie? Nataka mnipe majibu, mlihoji au mlikubali tu mkasaini sasa mmetuletea na sisi turidhie? Kwa sababu lazima kila Wizara iangalie *opportunities* ambazo tutakuwa tunapata kwenye Mikataba hii na moja ya *opportunities* ndiyo kama hizi tumepitisha juzi hapa Mkataba wa Kiswahili na kama Mkataba huu ungekuwa unasema kama *official language* itakuwa ni Kiswahili ina maana kwamba tungepata *opportunities* za ajira na vitu vingine. Sasa nataka nijue *during negotiations* na mpaka mkafikia kusaini mlikubaliana na kifungu hicho? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili nataka kujua ada hizi ni kiasi gani ambazo tumekuwa tunalipa kwa mwaka na tumefaidika nini kwa kila mwaka. Sisi tumekuwa tunafaidika nini katika Umoja huu wa Posta, tumepata nini *apart from capacity building* na mikutano, vitu gani *tangible* ambavyo sisi tumekuwa tunapata kama Taifa? Ningependa Waziri anipe majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimeona kwenye Mkataba huu kuna *Regulations* ambazo zitakwenda kuandaliwa na hizo ndizo zitakazo-*determine* ada ambayo itakuwa *fixed.* Sasa je hii *provision* ninyi mnaiangalia kwa namna gani, sisi tunakwenda kuwa *fixed* na wao Bunge kwa sababu sisi ndio tunaamua kwamba tuchangie kiasi gani kule? Sasa nataka maelezo kutoka kwenye *provision* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la tatu nataka nijue mmejipangaje kuhusu hali ya Posta ya Tanzania kwa sababu hali ya Posta ni mbaya. Mfano wa Posta pale Jimboni kwangu, kwanza jengo lao ni dogo sana wamepanga, wana kiwanja miaka mingi sasa, mna mpango gani tunaporidhia Mikataba hii, naomba kupata majibu ikiwa ni pamoja na kujenga ofisi zinazoeleweka za Posta. Katika maeneo mbalimbali ya nchi hii tumekuwa na Posta muda mrefu lakini unafika kwenye kajengo kao kadogo hakaelewekieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi sitakuwa na mengi ila naomba nipewe majibu sahihi kwenye hayo maeneo ambayo nimeuliza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakushukuru Mheshimiwa. Namwita Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Pindi Chana ajiandae, pia Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na Cecilia Paresso wajiandae.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika Mkataba huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi ya awali kumpongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa January Yusuf Makamba kwa kuleta Mkataba huu mzuri ambao ndani yake una maslahi makubwa na nchi yetu. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kuzungumza kwamba ni kweli Watanzania lugha ya Kiswahili sisi wenyewe hatutaki kuitumia. Kwa sababu pamoja na Bunge kuridhia lugha ya Kiswahili na Mataifa kuridhia, lakini bado lugha hii hatuitumii sisi wenyewe vilivyo, taarifa zinaletwa Kiingereza, Watanzania wetu walio wengi hawajui Kiingereza, sasa sijui kama tuna lengo hasa la kutaka Watanzania wajue mambo tunayoyapitisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Posta wa Mwaka 2009. Mimi Azimio hili naunga mkono mia kwa mia. Wenzangu wanasema kwamba limechelewa sana lakini nadhani kila jambo na wakati wake, wakati umefika leo Azimio liko mbele yetu. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono Azimio hili kwa pamoja, nina sababu ya kusema hivyo. Azimio hili endapo tutaridhia, ninaamini kuna mambo mengi ambayo nchi yetu itanufaika, Watanzania wetu watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukua jambo moja tu la kwamba Makao Makuu yake yatajengwa Tanzania kwa maana ya Arusha. Hili peke yake lina faida kubwa kwa Watanzania, vijana wetu watapata ajira, akina mama watafanya biashara, kina Mama Lishe watauza na biashara nyingi zitafanyika na mzunguko wa fedha utakuwa mkubwa. Ndugu Wabunge wenzangu, ninawaomba sana tuliridhie Azimio hili lenye nia thabiti ya kuleta Umoja mzuri wa Posta katika Afrika yetu na mawasiliano yetu kati ya nchi na nchi katika Afrika nzima yatakuwa mepesi, tutaweza kufanya biashara zetu, tutaweza kupata muda mzuri wa kujadiliana mambo mbalimbali, wakati Watanzania tukiwa na maslahi makubwa kwa kuwa wageni wataingia katika nchi yetu wakati wa vikao kama hivi. Kwa hiyo, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, hatuna sababu ya kusitasita katika hili, kazi iliyopo mbele yetu ni kuunga mkono Azimio hili ili liweze kufanya kazi zake kama lilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nitoe angalizo kwa Serikali. Ndugu zangu ni vizuri sana Azimio hili ambalo tunaliridhia leo faida zake zikaainishwa wazi tukazijua, Watanzania wakazijua na hata kama kuna mambo ambayo mnaona kwamba yanaweza yakatuletea taabu kidogo ni vizuri tukawa makini nayo. Waswahili wanasema “Ukiumwa na nyoka ukiona hata jani utadhani nyoka”. Wako Watanzania mpaka leo waliofanya kazi kwenye Reli ya Afrika Mashariki bado wanadai haki zao na taasisi mbalimbali zilizokuwa za Afrika Mashariki mpaka leo wako watu wamepoteza haki zao.

Kwa hiyo, ninaomba sana tuwe makini katika hili, tuangalie maslahi makubwa ya Tanzania tutakayopata kutokana na hili na pia tuweke tahadhari maeneo ambayo tunaona kabisa yanaweza yakaiumiza Serikali yetu. Hii itasaidia sana Umoja huu ambao tunauridhia leo kuhakikisha nchi yetu inapata maslahi makubwa na Watanzania watanufaika na Umoja huu ambao tunataka kuuridhia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mengi ya kuzungumza, nilipenda tu kuikazia Serikali kuainisha faida na udhaifu utakaonekana humu na kuwekea tahadhari mapema kabla ya mambo yote hayajaanza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono Azimio hili mia kwa mia na kwa kuwa sitapata nafasi ya kuongea tena nilitegemea Maazimio haya yangewasilishwa yote mawili halafu tuyachangie kwa pamoja. Sasa kwa kuwa limeshawasilishwa moja, mimi naunga mkono na Azimio la Mawasiliano mia kwa mia litakaposomwa mjue Mheshimiwa Diana Chilolo anaunga mkono na kwa kuwa Waziri na Naibu Waziri wenye dhamana ni hawahawa, nawashukuru sana na Mungu awabariki sana. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Maazimio haya yanayohusu Masuala ya Mawasiliano Afrika na niseme kwa sababu yako mawili na nimesoma yote, kwa hiyo nitakapokuwa nachangia, nitachangia aidha Azimio moja ama lingine yatatumika yote *interchangeable*. Kwa hiyo, naomba Mawaziri mchukue pointi nitakazokuwa nawashauri, lakini naanza kwa kusema kwanza naunga mkono hoja, ni Azimio muhimu sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Changia moja kwa sababu lingine Waziri hajawasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Haya nitachangia moja kwa sababu michango inafanana, masuala ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja na kwamba masuala ya mawasiliano hususan Posta, ni jambo la msingi sana. Baada ya kuridhia Mikataba hii ya Kimataifa ambayo inaitwa *International Conventions,* kwa kawaida huwa tunapaswa ku-*domesticate* ndipo unapoweza kutumia au kudai *remedy before the court of law*. Lakini tukiridhia hapa bila ya kufanya *domestication* yaani kubadili sheria zetu *locally* za masuala ya Posta, *The Telecommunication Act,* kazi tutakayokuwa tumeifanya hapa ni bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, hii Mikataba tunayoiridhia ni muhimu tukaiwekea *limitation of time. Once* Bunge likiridhia basi zile sheria ambazo zinatakiwa ziwe *amended* ili ku-*accommodates* yale ambayo tumeyaridhia yawe yanapewa *limitation of time, may be within six months or within the next Parliamentary Session.* Vinginevyo tutakuwa tunaridhia halafu hatujarekebisha sheria zetu za ndani huwezi kwenda katika chombo chochote cha kutenda haki Mahakamani ukasema labda kuna eneo fulani nadai haki kwa sababu hii ni Mikataba, ni *International Convention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba wakati anajibu Waziri tujue ni lini Mkataba huu tunaoridhia utakuwa *domesticated* yaani utakuwa *compatible* na zile sheria zetu. Hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu sasa hivi tunasema kuna kitu kinaitwa *E-Government,* mawasiliano yanakuwepo nchini, lakini bado maeneo mengi katika Halmashauri zetu mawasiliano ni changamoto. Kwa hiyo, tujaribu sana kuboresha masuala ya mawasiliano. Huduma za Posta zenyewe ziko Makao Makuu ya Wilaya na leo tunazungumzia kuwa na *communication the whole of Africa* wakati sisi Tanzania bado hatujaboresha. Ukiacha Makao Makuu ya Wilaya tunazo Wilaya mpya kadhaa. Kwa hiyo, lazima tuharakishe Wilaya mpya zote ziwe na huduma ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia huduma hizi za Posta sasa zianze kushuka kwenye Kata. Ziko Kata ambazo ni vijiji mji. Tuna Kata kama ya Manda, Lupingu, Mfumbi, maeneo ya Makete kule Ludewa, Njombe.

Kwa hiyo, maeneo haya sasa tuanze kushuka ili hizi huduma ziwe sahihi. *Otherwise* watakaokuwa wana-*enjoy* hizi huduma ni wachache sana katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza kwenye Majiji, lakini watu wa huku *local government* watakuwa bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu tukubaliane ni suala la gharama. Mawasiliano katika nchi yetu yamekuwa ni *too expensive*. Ukienda nchi nyingine, nchi kama India unakuta kutuma *message* kwa simu za palepale, *local* za India ni rupia moja lakini Tanzania *message* ni gharama, mawasiliano ni gharama, vocha zenyewe ni gharama, lakini kumbe mawasiliano yakiwa na bei ya chini watu wana-*communicate,* wanafanya biashara, wanalipa *TRA* uchumi unakua *faster*. Kwa hiyo, hili suala la gharama za mawasiliano, naomba tuangalie sana. Mashirika yetu ya mawasiliano yamekuwa yanachaji tozo kubwa kiasi kwamba wananchi inakuwa ngumu sana ku-*afford*. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo hakika lazima tuharakishe kufanya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni namna gani tunatumia haya mawasiliano. Mawasiliano wenzetu wanasema *communication is power*. Katika nchi nyingine mtu anapata matatizo labda ya matibabu, anai-*Google* tu *Diabetic* unaitibu namna gani. Mtu anapata matatizo fulani ana-*Google,* anakwenda kwenye masuala ya posta, anapata makabrasha, kuna vitu vinaitwa *Yellow Page*, kuna masuala ya biashara, wengine ni masuala ya elimu kwenye vyuo vikuu lakini sisi Watanzania hii *communication* tunaitumia sawasawa na azma hiyo?

Maana kwenye *vision* wamesema; *to make Africa an active participant in global information society.* Sasa kweli sisi hizi *communication* huko kwenye *ma-website, message* kwenye simu tunazotumiana, *are they real healthy?* Ni mawasiliano ambayo yana afya au hayana afya? Haya ni maeneo ya kujiuliza na tuendelee kupeana elimu. Kwa hiyo, nadhani masuala ya mawasiliano ni muhimu sana na kwanza mawasiliano yanapunguza gharama. Kama ilikuwa mtu asafiri kutoka *point A,* Ludewa sijui Makate uende mpaka Nairobi - Kenya, Uganda kwa mawasiliano tu yanapunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mkataba huu ni muhimu, tunatakiwa tuuridhie tena mapema na kwa kweli tutumie vizuri sana elimu. Lakini naomba sana tu-*domesticate* haraka vipengele vinavyohusika, tuvirekebishe ili uwe *compatible* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika mkataba limeeleza kwamba *official language of the Union* itakuwa ni *English and French*. Katika Mikataba ya Kimataifa kuna kitu kinaitwa '*reservation*.' Unaukubali Mkataba lakini kifungu fulani hukubaliani nacho unasema una-*reserve*. Kwa hiyo, katika *language* sisi hazina yetu ni Kiswahili. Kuna nchi zaidi ya kumi zinatumia Kiswahili mfano Zambia, Malawi lakini Kiswahili hiki jikoni kwake ni Tanzania. Sasa tusipotumia hii *opportunity* ya *OAU* kwamba sisi Tanzania ni chimbuko la lugha ya Kiswahili, *we are the treasury of this important language*, tutakuwa tunaacha wanasema Kifaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tunafanya *reservation* kwamba tunaunga mkono Mkataba huu lakini kwenye lugha tunaomba lugha ya Kiswahili iwepo. Ndiyo uzuri wa kutumia mamlaka yetu na ndiyo maana sisi hatupo kama Kenya, Kenya wakiridhia Mkataba kama huu *automatically* unakuwa *part of their law.* Sisi tukiridhia hauwezi kuwa *part of our law unless* tunau-*domesticate*. Ndiyo maana tunatunza kitu kinaitwa *sovereignty of our country*. Tuna *sovereignty,* tuna *tradition and culture*. Sasa Mkataba huu ili utumike Tanzania lugha ya Kiswahili iongozwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna eneo la *Organ of the Union*. Kutakuwa na Sekretarieti na kila kitu kama tulivyoshauriwa kwamba katika hizi *organs* lazima zizingatie *gender*. Kwa hiyo, tunashauri pia *organs* zote ambazo zitakuwepo ku-*manage* huo mkataba *women and men together should be considered. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ndiyo maeneo ambayo ningeomba sana yazingatiwe na kwa mara nyingine tena naunga mkono mkataba huu uridhiwe lakini ufanye kazi mpaka kule kwenye kata na vijiji, masuala ya mawasiliano yawepo kwa haraka sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kupata nafasi hii ya kusimama hapa na mimi kutoa mchango wangu kuhusu Azimio hili la PAPU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni vizuri Bunge lako kuelewa kwamba na ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati. Tumeletewa hii *Constitution and Convention of ATU and instrument of PAPU* iko kwa pamoja. Kwa hiyo, katika ule utaratibu wa kawaida hata vipengele vyote vipo kwa pamoja, ilikuwa ujadiliwe kwa pamoja lakini tumeshafanya kosa wakati mwingine hilo tulielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja kubwa humu pamoja na kwamba hiki kitu kimetokea *Cape Town* mwaka 1999 miaka 13 iliyopita, hii ya *PAPU* baada ya miaka kumi, ilipofika Juni, 2009 mkataba ukafanyiwa marekebisho kule Misri baada ya miaka kumi, sisi bado hatujaridhia. Serikali imeweza kukaa muda wote, *document* hii imeletwa kwa muda mfupi tuelewe mambo yote na turidhie. Huko kusema kweli kwa upande mmoja hatulitendei haki Bunge au hatuwatendei haki wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi katika mchango wangu kwanza niseme kitu kimoja na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha ni *Engineer* sasa tukitizama kuna mahesabu madogo tu hapa; tukiyatizama tunaweza kupata hoja ya msingi. Kwamba nchi zilizoridhia mpaka sasa hivi ni tano. Tukitizama kwa *population* ya nchi za kiafrika, ina maana tuna asilimia tisa ya walioridhia, kwa kauli yake Mheshimiwa Waziri, nchi tano mpaka sasa hivi ndiyo zimeridhia na leo Tanzania tunataka turidhie asilimia tisa. Tukichukua ile ya kuanzia Juni tu baada ya marekebisho kufanywa Misri ina maana miaka mitatu nchi tano zimeridhia.

Sasa ili kufanikisha kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri basi inatakiwa iridhiwe kwa asilimia 51. Ina maana nchi tano ni asilimia tisa bado tunahitaji nchi 27 kufikia asilimia 51. Ikiwa tano zimesharidhia bado nchi 25 ziridhie na ikiwa tano toka mwaka 2009 miaka mitatu, ina maana ikiwa inaenda kwa *speed* hiyohiyo tunahitaji miaka kumi na tano mingine. Sasa nini kilichopelekea Tanzania sasa hivi kuwa na haraka ya kuridhia au ni kwa sababu ya hizo fedha tutakazopata kujenga Makao Makuu Arusha? Hapa pana siri fulani. Serikali itueleze na kutufafanulia, haraka hii ya nini na tumekaa muda wote huo; ni kwa sababu ya kupata fedha hizo kujenga Makao Makuu Arusha au jambo gani? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kwamba hii Mikataba haina tofauti na mambo ya Sheria. Bunge likitaka kupitisha Sheria fulani hapa Kamati zinazohusika zinapewa fursa ya kuwaita wadau na kupata maoni ya wadau. Sasa iweje leo Bunge hilihili katika kuridhia mikataba ambayo mambo ni yaleyale ya kisheria tena mengine ya mitego, yana hatari kubwa sana kwa nchi kwa baadaye, Kamati hazipewi nafasi ya kutafuta wadau wakaja wakatoa maoni yao, nao tukawasikiliza. Katika suala la *PAP* mdau hapa si Posta peke yake, kuna watu wa *DHL* ni wadau wapo nchi hii, kuna watu wa *EMS* wapo nchi hii, kuna watu wa *UPS* wote wanahusika na mambo ya vifurushi na wapo nchi hii. Kamati haikupata nafasi ya kusikiliza maoni yao kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametupa faida nyingi sana zinazoweza kupatikana kwa kuridhia mkataba huu lakini upande mwingine wa shilingi hatuupati. Hasara mbona hajatueleza na kama hakuna hasara kwa nini Serikali ilikaa miaka 13 kutokuridhia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wamekaa nao kwa muda mrefu, wamechambua wameona *pro-and-cons*. Kwa hiyo, ina maana wakati Mheshimiwa Waziri anatueleza faida, basi ilikuwa na hasara atueleze ndiyo Bunge litapata ile picha kamili, jambo hili kwa nini limekaa muda mrefu, kwa nini tunahitaji umuhimu wa kuridhia leo? Haya mambo tusifichwe na Bunge lisiwe na *double standard.* Kama ilivyo kwa Miswada mingine ya Sheria hapa nchini huwaita wadau na kusikia maoni yao, lakini mikataba hii yote tunayoridhia hatuna fursa ya kuwaita wadau wengine ili na sisi tukapata maoni yao. Bunge litakuwa halitendewi haki na ikiwa hatulitendei haki Bunge ina maana hatuwatendei haki wananchi. Tupate fursa na wadau tuwasikilize maoni yao, maana tujiulize kwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko sehemu ya pili, bahati mbaya nitaiacha, kuna kitu kingine ambacho kinahitaji maelezo kamili. Hii faida ya kuridhia leo tumekuwa tukilipia gharama kabla hatujaridhia kwa muda wa miaka yote. Hebu Mheshimiwa Waziri atufafanulie, leo tukiridhia hizi gharama tulizokuwa tunalipia zitapungua au zitakuwa zilezile? Ikiwa hazitapungua ni kwa nini tulazimishwe kuridhia leo na wakati wote ule tulikuwa tunalipia gharama kabla ya kuridhia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu Mkataba kinazungumzwa kitu *OAU* na mpaka tunaletewa katika Kamati hakijabadilishwa pamoja na kwamba sasa hivi tuna *African Union*. Sasa hili moja katika jambo ambalo hata katika Kamati tulilieleza kama tatizo kwa sababu isingepaswa mpaka leo pamoja na marekebisho yaliyofanywa huko Misri kwa nini leo tuletewe kila kitu *OAU*?

Hii kidogo haileti picha nzuri. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu patizamwe mbali na faida tulizoelezwa lakini kile kilichojificha katika upande mwingine wa shilingi tuelezwe kwanza ndiyo tupate fursa ya kusema tunauridhia au hatuuridhii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Mkataba huu wa Umoja wa Posta Afrika. Sekta ya Posta nchini inaonekana kurudi nyuma na haiendelei kutokana na kukua kwa Sayansi na Teknolojia, masuala ya utandawazi na soko huria. Ni kweli kwamba wananchi walio wengi nchini hapa sasa tunatumia mawasiliano ya kisasa zaidi kuliko utumiaji wa posta lakini bado Watanzania walio wengi vijijini wanahitaji huduma hii ya posta. Nilitaka niulize Wizara ni kwa namna gani imeweza kujipanga kukuza hii sekta ya posta, kuboresha miundombinu ya posta ili hawa Watanzania walio wengi ambao bado wanahitaji huduma hii waweze kufaidika na huduma hii? Lakini ni namna gani Wizara kwa kuridhia mkataba huu, sekta yetu ya posta hapa nchini inaweza kukua na kuwasaidia hawa Watanzania ambao bado wanahitaji huduma hii? Pia nilitaka kuiuliza Wizara kuhusu ukuaji wa teknolojia, je, unaweza kumudu changamoto za utumiaji wa posta hapa nchini? Ni vyema ningepatiwa majibu haya ili tuone kwamba wananchi wanafaidika namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia suala la anuani za makazi. Nchi nyingine Barani Afrika ziko mbele sana katika utumiaji wa hizi anuani za makazi lakini kama nchi na Wizara imejipanga vipi? Utaona kwamba anuai za makazi ni pamoja na kuwepo na mitaa, nchi yetu tunajua kuna ujenzi holela, hakuna mitaa, hata kama mitaa imeainishwa lakini ni namna gani wananchi wanajua mitaa hii inaitwaje, ni namna gani wananchi wataendelea kupewa elimu na kunufaika na anuani hizi za makazi? Sasa Wizara pia ituambie ni kwa kiasi gani imejipanga kutoa elimu hii kwa wananchi lakini ni namna gani hili suala ambalo nchi nyingine zimepiga hatua kwa kuridhia mkataba huu, hili suala la anuani za makazi litawasaidiaje wananchi wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane pia na Wabunge wengine waliozungumzia suala la utumiaji wa lugha ya Kiswahili. Tumeambiwa kwamba Makao Makuu ya Mkataba huu yatakuwa Arusha kwa maana ya Tanzania lakini sisi kama nchi lugha yetu kuu ya mawasiliano ni Kiswahili. Tunawezaje kuweka Kiswahili nacho kiwe *official language* katika Mkataba huu ili Kiswahili nacho kiweze kutumika. Lakini nitoe wito kwa watendaji wote au kwa Serikali, inapoenda kuridhia Mikataba ya namna hii au kutoa mapendekezo mbalimbali kabla ya kuridhiwa na Bunge, ni lazima watie msukumo na kuthamini lugha yetu ya Kiswahili, tuone kwamba Kiswahili ndiyo lugha yetu tuendelee kuikuza na iweze kuijengea heshima nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami sitakuwa na mengi sana ya kuchangia lakini ningependa tu kuuliza maswali mawili, matatu kwa lengo la kupata ufafanuzi kwa sababu tunaingia katika soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi niungane na wenzangu kuunga mkono hoja ya kuridhia mkataba huu muhimu. Lakini pia lazima tujiulize maswali ya msingi, tunapotaka kuingia kwenye ushindani lazima tujiulize maswali ya msingi ya kutosha. Nilikuwa pia napitia hapa taarifa ya Kamati na taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani inasema tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Afrika mnamo mwaka 1980 mwaka ambao mimi nimezaliwa lakini huduma za posta nchini bado zinaendelea kusuasua na naungana kabisa na mchangiaji aliyepita Mheshimiwa Pindi Chana bado huduma zetu za posta katika *level* za Kata, *level* za Wilaya bado hazifanyi kazi kulingana na mazingira tuliyopo. Hata nikitolea mfano leo hii tuna Benki za Posta katika Mikoa mingapi, kuna Benki za Posta katika Wilaya ngapi? Kwa hiyo, bado tunatakiwa kama Tanzania tuendelee kuhakikisha tunaboresha huduma za Posta hapa nchini ili tuweze kushindana na wenzetu. Sasa hilo nilikuwa naomba sana kulisisitiza kwa sababu hata kizazi hiki cha *digital* nadhani huduma za posta hazipo kwa sababu huduma nyingi wanazipata katika mitandao, wanazipata katika *blogs* mbalimbali. Sasa tuna *challenge* ya kuhakikisha tunakabiliana na soko la ushindani na hasa katika huu mfumo wa sayansi na teknolojia. Hili pia nilikuwa nimependa kulisisitiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaporidhia mikataba mbalimbali au tunapoingia katika umoja mbalimbali, kilio kikubwa sana cha vijana wa Tanzania ni kukosa fursa na naomba nitolee mfano kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini nitolee mfano tu kwenye sehemu ndogo ya hoteli, vijana wetu wamekosa fursa ya kupata ajira katika nchi za wenzetu ambazo tunaingia nazo kwenye umoja. Sasa tunaenda kuridhia Umoja huu wa Posta kwa nchi za Afrika, ningependa kujua kama Wizara imejiandaa vipi kimkakati kwanza kuwapa elimu vijana ambao tayari wapo katika mfumo kwamba wanaenda kwenye soko la ushindani lakini wamejiandaaje kimkakati kuhakikisha wanawapa mafunzo ya kuwawezesha wao kumudu hili soko la ushindani na hata pia kuhakikisha vijana ambao wana taaluma husika kupata ajira na kufaidika na Umoja huu tulionao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo ambalo nilikuwa nimependa kusisitiza lakini na mimi sina mchango mwingine kikubwa tunatakiwa tuhakikishe tunaboresha huduma za Posta ili Umoja huu uweze kuwanufaisha vijana wetu, ili Umoja huu uweze kutoa fursa kwa vijana wa Kitanzania pamoja na nchi yetu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo kuhusiana na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika kwa maana ya *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo ambayo ukipitia Mkataba yanashangaza na lazima tuyazungumze, tuyapatie majibu. Jambo la kwanza, Mkataba unasema waliposaini, wakaidhinisha kwamba Makao Makuu ya Umoja wa Mashirika ya Posta Afrika yawe Arusha nchini Tanzania lakini mpaka sasa hivi naamaanisha miaka 32 tangu waliopoanza kusaini haya masuala, nchi ambayo ndiyo Makao Makuu yalipo hatujaridhia huo Mkataba yaani hapa ni uzembe au ni nini? Unajua ni kitu cha kushangaza kuwa umepewa Makao Makuu, kuna nchi zingine hazina Makao Makuu zenyewe zimeridhia Mkataba na kusaini lakini sisi ambao tuna Makao Makuu hatujasaini; lakini hatujaridhia. Hili swali ni nani ambaye anapaswa kujibu? Kama tunakwenda kwa mfumo wa namna hii, sisi ambao tuna haki na ndiyo wenye Makao Makuu maana yake ni kwamba huu Mkataba tunaoridhia hautakwenda na wala hatutafikia yale malengo ambayo tumejipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mpaka sasa hivi tuna wanachama watano tu na tangu ku-*sign* ni mwaka 1980 maana yake ni kwamba miaka 32 imepita walioridhia ni watano, mimi sitaki miaka mitatu baada ya kufanya marekebisho kule Misri, ninataka nitumie tangu walipo-*sign* mwaka 1980 maana yake ni miaka 32 walioridhia ni watano na wanahitajika watu 22 katika nchi wanachama 44 maana yake sasa tunahitaji miaka 140 ili tupate wanachama 17 wa ziada kwenye ku-*sign* Mkataba huu. Kama tunakwenda kwa mfumo huu, maana yake tunakwenda kuridhia Mkataba ili tu wale watu wanaohudhuria hivi vikao waendelee kupata posho na ku-*attend* vikao lakini haitakuwa na mantiki nzima kwa ajili ya msaada wa hili Taifa.

Tunapaswa kuelezwa na Serikali hali ya Mashirika ya Posta Afrika yapo katika hali gani kwa sababu kinachoonekana mashirika mengi ya Posta ni yale Mashirika ambayo yanakuwa yako *owned* na Serikali kwa maana ya nchi husika. Sasa mashirika mengi ambayo yanashikiliwa au yanaendeshwa na Serikali yamekuwa hayafanyi vizuri na mfano hai ni Shirika la Posta la kwetu nchini, ni Shirika ambalo tunaweza kusema kuwa limekufa, sasa kama kuna mashirika mengine yamekufa maana yake tunaendelea kuidhinisha au tunaendelea kuridhia Mikataba ya Mashirika yaliyokufa sasa faida yake ni nini? Haya ndiyo masuala ambayo tunahitaji kuyapata kabla ya kwenda huko ambako tunahitaji kuridhia huu Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na gharama ambazo zimekuwa zikilipwa miaka yote ya nyuma sasa tungependa tufahamu ni nani alikuwa anaidhinisha hizo gharama, kwa idhini ya nani, kwa Sheria ipi iliyowapa mamlaka kwa sababu unaporidhia Mkataba maana yake sasa tunasema kulingana na Mkataba ulioridhiwa na Bunge limepitisha basi ninyi ndiyo mna haki ya kuingia rasmi katika huo Umoja wa Mashirika ya Posta. Kwa hiyo, tunahitaji kufahamu haya masuala na tunatakiwa tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, niliomba zaidi kwenye Mkataba wa baadaye na wenyewe nitachangia lakini tunahitaji maswali hayo kabla ya kuridhia huu Mkataba. Naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Eng. Mfutakamba atakuwa ni msemaji wa mwisho na tukirudi Mheshimiwa Waziri atasoma Azimo la pili, halafu Mwenyekiti wa Kamati atasoma maoni ya Kamati na Msemaji ya Upinzani atasoma maoni ya Kambi ya Upinzani na baadaye tunawachangiaji kama watano wataanza kuchangia.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia. Kwanza, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Kaimu Katibu Mkuu, kwa kuwasilisha Azimio hili linalohusu Mkataba wa Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, niunge mkono hoja kwa 100%. Pamoja na Mkataba huu kuletwa leo hapa sisi kama Watanzania tuna fursa kubwa kwa sababu tuna mkataba huu na tunaweza kupata nafasi na fursa nzuri ya kuuboresha kwenye sehemu ambazo zina upungufu. Wale ambao tayari wameridhia tunaweza kuwafuata ambao ni nchi rafiki, tunaweza kuboresha ule upungufu ambao unaweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la anuani za makazi zitaturahisisishia kupata barua na vifurushi na uchumi utakuwa kwa haraka zaidi pia biashara kama *E-Commerce*, masuala ya *E- Goverment* pia yatakuwa na uharaka zaidi wa utekelezaji, kuna suala pia la usalama, kama anuani za makazi zinafahamika na pia suala la huduma kama za afya na matumizi rahisi ya *GPS*, hii ni fursa nzuri ambayo mimi ningeomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tupitishe na turidhie Mkataba huu haraka iwezekanavyo ili faida zote hizi ziweze kupatikana.

Hata utaratibu wa usafiri ukiwa na *GPS* ile anuani huambiwi ukifika mahali kata kona kulia, kushoto na kadhalika lakini *system* ya *GPS* na anuani za makazi zitatusaidia zaidi kwenda sehemu moja na kurudi, kama kuna shughuli ya sherehe au shughuli za dharura na faradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la lugha. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwenye Mkataba zimezungumzwa lugha mbili, sisi tuna fursa nzuri kwa sababu wiki jana hapa tumezungumzia suala la Kiswahili na mimi ninaamini tukiweza kujumuisha lugha ya Kiswahili katika shughuli za *PAPU*, itakuza fursa nyingi zaidi za matumizi ya Kiswahili, Kiswahili kitaongeza masuala ya utamaduni, Kiswahili pia kitakuwa ni lugha moja ambayo ninaamini kabisa *Microsoft,* wataalamu wetu Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwenye *IT* kule wameshaanza kuiweka katika *system* mbalimbali za *computer.* Hii ni fursa nzuri, tumechelewa lakini tumepata nafasi nzuri ya kuweza kutumia lugha yetu ya Kiswahili kwa matumizi ya *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kwamba tukitaka kuongeza lugha zaidi ya Kifaransa na Kiingereza, sisi tungewaomba Wizara wanapokwenda katika majadiliano kule kwenye *Convention* wawataarifu kuwa hata lugha ya Kiingereza na Kiswahili, hawa wanaochangia ndiyo wanaogharamia, sasa iweje sisi tunachangia kwenye Kiingereza, tunachangia kwenye Kifaransa, tunaposema tuongeze na Kiswahili, nimeona kwenye Mkataba wanasema hiyo nchi inayotaka au wanayotaka kuongeza lugha moja ni lazima wagharamie wenyewe, hiyo siyo sahihi.

Hoja hapa ni kwamba tunaongeza fursa za watumiaji wengi katika *Convention* hii kwa hiyo lugha ya Kiswahili ilipiwe kama vile Kifaransa na Kingereza kinavyolipiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la wao kutuletea sisi masharti kwamba unapotaka kuongeza lugha nyingine lazima ulipie, mimi ninafikiri siyo sahihi na siyo halali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wanapokwenda kwenye *Convention* kule waeleze hii ni lugha moja inafahamika na inatumiwa na wananchi mbalimbali. Kwa hiyo, nayo itumike na iweze kuwa moja ya lugha kubwa ambazo zitatumika katika kuendeleza shughuli za *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, mimi naomba tuunge mkono Azimio hili ili Wizara iende ikafanye kazi na tuweze kufaidika kwa kiasi kikubwa badala ya kusema turudi, twende, turudi haitusaidii ndugu zangu, tuunge mkono hoja na mimi ninaunga mkono hoja 100%, ahsante sana. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ENG. MOHAMED JUMA HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa kwa Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo wako kwa nia ya kuweka kumbukumbu vizuri katika *Hansard*.

Kabla ya Mheshimiwa Rajab hajatoa taarifa kwa mzungumzaji Mheshimiwa Wenje pale kuhusu kuchanganya haya Maazimio na lililokuwa limewasilishwa, mchangiaji Mheshimiwa Zambi baada ya kuhitimisha na maelezo yake mazuri aliunga mkono akasema, anaunga mkono Maazimio yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninataka mwongozo wako aweze kurekebisha *Hansard* kwa kusema kuwa anaunga mkono Azimio moja tu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mnyaa, ni kwamba hatuwezi kusema tunaunga mkono Maazimio yote mawili wakati Azimio moja lilikuwa halijawasilishwa. Kwa vile tutakaporejea saa kumi na moja Mheshimiwa Waziri atakuja kusoma Azimio la Bunge la Kuridhia Katiba na Mktaba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika wa mwaka 1999 yaani *Constitution and Convention of the African Telecommunications Union* kwa ufupi *ATU*, halafu Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Mkataba huu atasoma maoni ya Kamati yake na baadaye Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani atatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio hilo la Bunge. Baada ya hapo tutafanya mjadala ambao mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Wenje, atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk,Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Freeman Mbowe, hawa watachangia tutakapomaliza baadaye Mheshimiwa Waziri atafanya majumuisho kwa Maazimio yote mawili na Bunge tutalihoji kuridhia Maazimio yote mawili.

Kabla sijasitisha shughuli hizi, nina tangazo kutoka Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, nilitangaza kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo aliwaomba Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha wakutane ukumbi wa Pius Msekwa saa saba. Pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo, wanatakiwa pia Wajumbe wa Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira lakini vilevile na Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria wote kwa pamoja Kamati hizo tatu wakutane pale.

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia niwakumbushe kuwa kuna semina inaendelea ukumbi wa *African Dreams* saa saba. Kwa hiyo, tutakwenda kule na baada ya semina hiyo tutarejea hapa, saa kumi na moja tuwe ukumbini.

Baada ya matangazo haya, ninasitisha shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika wa Mwaka 1999 *(Constitution and Convention of the African Telecommunication Union (ATU) of 1999)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika *(Constitution Convention of the African Telecommunication Union (ATU)* ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kwa maelekezo na michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili, wakati wa vikao vilivyofanyika baina ya Kamati na Wizara yangu kati ya Tarehe 1-2 Novemba, 2012. Napenda kuwahakikishia Wabunge wa Kamati kwamba michango yao tumeithamini na pia tumeifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu mapendekezo ya kuridhia Katiba na Mkataba uliokusudiwa ambao ninaliomba Bunge lako Tukufu liweze kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Mawasiliano Afrika ni wakala maalum wa Umoja wa Afrika *African Union* (AU) ambayo Makao Makuu yake yapo Jijini Nairobi Nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja huu ulianzishwa rasmi tarehe 7 Disemba, 1999 baada ya kubadilishwa jina kwa kuwa uliokuwa Umoja wa Mawasiliano Afrika *Pan African Telecommunications Union (PATU)* ulianzishwa tarehe 7 Disemba mwaka 1977 chini ya uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, *Organization of African Union* (OAU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya kubadilisha jina la umoja yalichukuliwa kwa lengo la kuupa nguvu zaidi umoja huo katika kuongeza ushirikiano na kusimamia maendeleo ya miundombinu na huduma za Teknolojia, Habari na Mawasiliano TEHAMA katika Bara la Afrika. Aidha, mabadiliko haya yalikusudiwa kuruhusu aina mpya ya uanachama ikiwemo wanachama makampuni binafsi yanayotoa huduma za mawasiliano pamoja na kuwezesha umoja huo kukabiliana na changamoto za mabadiliko na kasi ya ukuaji wa TEHAMA duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa jumla ya nchi 17 zimekwisharidhia Katiba na Mkataba wa Umoja huo. Mkataba huo ulianza kutumika rasmi tarehe 28 Aprili mwaka 2007 mara baada ya nchi kumi kuwasilisha hati za kuridhia kama inavyotakiwa na Katiba ya *ATU*. Tanzania kama mwanachama wa Umoja huo, bado haijaridhia Katiba na Mkataba japokuwa imeendelea kutimiza masharti mengine ya uanachama ikiwepo kulipa ada na kushiriki mikutano mbalimbali ya kimaamuzi ya Umoja huo. Hii ni pamoja kushiriki kwenye Baraza la Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowasilisha kuridhiwa ni Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano wa Afrika ambazo zilipitishwa na nchi wanachama mwaka 1999 ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya Katiba. Katiba imegawanyika katika sura sita. Sura ya kwanza inaelezea uanzishwaji, dhima na dira, madhumuni, muundo, uanachama na lugha rasmi ya Umoja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya pili inazungumzia muundo wa utendaji wa umoja huo unaojumuisha mkutano mkuu, baraza la utawala, mikutano ya watalaam na Sekretarieti ya Umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya tatu, inazungumzia hadhi ya kisheria na hati/makubaliano ya Umoja huo, ambazo zinajumuisha hadhi ya kisheria, uhuru wa nchi mwanachama, haki na wajibu wa mwanachama na wanachama shiriki, uridhiwaji wa Katiba na Hati za Makubaliano, kukubali Katiba na Mikataba, Kanuni na

Utaratibu za Umoja, kusimamishwa Uanachama, kurudishiwa uanachama na utekelezaji wa hati/makubaliano na Katiba ya Umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya nne inazungumzia masuala ya fedha ya Umoja. Aidha, sura ya tano inazungumzia masuala ya uhusiano baina ya Umoja huo na Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine na sura ya sita inazungumzia kupoteza uanachama, mabadiliko ya Katiba, kuanza kutumika kwa Katiba na kusainiwa kwa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mkataba maudhui yake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya kwanza inazungumzia Mkutano Mkuu ikiwa ni pamoja na uthibitisho wa washiriki katika Mkutano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya pili inazungumzia Baraza la Utawala na uwakilishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara ya tatu inazungumzia sifa na uteuzi wa Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nne inahusu Kamati za Kitalaam na Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tano inafafanua kuhusu washiriki wa mikutano ya kitaalam na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya sita inazungumzia ushirikiano na misaada ya kitalaam katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya saba fursa za uhusiano kati ya Umoja na Jumuiya za Kimataifa, ushirikiano wa kitaalam na lugha rasmi za umoja huo zimefafanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nane inahusu taratibu za kujitoa na marekebisho na utekelezaji wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika ni pamoja na Tanzania kushirikiana na nchi zingine za Afrika katika masuala mbalimbali yenye manufaa kwa nchi ikiwemo kuliunganisha Bara la Afrika kimawasiliano. Nchi yetu tayari imenufaika kwa kuziunganisha nchi jirani kwenye Mkongo wa Taifa wa mawasiliano na mikongo ya baharini, kuainisha sera na miongozo ya udhibiti ya kisekta na kutangaza vivutio na fursa za uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Mikataba ya Kimataifa ya aina hii inapaswa kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** Umoja wa Mawasiliano Afrika ulianzishwa kwa lengo la kusimamia maendeleo ya miundombinu na huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Bara la Afrika;

**KWA KUWA** Tanzania kama nchi mwanachama haijaridhia Katiba na Mkataba wa *ATU* ingawa inaendelea kutimiza masharti mengine ya uanachama ikiwemo kulipia ada na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimaamuzi ya Umoja huo;

**KWA KUWA** baada ya kuridhia Katiba na Mkataba wa *ATU* Tanzania inaweza kushirikiana kikamilifu na nchi nyingine wanachama katika kukuza ushirikiano katika masuala ya utafiti na maendeleo, kujenga uwezo wa kitalaam na kuweka mikakati madhubuti ya kuendeleza miundombinu na huduma za TEHAMA ikiwemo la kuliunganisha Bara la Afrika na Dunia kupitia huduma za mtandao wenye ubora na kwa gharama nafuu;

**KWA KUWA** Sera ya Taifa ya Mawasiliano *(National Telecommunication Policy)* ya mwaka 1997 inaagiza kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika sekta ya mawasiliano ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na teknolojia hii ya TEHAMA;

**KWA KUWA** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina jukumu la kuridhia Katiba na Mikataba inayohitaji kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 naomba kunukuu:

“Kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, Bunge laweza kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa” mwisho wa kunukuu.

**KWA KUWA** hakutakuwa na gharama ya ziada kwa Tanzania kuridhia Katiba na Mkataba huu zaidi ya kulipa ada ya uanachama ya kila mwaka kiasi cha shilingi bilioni 40 za Kitanzania ambayo Tanzania imeendelea kulipa;

**HIVYO BASI** ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika “*The Constitution and Convention of of the African Telecommunication Union”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ninamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kutoa maoni ya Kamati kuhusu kuridhia Katiba na Mkataba huu.

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasoma mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia bila kujali itikadi ya vyama vyetu. Naomba waendelee kunipa ushirikiano huo na waendelee kuniamini, nami kamwe sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawapongeza viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi walioshinda uchaguzi katika nafasi mbalimbali za uongozi wa Chama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba nisome maoni ya Kamati hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la kuridhia Katiba na Makataba wa Umoja Mawasiliano ya Simu Afrika wa mwaka 1999 (*Constitution and Convention of the African Telecommunication Union of* 1999).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, iwapo Bunge lako Tukufu litaridhia Azimio hili, nchi yetu itapata manufaa yapatayo:-

(i) Kushirikiana na nchi nyingine kukabiliana na changamoto zinazokabili mawasiliano ya simu katika nchi zetu kutokana na mabadiliko ya kasi ya sayansi na teknolojia.

(ii) Kunufaika katika kubadilisha utalaam, mafunzo, ufundi, tafiti mbalimbali zitakazoongeza tija katika nyanja za mawasiliano ya simu.

(iii) Kushamirisha sera ya Taifa ya Mawasiliano ya mwaka 1997 inayoagiza kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika sekta ya mawasiliano ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na TEHAMA.

(iv) Kwa kuwa, nchi yetu inaendelea kulipa ada kwa ajili ya uanachama wa Umoja huu, kuridhia Azimio hili kutahalalisha sababu za malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupokea maelezo kutoka Serikalini kuhusu Azimio hili, Kamati ilijadili na kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa Ibara ya 3(d) ya Katiba ya Umoja huu inasema lengo ni kukuza rasilimali watu kwa kutoa mafunzo, Kamati inashauri kuwa, kuwe na mpango mahsusi wa kuandaa Watanzania kunufaika na mafunzo haya.

Aidha, kwa kuwa nchi yetu inatoa michango katika Umoja huu na Jumuiya zingine zinazofanana na hii, Kamati inashauri Bunge hili

lijulishwe nchi imenufaikaje kwa upande wa ajira. Wapo Watanzania wangapi na katika ngazi zipi kwa kuzingatia Ibara ya 8(4)(g) ya Katiba ya Umoja huu ambayo inaeleza kuwa kutakuwa na ajira ya kada mbalimbali.

(ii) Ibara ya 6 ya Katiba ya Umoja huu inaeleza kuwa lugha rasmi ya Umoja huu zitakuwa ni Kiingereza na Kifaransa, Kamati inashauri kuwa Umoja huu upo chini ya Umoja wa Nchi za Afrika, pia Bunge la Afrika ambalo lugha zinazotumika ni pamoja na Kiswahili, yaani Kiingereza, Kiarabu, Kifaransa, Kireno na Kiswahili. Ni vema Umoja huu ukachukua sura ya Umoja wa Afrika na Bunge la Afrika ili Kiswahili kiwe Lugha rasmi ya Umoja huu.

(iii) Ibara ya 26 ya Katiba ya Umoja huu inaitaka nchi mwenyeji kuukopesha fedha Umoja iwapo kwa wakati huo Umoja huo hauna uwezo wa kifedha. Kamati inashauri uwekwe muda maalum wa Umoja huu kulipa nchi husika fedha zake ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na matatizo ya kifedha.

(iv) Ibara ya 27 ya Katiba ya Umoja huu inaeleza kuwa nchi itakayofanya utafiti kwa msaada wa Umoja huu haitalazimika kugharamia yenyewe shughuli za utafiti husika. Kamati inataka kupewa maelezo kuhusu Ibara hii kwani matokeo ya utafiti huo yanaweza kuwa ni manufaa kwa Umoja huu, la sivyo nchi iliyofanya utafiti ilipwe iwapo matokeo ya utafiti yatakuwa na manufaa kwa Umoja huu

au nchi nyingine mwanachama irejeshee nchi iliyofanya utafiti husika sehemu ya gharama ya utafiti huo.

(v) Ibara ya 2 (2) (2.2) inaeleza kuwa Wanachama kutoka kila Kanda watapendekeza kwenye Mkutano huu, mtu mmoja atakayegombea nafasi katika Baraza la Umoja huo. Hata hivyo Kamati inashauri kila nchi mwanachama ipendekeze mgombea wake kwani Kanda haziko kwenye Muundo wa Umoja huu.

(vi) Ibara ya 7 (6)(6.2) inaeleza kuwa nchi itaendelea kulipa ada na kutekeleza majukumu mengine hata kama imesimamishwa uanachama. Kamati inaona kuwa jambo hili si sahihi kwani nchi iliposimamishwa uanachama pia inakosa manufaa yatokanayo na kuwa mwanachama hivyo kuendelea kulipa ada na kutekeleza majukumu mengine itakuwa ni hasara kwa nchi husika.

(vii) Katika mawasiliano ya simu kwa sasa kuna uwezekano wa kuwa na laini moja kutumika na ikipigiwa na kupatikana mtumiaji akiwa nchi yoyote (*roaming*). Hata hivyo pamoja na kuwa na umoja huu baadhi ya mitandao iliyo na utaratibu huu wa *roaming* hautumiki katika baadhi ya nchi. Kamati inashauri kuwa umoja huu ufanye juhudi kuhakikisha kuwa kunakuwa na mawasiliano bora katika nchi zote zilizo katika umoja huu.

(viii) Kifungu Na. 7 (6) kinaeleza kuwa nchi inaweza kufukuzwa uanachama kwa sababu, pamoja na mambo mengine, ya kuwa na sera tofauti na za Umoja huu. Kamati ina wasiwasi iwapo sera zote za mawasiliano katika nchi wanachama zinafanana kutokana na mazingira tofauti ya kibiashara, kisiasa na kijamii.

(ix) Azimio hili lilianzishwa mwaka 1999, linaletwa leo baada ya miaka 13 kupita na wakati huo huo nchi yetu imekuwa ikilipa ada ya kiasi cha Sh.40,000,000/= kwa mwaka kwa miaka yote hiyo. Ni imani ya Kamati pia kuwa kwa kutoridhia Azimio hili nchi yetu haijanufaika na Umoja huu. Hivyo utaratibu huu uepukwe kwani unalitia hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Prof. Makame Mnyaa Mbarawa na Naibu Waziri Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Florence Turuka na Wataalam wa Wizara hiyo kwa kunipa ushirikiano wao na kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kazi waliyoifanya ya kuchambua Azimio hili kwa kina na kunipa heshima ya kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Inocent Edward Kalogeresi, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli na Mheshimiwa Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Mheshimiwa Prof.Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Munde

Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Sara Msafiri Ali, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati hii ipasavyo. Aidha, nampongeza Katibu wa Kamati hii, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi, kwa kazi nzuri ya kuandaa taarifa hii kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, Kamati kwa ujumla wake haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa Azimio hili na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuliridhia ili kuendeleza ushirikiano wa nchi za Afrika katika masuala ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni haya, Kamati yangu inaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Nakushukuru Mheshimiwa Kabati. Sasa namwita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano ya Afrika. Mheshimiwa Nassari, karibu!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii na naomba sasa nisome hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhusu Azimio la Kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano ya Simu Afrika ya Mwaka 1999 yaani *(Constitution and*

*Convention of the African Telecomunications Union of 1999)* chini ya Kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haipingani na hoja iliyopo mbele ya Bunge lako ya kuendeleza mahusiano yaliyopo katika nchi za Afrika ikizingatiwa Mkataba huu ulishasainiwa na Serikali baada ya kuanzishwa rasmi mnamo mwaka 1999, hivyo ni vema Serikali ikazingatia suala la kupanua wigo wa majadiliano ndani na nje ya Bunge juu ya Mikataba mbalimbali ambayo Serikali imekuwa ikiingia katika Jumuiya za Mashirikiano tofauti hususani Mkataba huu ili kuweza kupata michango muhimu kutoka kwa wadau na kuweza kupata zaidi mitizamo mbadala ambayo inachangia katika kuboresha ushiriki wa manufaa na hivyo kuepusha Taifa kutumbukia katika hasara pale Mikataba inapokuwa haina manufaa kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kuridhia Katiba na Mkataba huu ni vema Serikali ikakumbuka kwamba hivi sasa ni ndani ya Mkutano huu wa Bunge mnamo tarehe 1 Novemba, 2012 Bunge liliridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Katika Katiba Ibara ya 6 na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika katika Ibara ya 7 kifungu namba 5(1) kinaelekeza lugha rasmi za Muungano zitakuwa Kiingereza na Kifaransa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia hatua zilizofikiwa na Bunge hili Tukufu za kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Tume ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuona umuhimu wa kushawishi nchi wanachama wa Umoja wa Mawasiliano ya Simu Afrika kuingiza katika Katiba na kutambulika kama lugha rasmi za

Kiafrika ambazo zilikubaliwa na Umoja wa Afrika kuwa lugha rasmi ambazo ni Kiarabu, Kireno na Kiswahili. Pia kama ilivyoelekezwa na kukubaliwa katika Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika (*Pan African Postal Union)* katika Ibara ya 5 nanukuu:-

*"The official languages of the union are Arabic, English, Portuguese and Swahili".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hitaji la Kikatiba na Mkataba katika Ibara ya saba 7 ya Mkataba kifungu cha 5(3) kutaka nchi zenye uhitaji wa kuingiza lugha yake kama lugha ya kazi kugharimia gharama zote za matumizi ya lugha husika, ni vema Serikali ikaona hili kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutumia fursa iliyopo ya ushirikiano wa Afrika Mashariki na kuhakiki kwa pamoja kama wanachama walioridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Tume ya Kiswahili hivyo kushiriki kuipeleka katika Umoja huu ili ikubaliwe kuwa lugha ya kazi kama moja ya lugha za asili ya Kiafrika kuwa miongoni mwa lugha za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa kupitia Ibara ya 8 ya Mkataba kifungu cha pili (2) kinachotoa fursa ya kuwasilisha mapendekezo katika Mkutano wa Jumuiya kwa nchi wanachama na hoja kupitishwa kutokana na wingi wa kura, ni dhahiri fursa hii ni njema kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kushawishi nchi wananchama kuingiza lugha moja yenye asili ya Kiafrika hususani Kiswahili ili itumike kama lugha ya kazi katika shughuli za Jumuiya pasipo nchi husika kugharimia hivyo Jumuiya kugharimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ambayo inanekana ni mazoea ya Serikali katika masuala mbalimbali ya Kimataifa, Serikali hii kwa mara nyingine tena toka iweke sahihi Mkataba huu mwaka 1999 leo hii ndio unaletwa Bungeni ambapo ni miaka kumi na tatu hadi kufikia sasa, ikizingatiwa masuala ya mawasiliano yanawekewa kipaumbele kikubwa sana duniani na ni nyenzo mojawapo ya kuelekea kwenye maendeleo lakini cha kushangaza Serikali iliweka Katiba na Mkataba huu kabatini bila kuletwa Bungeni kuridhiwa na kuanza kupata faida za Umoja huu katika masuala ya mawasiliano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito maalumu kwa Serikali kutochelewesha mambo muhimu kama haya kwa ajili ya mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Ibara ya 15 kuzungumzia kutoingiliwa kwa uhuru wa kila Taifa kujiamulia mambo yake yenyewe kuhusu mawasiliano Katiba na Mkataba huu haujaweka msisitizo wa kulinda mila na desturi zetu kama Waafrika katika mawasiliano. Jambo hili limekuwa likiachwa mara kwa mara lakini kutokana na mwingiliano katika masuala ya mawasiliano, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni vizuri kama Taifa tukazingatia masuala ya mila na desturi zetu kwa ajili ya kupanuka kwa wigo wa mawasiliano na hivyo mila na desturi zimeanza kumomonyoka jambo ambalo lina athari kubwa katika kujenga misingi ya kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Hotuba yake ya Bajeti Kuu ya mwaka wa fedha 2012 ambayo niliisoma hapa, tulipendekeza umuhimu wa kuanzisha Mamlaka ya

Maendeleo Vijijini kwa ajili ya kuongeza kasi ya maendeleo ambapo tulipendekeza kuboresha miundombinu pamoja na kuanzisha viwanda vya kusindika mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani katika Katiba ya Umoja wa Mawasiliano unaopendekezwa Ibara ya 3 (d) inazungumzia kuwa na programu maalumu kwa ajili ya mawasiliano Vijijini hasa kwa nchi zinazoendelea. Hili ni jambo muhimu sana hasa ukizingatia kuwa hata katika mawasiliano ya simu maeneo mengi ya Vijijini hakuna mawasiliano mazuri ya simu na hili linatokana na makampuni mengi ya simu kujikita Mijini. Ni vyema basi tukaelezwa utekelezaji wa Sheria iliyopitishwa na Bunge mwaka 2006 inayoitwa "*The Universal Communications Service Access Act, 2006*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwa sababu mara kadhaa wamekuwa wakiomba Serikali kusisitiza makampuni ya simu kujenga minara kwa ajili ya maeneo yao Majimboni, mathalani baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Tabora hayana mawasiliano ya simu hasa katika Kata ya Kiloleli, Wilaya ya Sikonge, Kata ya Miyenze, Wilaya ya Uyui na kadhalika. Hali ni hiyohiyo katika Kata ya Lwezera Wilaya ya Geita, nako mawasiliano ya simu pamoja na umeme ni tatizo kubwa kwa wananchi hivyo Katiba na Mkataba huu ni muhimu sana kwa kuwa lengo mahsusi ni kuchochea masuala ya mawasiliano hasa katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa moja ya malengo ya Katiba na Mkataba huu ni kuwa na mpango wa kubadilishana wataalamu wa masuala ya mawasiliano,

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali sasa kuona ni vema kama Taifa tukawajengea uwezo wataalamu wetu wa ndani ili kuweza kuhimili ushindani katika tasnia ya mawasiliano na nchi nyingine kwa sababu mpango huu hauwezi kuwachukua watu ambao uwezo wao ni mdogo kuliko nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya rejea ya Hotuba yetu ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia hapo mwezi wa Saba mwaka huu, tulitaka kujua juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* kuhusu kupata mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kuelewa uhalifu na kubaini *sms* (ujumbe mfupi wa maneno) zinazoweza kutumwa kutoka kwenye mtambo wa Gi2 na kuonyesha kuwa *sms* hiyo imetoka kwenye namba ya mtu mwingine wakati mhusika na namba hiyo hana taarifa na hilo, suala hili linajulikana kama "*sms spoofing*" kwa kitaalamu na ili kuweka kumbukumbu sawa ni kwamba kulitokea tuhuma humu ndani ya Bunge juu ya Mbunge kumtumia Mbunge *sms* za kumtishia maisha. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ushahidi ili kumaliza migogoro ya kiteknolojia pale inapotumiwa makusudi kwa nia ya kuhatarisha maisha ya mtu. Mbali na kuridhia Mkataba huu, ni lini hasa Serikali itaweka Sheria kuthibiti matumizi ya taarifa za "*sms spoofing*" hapa nchini au kukubaliana na matumizi yake au kupiga marufuku matumizi ya mtambo unaofanyakazi hiyo "*spoofing*"?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kujiunga na ushirikiano huu baada ya kuridhia ni dhahiri ile teknolojia ambayo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* hawana au wanashindwa kuipata sasa wataweza kuipata kupitia ushirikiano huu kama msaada kutoka kwa nchi zingine mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa Joshua Nassari kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaanza majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Ezekia Wenje atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe, atakuja Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, atakuja Mheshimiwa Rajab Mbarouk na tutamaliza kama orodha itakuwa hivihivi na Mheshimiwa Assumpter na Mheshimiwa Mangungu. Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Katika Mkataba huu ambao tumeletewa sasa tujadili ni Mkataba ambao ulisainiwa mwaka 1999, sasa toka mwaka 1999 leo ndio umeletwa Bungeni mwaka 2012, ni kama miaka kumi au na zaidi. Sasa ndani ya miaka kumi, ni muda mrefu ambapo mambo mengi yanatokea, ugunduzi wa sayansi na teknolojia umeshabadilika, ukiangalia hata mazingira ya biashara ya *Telecom* yameshabadilika. Kwa hiyo, muda wa miaka kumi ni muda mrefu kiasi kwamba mazingira yaliyotengeneza Mkataba huu ukiangalia na leo ni mazingira ambayo ni tofauti sana. Sasa ushauri wangu

kwa Serikali ni kwamba tunapokuwa na Mikataba kama hii ya Kimataifa iwe inaletwa mapema ili Bunge lako liridhie katika kipindi ambacho mazingira ambayo hizo Sheria zinatengenezwa na Mkataba wenyewe uwe unaendana na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika huo Mkataba, *Article 3(h)* inaongelea namna ya kuleta usawa katika biashara ya mawasiliano na huu Mkataba unasema kwamba kazi ya hii *committee* au kazi ya huu Umoja, mojawapo itakuwa ni kazi ya ku-*harmonize tariffs* yaani bei ya mawasiliano katika nchi mbalimbali, lakini nashangaa kama huu Mkataba ulitengenezwa mwaka 1999 na nimeona kama nchi 26 ndio nchi ambazo tayari zimesha-*sign* huu Mkataba, kwa nini? Bado ukiangalia bei ya mawasiliano labda nchi ya Burundi ukilinganisha na bei ya mawasiliano labda Uganda na Tanzania bado kwa nini kuna tofauti? Kwa sababu naamini kwamba tuki-*harmonize,* tuki-*standardize* bei ya kupiga simu katika nchi mbalimbali wanachama hizi nchi 26, naamini itakuwa nafuu hata kwa Mtanzania hapa anayetaka kupiga simu Burundi au anayetaka kupiga simu Zambia katika hizi nchi wanachama. Sasa kama lengo ni ku-*harmonize* hizi *tariff,* naomba wawakilishi wetu wa Tanzania katika huu Umoja, jambo hili lisukumwe sana,

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kutumia Ibara ya 8(2) ya huu Mkataba, inayotoa fursa ya nchi wanachama kupeleka mapendekezo, najaribu kupendekeza kwamba mambo ya kuweka sawa katika *Telecom,* katika sekta hiyo ya mawasiliano isiwe mambo ya bei pekee yake, *tariff*, ikiwezekana tupeleke, tu-*standardize* yaani *investment*,

uwekezaji unaofanyika katika sekta ya mawasiliano, zile *incentives* ziwe sawa ili kama kuna mtu anakuja ku-*invest* labda Kenya ambayo ni nchi mwanachama katika nchi hizi 26, *investment policies* kwa maana za *incentives* ziwe sawasawa na Tanzania. Hii itatupunguzia hii *crisis* ambayo iko leo kwamba katika nchi za Afrika Mashariki kwa mfano tuna mashindano makubwa sana ya kupunguzia kodi wawekezaji, mashindano yanayofanya Serikali zetu zinapoteza pesa nyingi ambazo zingekuwepo katika *form* ya kodi ili kurekebishia wananchi mambo mengi katika huduma. Kwa hiyo, tusi-*harmonize tariff* pekee yake, twende katika mbinu, namna tunavyoweza ku-*standardize* hata hizi *incentives* za *Telecom Investment Companies* zinazokuja katika hizi nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini isiishie hapo tu. Kwa nini leo kwa mfano, katika hizi nchi wanachama 26, kwa nini ukienda Uganda, *Telecom Companies* ambazo labda zimewekeza Uganda, kwa nini zilipe kodi kubwa kuliko labda wanaowekeza Tanzania na nimeona katika hizi nchi wanachama, nafikiri Ghana pia ni wanachama. Sasa kama Ghana wana mfumo ambao wanaweza wakapata kodi nyingi kwa maana kwamba waka-*monitor revenue* ambazo kampuni za simu zinapata, sasa ifikie wakati tuige basi mambo mazuri yanayofanyika katika nchi nyingine ili ku-*standardize* na sisi pia tuweze kupata *revenue* katika *Telecom Sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ni muhimu sana kwangu. Huu Mkataba utatusaidiaje katika kurekebisha na kuboresha demokrasia za kisiasa kutumia *telecommunication?* Nikiwa na maana gani? Inapofika

kwenye kipindi cha uchaguzi, hii mifumo ya mawasiliano ya *Telecom* inatumika vibaya sana, kuna wengine wanatuma hata *message* mbovu sana dhidi ya wagombea wa vyama vingine, lakini inafikia wakati kuna *fear* mpaka kwa *Telecom Companies*. Nchi kama kwetu kwa mfano makampuni ya mawasiliano, inafikia wakati chama cha upinzani kinaenda kuomba kwa mfano kutumia mfumo labda wa simu kuwasiliana labda na wanachama wake, *telecom companies* kwa *investment system* ya nchi kama yetu wanaogopa. Yaani unakuta vyama vya upinzani hawawezi wakapata fursa sawa ambayo Chama cha Mapinduzi inaweza ikapata kutumia fursa za *telecom* katika kufikia wapiga kura kwa sababu kuna *fear, investors* wanaogopa.

Sasa mimi nilitegemea mikataba kama hii Kimataifa itatusaidia pia kuweka mazingira ya kutumia *telecom industry* katika ku-*promote* demokrasia katika nchi wanachama na hii ni muhimu sana na kama tunaweza tukaisukuma kwa sababu demokrasia kama iko pana na iko *stable* ndio nchi itapata amani hii tunayotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachotaka kuzungumzia ni kwamba mkataba kama huu ndio umetusaidia au umetuwezesha kupata hata *fibre optic network,* hii *cable* ambayo tunasema mkongo wa mawasiliano, lakini mimi kama Mtanzania, mwananchi wa kawaida anayetoka huku chini sija-*feel,* sijui kama Wabunge wenzangu wengine mnaionaje hili. Naomba Serikali itupe tathmini kwamba baada ya kuunganisha mkongo wa mawasiliano, gharama za mawasiliano Tanzania zimerudi chini kwa kiasi gani na hata tuseme *speed* ya *internet* kwa mfano Tanzania imeboreka kiasi

gani? Kwa hiyo, tungeomba tupate tathmini ili tujue kama kweli kuingia kwenye *fibre optic* ambao ni mkongo wa mawasiliano ambao huu Mkataba pia upo, je, imetuboreshea chochote? Ningependa Mheshimiwa Waziri nipate taarifa hizo kutoka kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho ni kwamba ukiangalia huu mkataba, makampuni makubwa ambayo yame-*feature telecom* Tanzania naona *TTCL* tu na *ZANTEL*, lakini kwenye soko la mawasiliano *telecom* Tanzania kuna *players* wengi, wapo watu kama akina *VODACOM*, wako watu kama kina *AIRTEL*, wapo watu kama *TIGO*, kuna *SASATEL* sijaona kama wame-*feature* kwenye huu mkataba. Kwa hiyo, napenda pia Serikali ituambie hawa wengine wanakuwa *involved* vipi kwa sababu nimeona tu jina la *TTCL* pamoja na *ZANTEL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Wenje kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu, japo mchango wangu kwa kweli, utakuwa ni mfupi sana. Nimesoma makabrasha mbalimbali ambayo Serikali, kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, imetuletea na nimehoji sana, umuhimu wa sisi kushiriki katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, kwa bahati mbaya sana na labda Mheshimiwa Waziri, atatusaidia katika hatua za majumuisho, Mkataba huu hauwafungi wanachama. Mkataba huu unaruhusu *Member States* na unatoa kabisa *sovereignty,* yaani hauingilii *sovereignty* ya *Member States.* Bado Taifa lolote ambalo limeridhia na kusaini Mkataba huu, linapewa Mamlaka na lina uhuru kwa Mujibu wa *Article 15,* ambayo inazungumzia, *Sovereign Rights of Member States of the Union.* Kwamba, unaweza ukawa mwanachama wa umoja huu, lakini bado una mamlaka ya kujiwekea utaratibu wako mwenyewe unavyopenda kwa ndani; kwa hiyo, hakuna *any enforcement mechanism* katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli Mkataba huu ni Mkataba wa Kirafiki, hauna kipengele chochote kinachomfunga mwanachama yeyote kufanya lolote na hakuna mamlaka yoyote ya umoja huu, kuingilia nchi nyingine yoyote katika kujaribu kuwasaidia ku-*regulate Telecom Industry* katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambacho kilikuwa kinani-*concern* zaidi ni Serikali, kutokujiandaa vya kutosha. *With due respect,* Serikali, inapoleta hoja kama hizi, *whether* ni nzuri ama ni mbaya, tunategemea wafanye *home-work* yao kidogo, waweze kuwafahamisha Wabunge kwamba, kwa miaka 13 pengine ambayo tumekuwa wanachama wa umoja huu, kimefanyika nini? Ni nini *status* ya umoja huu? Kuna faida gani kweli kweli ya kuwa kwenye umoja huu? Kimetusaidia nini? Kimeharibu nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumeletewa orodha ya *Member States* na *Associate Members* ambao wapo, ambao Mheshimiwa Wenje, amewazungumzia hapa kidogo kwamba, kwa upande wa Tanzania, tunakuwa *represented* na wale *Stakeholders* ambao hawana hata zaidi ya 20% ya soko la sekta hii tunayoizungumza. Lakini je, nina hakika kuna nchi nyingine ambao wameridhia Mkataba huu, lakini hawalipi *subscription.* Kama wasipolipa *subscription* ina maana wana haki, kwa mujibu wa *Article 20,* wana haki ya kuwa *suspended.* Lakini hatuna habari yoyote kama kuna mtu yeyote ameshawahi kuwa *suspended?* Hatuna taarifa ni wangapi wamebaki kuwa *active members?* Hakuna *enforcement mechanism* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hapa linaridhia kitu leo, ambacho naamini idadi kubwa ya Wabunge hapa ndani, hawajui hiki kitu ni nini na wala kinafanyaje kazi kwa sababu, Serikali, haikutusaidia kutuletea taarifa kidogo ya ziada angalau kujua *status* ya Taasisi tunayoizungumza mahali hapa. Kwa hiyo, niombe tu siku zijazo kwa faida ya Taifa, Serikali, mnapokuwa mnatuletea Maazimio kama hayo, wapeni Wabunge, taarifa zaidi za ndani, ili hata tunaposhauri, tuweze kushauri vitu ambavyo tunavishauri *from an informed position,* kuliko katika hatua ambapo sasa watu wanazungumza tu mambo ambayo ni ya jumla jumla na kwa kweli, hatuna uwezo sana wa kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi nataka nilizungumze hilo moja tu la msingi kwamba, hatuna mamlaka ya kubadilisha chochote katika Mkataba huu; tunaweza kuuridhia ama kutokuuridhia. Lakini vile vile tunaweza tukawekewa utaratibu wa kutoa mawazo yetu

kwa Serikali, ili Serikali mtakaposhiriki katika vikao vingine, kwa mfano, tuna Mkutano mwingine wa *EU Conference,* wana *Conference after every four years.* Ile *Conference* ndio ina *mandate* ya kuweza kufanya *any amendment* katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Bunge hili litaridhia leo, lakini biashara yake itaishia pale. Kwa hiyo, ni vema Serikali, mkawa mnatusaidia kwamba, mnapokuwa mnafikiri tunakwenda *Conference,* mnatutayarisha mapema. Wabunge, wanaweza wakatoa ushauri ama wakatoa mapendekezo mbalimbali kuhusiana na namna ya kuboresha Mkataba huu, kwanza uweze kupata *enforcement mechanism* kwa sababu, hakuna *enforcement mechanism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni Mkataba wa kirafiki kama Mkataba wa Mahusiano Binafsi, ambao kwa kweli, hauwezi kuingilia Taifa lolote. Kwa hiyo, mtu kuwa *member* ama kutokuwa *member* hakumwathiri na hatujui sisi kama Taifa tumeathiriwa kwa kiwango gani na Sheria zetu za ndani kwa kutumia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilipenda kuzungumza hoja hiyo moja tu na niishie hapo, nikiiomba Serikali, kwamba, katika siku za usoni tafadhali mfanye *homework* yenu kidogo; mkituletea kitu hapa, mtuletee kitu ambacho kidogo kimefanyiwa tafiti kidogo. Tuweze angalau kukaridhia kitu ambacho tunakijua basi kwa sababu, hiki sio kitu kipya, ni kitu kimekuwepo *for the last 13 years.* Kama kitu kinakuwepo kwa miaka 13 ina maana kuna mambo yamefanyika; Makao Makuu yako Kinshasa,

hatujui kama bado yako Kinshasa na hatujui kama yamekuwa Kinshasa kwa miaka 13?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungetegemea Serikali, ituletee *brief* kidogo tu kwamba, hiki kitu kimeanza miaka 13 iliyopita. Kimetoka hatua moja, mbili, tatu, kimepata vikwazo moja, mbili, tatu na sasa tuko kwenye *position* fulani, ili Wabunge tukitoa ushauri, tutoe ushauri ambao kidogo una-*logic* kuliko ushauri wa jumla jumla ambao tunakuwa tunautoa hapa wakati Mkataba wenyewe hau-*bind any Member State* kwa jambo lolote lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio hilo tu naomba niwasilishe kwa ajili hasa ya mambo ya siku za usoni. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nina mambo matatu ya kujaribu kuchangia kwenye Hoja hii, japokuwa wenzangu wamezungumza. Lakini nataka nijikite tu katika maeneo hasa hili linalonisikitisha la kwamba, Mkataba huu ni karibu miaka 13 sasa, ndio unaletwa hapa Bungeni ili Bunge liuridhie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa wenzangu wamefafanua ni kwamba, pamoja na umbali wa miaka 13, bado umekuja kwa haraka-haraka na *information* hazikuwa sawasawa. Kitu ambacho ukiangalia *context* ime-*change,* mazingira ya miaka 13 iliyopita yamebadilika, uelewa wa watu umebadilika, lakini Serikali, inaonekana huu ni utamaduni kwamba, wanajua wakileta kitu chochote

Bungeni, Wabunge huwa wanapeleka tu. Niungane na Mheshimiwa Wenje, alisema siku moja kwamba, Bunge hili, hata Sheria halitungi, ila linapitisha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba heshima ya Bunge; Mheshimiwa Waziri, hebu tuheshimu heshima ya Bunge na Serikali itimize Wajibu wake, ione Wabunge, tuna wajibu na sisi tunawawakilisha wananchi. *Information* kama hizi tungeletewa mapema tukazijua, tukajadiliana, tukashauriana, tukaona yapi ni mazuri kwa mustakabali wa Taifa hili. Badala yake, *it seems Government* mna-*take for granted* kwamba, tukiwapelekea hawa jamaa tunawaswaga tu; kitu ambacho sio kizuri sana. Ningeomba Wabunge, mambo kama haya tuyakemee kwa pamoja kwa sababu, hayana afya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika Ibara ya 8(2), kinachotoa fursa ya kuwakilisha mapendekezo katika Mkutano, kama ambavyo Kambi ya Upinzani imependekeza maoni yake, inaonesha katika Mkataba huu kwamba, lugha zinazotakiwa kutumika ni lugha mbili, yaani Kifaransa na Kingereza; ambapo, juzi hapa kama Bunge, tumeridhia *protocol* ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ulikuwa ni wakati muafaka kwa sababu katika Mkataba huu inaonesha kwamba, nchi inaweza ikaamua kutumia lugha zile na kugharamia yenyewe kupata watafsiri na nini. Lakini nadhani kwa Serikali, sasa ni wakati wa kushawishi nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba, tuhakikishe tuna-*push* Kiswahili chetu ili kwa kushirikiana na tugharimie wote kwa

pamoja kiingie katika Mkataba huu, ili isaidie kuki-*boost* kwa ajili ya maendeleo na manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kwa kutumia hii Ibara ya 8(2), ambacho kina fursa ya kutoa mapendekezo; Tanzania tumekuwa na matatizo sana ya bei za simu. Vile vile, siku moja nimezungumza tumekuwa na matatizo ya hizi *drop calls, e-mail* zinakatika uko kwenye *Skype*, mtu unafanya mitihani yako, haiko *reliable;* sasa kupitia Mkataba huu Serikali, inawezaje kwenda kusaidiana na nchi zote, tukilinganisha na nchi nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia mambo ya *internet* ukilinganisha na *South Africa,* tuna bei kubwa sana sisi. Ni namna gani Serikali, inaweza ikasaidia kuhakikisha kwamba, inapenyeza kujaribu ku-*regulate* haya mambo kusudi wananchi wa Tanzania, waweze kunufaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili la lugha ningeweza kusema Serikali, sijui ilichukua jukumu gani inapokaa na kwamba, tuna lugha zetu za Kiafrika. Ni kwa nini, mlipokuwa mnaingia kwenye Mikataba hii mnashirikiana nao, kwa nini hamku-*push* kuwa na *native languge?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa- *colonized* na hao Wafaransa, tumekuwa-*colonised* na hao Wazungu; bado tunashindwa kujiamini kwamba, tuna lugha zetu *native?* Kwa mfano, Kiswahili ni lugha nzuri, kwa nini ninyi mliokuwa mnashiriki hamkujaribu ku-*push* mambo haya, ili tuwe na *native language* ambayo tunaweza tukaji-*express* vizuri kwa lugha yetu wenyewe? Ambapo tunaweza tukajieleza, tukahakikisha; Wataalam wanasema, mtu anajieleza vizuri

kwa lugha yake mwenyewe kuliko kuiga lugha za kigeni, ambao huu ni ukoloni mambo leo ambao tunatakiwa tuutoe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hili suala la kuchelewa katika miaka 13, naomba tu Serikali, ielewe kwamba, haya ni mazoweya machafu ambayo tungependa iyaache. Kwamba, umekuwa ni utaratibu wa Serikali, muda mrefu mambo mengi utakuta yanaamuliwa, kuna urasimu usiokuwa na sababu, ulimwengu sasa hivi unakwenda kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungeiomba Serikali, hebu twende na wakati, mambo yanapokwenda wananchi waarifiwe, wananchi wawe-*informed* kwamba, hiki ndicho kinachotokea, tunatakiwa tutoe maamuzi. Miaka 13 ni mingi sana, kwa hiyo, huu utamaduni wa kuchelewa chelewa ndio umezoeleka. Mambo hayaendi kwa *speed* kulingana na ulimwengu, unakwenda *speed* sana. Ukiangalia *IT* inakwenda *speed* sana, ukichelewa miaka miwili, mitatu, imekuacha. Kwa hiyo, ni lazima twende na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu, aliwahi kusema sisi tunatambaa wakati wenzetu wanakimbia. Kwa hiyo, hebu kwa pamoja tushirikiane kama Bunge, tuishauri Serikali, iende na kasi. Mambo kama haya ambayo ni ya sisi sote tufahamishane mapema, ili tusaidiane kwa pamoja kwa ajili ya uchumi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa tena nafasi, ili niweze kuchangia katika *Convention* hii, ama kuridhia au kutokuridhia. Kwa sababu, mnapotuletea kwamba, turidhie tu maana yake ni kwamba, mna uhakika kwamba, sote tuliomo humu tutaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu mpaka manne, lakini la kwanza kabisa, nataka kusema kwamba, CCM acheni ubishi wenu; hii nchi mnaipeleka pabaya na mtatutia katika mashimo ambayo kwa kweli, vizazi vyetu vinavyokuja vitakuja kutulaumu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengi tumeyatoa. Binafsi yangu nimependekeza kwamba, jamani Muswada huu hebu kwanza usiletwe Bungeni, vipengele vingi humu ni vya Kisheria, vinahitaji kuvijadili kwanza na ikiwezekana basi, pafanywe Semina kwanza kwa Wabunge, waelimishwe juu ya mambo haya, lakini hamtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nataka niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa sababu, hawa ndio walioweza angalau kufichua haya madudu yaliyokaa huku miaka na miaka bila ya kuletwa hapa Bungeni. Kwa kweli, sitosita kumshauri Profesa Lipumba, mwaka 2015 wakati anaunda Serikali yake, kuwachukua hawa vijana, kwa kweli, wanaweza kuisaidia nchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze na *Article Number (4)* ya huu Mkataba. *Article Number (4)* inasema: *Composition of the Union;* Muundo wa hii *Union.* Muundo

wa hii *Union* unasema kwamba, *Member State shall be any Member State of the OAU.* Hebu Mheshimiwa Waziri, naomba unisaidie, hivi kuna *OAU* tena dunia hii? Vipi mnatuletea kitu ambacho sijui ukisemesemeje, *OAU* iko wapi? Sasa hivi hakuna tena *OAU,* sasa hivi kuna *AU;* kwa hiyo, ina maana huu Mkataba sisi tuupitishe tu hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo, mbali ya kipengele hicho cha *(e),* ambacho kinasema *Member State* lazima awe ni Mwanachama wa *OAU,* lakini hapa kuna kingine kinasema kwamba, *any African State not a Member of OAU which, appears on Membership of this Union.* Lakini na kingine kinasema *any Member State which, loses its Membership of the OAU,* au mmetumia Kipengele hiki? Kwamba, mmeshapoteza ule uanachama wa *OAU* kwa sababu, haupo? Kwamba, sasa hivi ndio mnataka kuingia katika Mkataba huu? Naomba hili mtuweke sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la lugha. Naungana na wenzangu kwamba, kwa kweli, kuna kila haja ya kutaka kutumia Kiswahili. Ila nakwambia Mheshimiwa Waziri, kwamba, uwezo wa kutaka kufanywa mabadiliko katika hili, unao. Kwa sababu, kwa kutumia Mkataba huu huu na Katiba hii hii, basi kimo Kipengele ambacho wewe kinakuruhusu kupeleka mapendekezo yako. Naomba pendekezo la mwanzo utakalolipeleka liwe la kufuta ile *OAU* humu ukaweka *AU;* lakini la pili ni kupendekeza kutumika kwa Kiswahili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa iko *amendment of the Convention, Article Number (8).* Imesema, *a Member of the union may propose any amendment to this Convention.* Kwa hiyo, hiki Kipengele kipo kinakuruhusu na wewe ndiye ambaye kwa mujibu wa Mkataba huu, utakayeongoza jopo la Wataalam wetu wa Tanzania, watakaokwenda katika Mikutano hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba haya mapendekezo ambayo Wabunge wanayatoa basi uyaharakishe kuyafanya kama ni *proposal* na uyapeleke, ili yaweze kufanyiwa kazi; bila hivyo, usikubali kuingia katika huu Mkataba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee mbele kidogo. *Accreditation of Delegation to the Conference.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa, *Delegation* ambayo inatakiwa iende katika Mikutano hii ambayo itakuwa na *right* ya kuweza kusaini *final Acts,* ni lazima kibali chake kitokane na Rais ama Waziri wa Mambo ya Nje. Mmetuingiza mkenge katika Mikataba mingi ya Kimataifa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, neno Mkenge, lifute. Sio msamiati wetu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi najua wewe unalifahamu, lakini inawezekana kweli, wenzetu wengine wakawa hawalifahamu; mmetupeleka pabaya katika Mikataba

mingi, sasa naiomba Serikali, kwa kweli, muwe makini katika suala hili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mchungaji Msigwa hapa, *speed* sasa hivi ya *IT* ni kubwa duniani. Pale kitakapokuja kibali kutoka kwa Rais, wakienda watu tu mambumbumbu, kwa kweli kuna hatari ya kuja kuipeleka hii nchi pabaya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Rais, atakaporuhusu watu wa kwenda kule; atakapotoa kibali kwa watu wale ambao watakwenda kufanya *final,* basi wawe ni watu wazuri. Wawe ni Wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la hawa *Member States and Associate Members.* Hivyo, nataka nijue Mheshimiwa Waziri; hapa umetuonesha kwamba, nchi wanachama au wanachama washiriki, tumekuta kwa Tanzania wako *Zantel* pamoja na *TTCL;* hivyo, inaonekana kwamba, huu Mkataba wakati unataka kuletwa hapa, haukuita *Stakeholders* wengine? Au kuna nini ambacho mlikifanya ili hawa *Stakeholders* wengine wasiingie? Kwa sababu, hapa namkuta *Vodacom* yupo, lakini wa Afrika Kusini, sio wa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalieni *TTCL* ana mapato gani? Sasa hivi *Vodacom* ana *transaction* ya *above seven trillion* kwa mwaka ya hizi *M-Pesa* na mambo mengine madogo madogo. Leo ni kwa nini asiingie katika kitu kama hiki? Ni kitu gani kimewakwamisha Mawaziri, ili msiwashawishi hawa na wao waweze kuingia hapa? Leo

tumefika mahali wananchi wanachukua simu nne nne, tano tano mfukoni. Hivi mmewashirikisha vipi katika kulizungumza hili? Tunataka kuingia katika ushirikiano na wenzetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri kwamba, hili mliangalie upya. Bado muda mnao, vipengele vinawaruhusu vya kwenda kufanya *amendment,* ili *proposal* yenu muweze kuipeleka kama kuongeza au kupunguza. Yashawishini na Makampuni mengine yaweze kujiunga kwa sababu, haya haya ndio yanayosababisha haya Makampuni ya Simu mpaka leo yakawa hayataki kuingia katika masoko haya ya hisa. Mpaka leo hapa *Dar-es-Salaam Stock Exchange,* hawajaingia akina *Vodacom* kwa sababu, njia ndio hizi hizi wanamopenya. Mnashindwa kuwashawishi; hili naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimalizie kwa *TTCL.* Kwa kweli, *TTCL* wana hali ngumu, ngumu, ngumu kabisa; hawana uwezo wa kuingia ushindani na nchi yoyote ya Kiafrika, hawana. *TTCL* sasa hivi wanachokitegemea kikubwa ni Mkongo wa Taifa. Huo wanautegemea lakini hawana *Management,* hawana kingine chochote; kwa kweli, kuna haja ya Serikali, kuwekeza zaidi katika *TTCL,* ili angalau *TTCL* iwe inaweza kuingia katika mashindano au kushindana na baadhi ya nchi, kukimbizana na suala zima la ukuaji wa *IT,* tutake tusitake, *TTCL* ndio roho ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa nchi uko pale, siamini kwamba, nchi hii inaweza kuachia mawasiliano yote yakawa huru watu wakafanya wanavyotaka, siamini;

naamini kwamba, *TTCL* ndio roho ya nchi. Naiomba sana Serikali, tuzidi kuwekeza katika *TTCL. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kabisa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, yupo hapa na ananisikia. Ili nisiendelee kulumbana na Waziri wako, naomba Ofisi ya *TTCL* Pemba, ijengwe. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mawazo yangu juu ya kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano ya Simu Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maswali yetu siku zote yatabaki kuwa yale yale, unaposaini mkataba miaka kumi na tatu iliyopita kwa maana ya mwaka 1999, halafu hauridhii, mantiki yake ni ipi? Haya ndiyo maswali, tunahitaji majibu, unaposaini mkataba mwaka 1999 halafu hauridhii, unamaanisha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ukiangalia katika hali ya kawaida mwaka 1999 kwa mfano, mimi peke yangu nilikuwa niko sekondari, sasa mkataba uliosaniwa mwaka 1999, leo ndiyo nakuja kuupitisha kama Mbunge, kweli inaleta mantiki ya kawaida hapa? Sasa kama mwenendo ni huu kwamba mikataba inakaa kwa muda mrefu ni mikataba mingapi imesainiwa haijaletwa ndani ya Bunge. Sasa hii ndiyo ambayo tunatakiwa Serikali ijue kwa sababu hapa inaonesha kabisa kwamba, Serikali haiwajibiki ipasavyo kwa wananchi wake na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia katiba inavyoonyesha ibara ya 8(2) tangu mwaka 1999 watu wamekuwa wakienda kwenye mikutano mikuu ya Shirika la Umoja la Simu Afrika mara nne, kwa sababu mkutano mmoja huwa unafanyika kila baada ya miaka minne, lakini watu wamekuwa wakienda wanarudi, wakienda wanarudi bila kuleta taarifa yoyote ndani ya Bunge, miaka kumi na tatu, tunakwenda wapi katika mfumo huu wa kuiongoza nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na sisi hatupendi kuendelea na *business as usual* na tungependa moja ya mkataba wa leo na Katiba ya leo ambayo inatakiwa iridhiwe, Bunge sasa vile vile liende kuamua kwamba Mikataba yote iliyozidi zaidi ya miaka mitano iliyosainiwa nyuma sasa iletwe Bungeni na ipitishwe mara moja ili watu waweze kujua ukweli hatuwezi kuendelea na michezo hii kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine inatakiwa tafsiri na nilizungumzia wakati wa Shirika la Posta, unapolipa ada ambayo wewe unashiriki lakini haujaridhia tafsiri yake vile vile ni nini. Kwa hiyo, tuelezwe na Serikali tunalipa ada, lakini hatujaridhia maana yake vitu vingine huwa vinachanganya, hujaridhia kitu halafu unatoa maana yake ni nini! Kwa hiyo na yenyewe tunasema ni kukiri udhaifu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tunakwenda kwenye ibara ya 15 ambayo katika Mkataba huu inazungumzia uhuru wa mwanachama kujiamulia mambo yake mwenyewe. Sasa tulikuwa tunategemea Mkataba

huu uwe na mantiki moja kubwa kwamba, uwe una uwezo wa kuingilia nchi wanachama katika masuala mazima ya biashara ya simu na mambo mengine ikiwemo uendelezaji wa soko wa biashara ya makampuni ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa kampuni inasema; nchi inaweza kujiamulia na tunaposema nchi inaweza kujiamulia maana yake ni nini? Maana yake sasa ndiyo unakuja katika nchi yetu kuna misamaha ya kodi, vipindi vya neema kampuni inakuja inakuwa miaka mitano hailipi kodi haiwezi kusimamia bei zake na haiwezi kufanya jambo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mwenendo maana yake hatufanyi kitu chochote kwa sababu mkataba utakuwa hautusaidii chochote, lakini tungekuwa na uwezo kama kampuni inaweza kuruka isilipe kodi kwa mfano, tunaambiwa yanabadilisha majina kutoka *Airtel* sijui *Zain* na vitu gani huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hali ni hii, maana yake tungekuwa tuna uwezo kama nchi kwenda katika umoja wa mawasiliano ya simu ya Afrika kwenda kulisemelea hili suala kwamba kampuni fulani imewekeza katika nchi ya Tanzania, lakini katika kipindi chote cha miaka kumi iliyowekeza imekuwa ikibadilisha majina mara kwa mara na imekuwa hailipi kodi.

Lakini hili suala halipo, sasa tunakwenda kukubali ama kuridhia mkataba wa aina gani. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo sisi tungependa kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni lazima lieleweke wazi kabisa kwamba Tanzania ni nchi ambayo soko lake la simu ni la uhakika, kwa hiyo, tunahitaji kuwa na mikataba ya kwetu wenyewe yenye nguvu zaidi, hata hii mingi ambayo inaweza kusimamia soko la simu na kuweza kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo, ukiangalia pale Benezwela Hugo Shavesi alipokuwa amechukua nchi aliamua ku-*nationalize* Makampuni yote ya Simu na ndiyo imekuwa ikipatia pato la Taifa kubwa sana ukiachia mafuta na mambo mengine, lakini Makampuni ya Simu ama Mashirika la Simu yamerudishwa kwa wananchi, yamekuwa yakilipatia zaidi mafao Taifa lao. Sasa na hii ingewezekana zaidi na ingetusaidia sana kuliko maeneo mengine kama tungeweza ku-*nationalize* vile vile Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia, ikumbukwe kabisa kwamba, mwaka 2006, tulipitisha Sheria ya Mawasiliano Vijijini. Ukipitia vilevile ibara ya tatu ya mkataba huu inazungumzia programu maalum kwa ajili ya mawasiliano ya simu vijijini, sasa ya kwetu imetushinda mwaka 2006 tunakwenda kusaini ya wenzetu wakubwa. Je, tutauweza na sasa tunatakiwa tujue, je, kwenye vijiji vyetu katika nchi nzima ya Tanzania kwa sheria tuliyopitisha mwaka 2006 kuna vinamawasiliano ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utagundua karibu asilimia 80 ya vijijini hakuna mawasiliano ya simu na watu hawapatikani, lakini leo tunakwenda kuridhia mkataba mkubwa wakati sheria ya ndani yenyewe imetushinda. Kwa hiyo, ningependa haya masuala yaweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, ni kuhusiana na lugha ambayo inatakiwa itumike, zimezungumzwa lugha mbili, Kifaransa pamoja na Kiingereza, lakini kila baada ya mikutano minne, tunaruhusiwa kwenda kufanya marekebisho yakiwemo ya Katiba pamoja na masuala mengine madogo madogo. Kwa hiyo, hili liende kama pendekezo baada ya mkutano unaofuata. Kwa hiyo, kikao kinachokuja Umoja wa Mawasiliano ya Simu Afrika wazungumzie hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa David Silinde kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Mshama, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Peter Serukamba na mwisho Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye wajiandae. Mheshimiwa Mshama, hayupo, basi namwita Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii iliyokuwepo mbele yetu leo. Lakini nianze tu kwa kuwakumbusha ndugu zetu wale ambao wamekuwa wakishutumu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba, imekuwa kaidi huku wakisahau yenyewe ndiyo

ambayo imetekeleza sera mpaka kufikia hivi sasa tuna mawasiliano haya ya simu na mawasiliano mengine. Lakini niwaambie tu hayo ni mateke ya punda anayekufa, kwa maana kwamba, tumedhihirisha uwezo bado tunao kwa kushinda chaguzi zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wazungu waliwahi kusema lugha moja kwamba *better late than never,* hili ndilo ambalo linafanyika. Wengi waliochangia wamesema kwamba, mkataba huu umesainiwa mwaka 1999, naamini labda wengine kwa kujisahau tu kwa sababu siwezi kukubaliana nao kwamba umri wao ulikuwaje mpaka wasiwe na kumbukumbu kwamba mwaka huo kampuni za mawasiliano ya simu zilikuwa ni mbili tu, *mobitel* na Kampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuweke mazingira, tulaumiane, lakini tuweke mazingira ya kukumbuka kidogo, maana yake tunaweza tukazungumza hapa *Zantel* ndiyo kampuni ya mwisho kabisa kusajiliwa, nadhani mwenzangu ulikuwa kule unalima mpunga, taarifa hizo ulikuwa huna. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi katika *article three* ya Azimio hili lenyewe imezungumzia *objective of the union*, lakini ukienda kwenye kipengele (b) imesema kwamba: "*To promote the financing and funding of telecommunication development*." Ndani ya Bunge hili mara nyingi tumekuwa tukilalamikia mawasiliano ya vijijini, lakini tunao Mfuko wetu wa mawasiliano kwa yote *UCAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaridhia hili, tunaomba Serikali sasa iongeze nguvu kupeleka mawasiliano katika maeneo ya vijijini na sasa ifike wakati wa kusahau maeneo ya mijini kwa sababu hakuna uzalishaji wa kutosha, kule ambako vijijini tunakotoka sisi wengine, ndiko ambako tunazalisha na kupeleka vyakula katika masoko kama ilivyodhumuniwa katika *objectives* hizi kipengele (e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie, wachangiaji waliopita wamelizungumza lakini kipengele cha sita ambacho kimezungumzia lugha ambayo itatumika katika Katiba hii kuwa ni Kifaransa na Kiingereza. Lakini kwa mujibu wa hotuba ya Waziri na maelezo ambayo yametolewa yameainisha kwamba, hii inatokana na Umoja wa Afrika ambao umeridhia kwamba lugha ya Kiswahili iwe miongoni mwa *official language* za Umoja ule. Sasa tunamwomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi kwamba, Kiswahili namo iingizwe kuwa ni lugha *official*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilisisitize katika hili pamoja na kuwa tumezungumzia, tumechelewa sana lakini mpaka sasa kama tulivyoainishiwa ni nchi 26 tu, lakini napenda kufahamu wakati unajumuisha ni kigezo kipi ambacho kilitumika kuweka Makao Makuu haya kuwa Kongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Murtaza Mangungu, namwita sasa Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye ajiandae. Mheshimiwa Serukamba!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuleta hoja ya kutuwezesha kupitisha Azimio hili, lakini kama walivyosema wenzangu, Azimio hili limechelewa sana, ningeomba hawa watu wa Serikali watusaidie kwa sababu watakuwa wameshasaini mkataba ule, ni muhimu sana kuleta mapema zaidi, unaweza ukaona pamoja na maendeleo makubwa yaliyopatikana na faida kubwa zilizopatikana bado naona kwa kuchelewa inabadilisha watu kutokuona hizo faida zilizopatikana kwa kujiunga kwenye umoja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiusoma mkataba huu ukasoma na *convention* yake yote unaona kwenye *industry* ya *telecommunication* bado ni *rare profession*. Kwa hiyo, unaona umuhimu wetu kama nchi tunahitaji kujiunga kwenye *board* hizi ili tuweze kubadilishana uzoefu, kubadilishana ujuzi. Kwa sababu ukiangalia kwenye vyuo vyetu vinavyofundisha *Tele-education per se* bado ni vidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Tanzania tunafanya vizuri sana katika mawasiliano ya simu, ukiangalia leo Tanzania sasa tumeanza kwenda kwenye *four G*, ni nchi chache sana Afrika ambazo zimefika kwenye *four G*, wakati tumeanza *three G*, kuna baadhi hata ya nchi za Ulaya zilikuwa hazijakwenda kwenye *three G*, lakini Tanzania tayari tulikuwa tumeshakwenda kwenye *three G* na sasa tunakwenda kwenye *four G* kwa vyovyote vile haya ni maendeleo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo *yes,* lakini tuseme ukweli, kwenye sekta hii tumefanya vizuri sana na labda niwaambie Waheshimiwa Wabunge mawasiliano kwa maana ya Tanzania *Telecommunication* Commission (*TCRA)* imekuwa *veted* kama chombo bora Afrika katika kusimamia mawasiliano ya simu Afrika, maana yake watu wetu wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya yamefanikiwa kwa sababu, ukiangalia unaona kila wakati wako kwenye *consultation* na *working group* nyingi, wanakwenda ITU, wanakwenda sasa *ATU* na yote imefanya ndiyo maana tumeweza kwenda mbali zaidi katika mawasiliano haya ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia leo tumeanzisha mkongo wa Taifa, mkongo ule kama nchi za jirani tusipoutumia tutakuwa tumepata hasara, kama nchi tumeweka fedha nyingi sana, lakini kwa sababu tunaingia kwenye umoja huu, maana yake hata nchi zinazotuzunguka zitatumia mkongo huu kupeleka *information* zao *another part* ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliweke vizuri suala la bei za simu, mwaka 2005, *GSM survey* ilionesha Tanzania tulikuwa wa pili duniani kwa bei kubwa ya simu, lakini *GSM survey* ya mwaka 2010, 2011 Tanzania sasa sisi tuna bei ya chini ya kupiga simu kuliko nchi yoyote ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu ambaye anafuatilia tuangalie sasa tuko bei ya chini kuliko nchi yoyote ya Afrika, maana yake tumepiga hatua kubwa na unaweza ukaona *penetration* yetu ya kwenda vijijini ni kubwa sana Tanzania na tusisahau kuwa, nchi yenyewe ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kusema kwamba, naunga mkono Azimio hili, ila ninachoomba kwa Serikali, maazimio haya ni vizuri yaletwe haraka iwezekanavyo. Angalia tuliingia mkataba huu mwaka 1999 na kama nchi tumeendelea kulipa kodi, kwa maana kulipa *obligation* yetu, ndiyo maana tunaendelea ku-*benefit* na hiyo mikutano. Tunakwenda kwenye mikutano yote kwa sababu tumekuwa tunalipa, lakini tumekuwa tunalipa kabla hatujaleta Bungeni ili Bunge liweze kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali kwa mikataba mingine yote twende kwenye mashelfu tuangalie ili tuweze kuileta iweze kupitishwa na Bunge, *otherwise* kujiunga kwenye *ATU* ni jambo zuri, Tanzania tumefanya vizuri sana katika mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Serukamba, sasa namwita Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye na Mheshimiwa mtoa hoja Naibu wake ataanza na baadaye atahitimisha mtoa hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mbarawa pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Januari Makamba kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya toka wamekabidhiwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mawaziri waliowatangulia wamefanya kazi nzuri kwa kuweka sera nzuri sana ambayo imetuwezesha leo hii Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza duniani kwa kuwapa watu huduma ya simu hadi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 wakati tunaanza kufanya *restructuring* ya *sector* idadi ya simu kwa kila watu 100 zilikuwa simu 36, lakini leo hii tumeshafikia karibu simu 60 au zaidi kwa watu 100. Ni hatua kubwa sana ambayo tumepiga na yote hiyo inatokana na sera nzuri, sheria nzuri pamoja na kusimamiwa ipasavyo utekelezaji wa sera hiyo pamoja na sheria. Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wote katika sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *African Telecommunication Union*, kwanza shirika hili lina historia kubwa kidogo ukianzia lilipoanzishwa ile *Pan African Telecommunication Union* mwaka 1977.

Lengo kubwa lilikuwa ni nchi za Kiafrika kutafuta namna ya kujikwamua kutokana na gharama kubwa wanayolipa kwa kusafirisha *traffic* za simu, kwa mfano, unapiga simu kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam. Itoke Dar es Salaam iingie kwenye satellite ya *Bridge Telecom,* itoke hapo iingie kwenye *satellite* ya *ATMT,* ndiyo pengine iende Washington au mji mwingine ambao inatakiwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Kiafrika zikatafuta namna gani tutapunguza gharama hizi na ndipo wakaanzisha shirika hili ambalo lilisaidia kuunganisha mawasiliano hapa Afrika. Kwa wale ambao wamekuwa wakifuatilia historia ya simu katika nchi hii, mtakumbuka tulikuwa na *network* inayoitwa *Pan Afri Tel* ambayo ilikuwa inatokea hapa Dodoma inakwenda mpaka Malawi inaenda mpaka Zambia pamoja na nchi nyingine za Afrika ambayo ilikuwa inatusaidia kuunganisha *traffic* za simu ndani ya nchi za kiafrika bila kupitia kwenye nchi za Ulaya au Marekani. Kwa hivyo, shirika hilo limefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo faida nyingi za kuwa na shirika hili, lakini moja ya faida ambazo tunaziona hivi leo ni kwamba, huu mkongo wa *East African Sub Marine System* ambao unaunganisha Afrika Mashariki pamoja na sehemu nyingine yoyote ya dunia kupitia mkongo unaopita baharini ulibuniwa na kutekelezwa kupitia shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwa kuwa na mkongo huo tunaweza kuwasiliana na sehemu nyingine zozote za dunia bila kupitia kwenye *satellite* ambayo gharama yake ni kubwa sana. Ndiyo maana bei ya simu hapa nchini inazidi kushuka siku hadi siku, yote isingewezekana bila kuwa na chombo ambacho kinatuunganisha sisi na nchi nyingine za Kiafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo faida nyingine pia ambapo kama tulivyosema ni kwamba kuna ushirikiano wa kufanya utafiti kwa pamoja na kuendeleza teknolojia ya Mawasiliano ya Simu. Tumeweza kushiriki katika utafiti huo unaosimamiwa na shirika hili pamoja na Shirika la Mawasiliano ya Simu ulimwenguni kwa maana ya A*TU* na faida zake ambazo tumezipata nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja ambazo wenzangu wameelezea kuhusu shirika hili kwamba linafanyaje kazi. Shirika hili kwa bahati mbaya lilipata kuyumba kidogo kutokana na Makao yake Makuu kuwa Kinshasa. Matatizo yalipotokea Congo shirika hili liliathirika na ndiyo ikalazimika Makao yake Makuu yaani *AU* ikaamua kwamba shirika hili lihamishwe kwa muda kutoka Kinshasa lipelekwe Nairobi ambapo ndiyo Makao Makuu ya muda yalipo mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuhamishwa huko, limeyumba kwa sababu ya hali ya kisiasa iliyopo katika nchi jirani yetu ya Congo. Lakini tunaamini kabisa kwamba kwa ushirikiano na hali ya Congo itakapokuwa nzuri wakirejea kwenye Makao yao Makuu, basi shirika litaendelea kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja ambalo ni wito kwa Watanzania, Watanzania tunapenda kubaki nyumbani, hatupendi ku-*venture* kama wenzetu. Mashirika haya sisi tunachangia fedha na tena ni fedha nyingi sana, fedha zile zinatumika kwa ajili ya kuendeshea shirika hili pamoja na shughuli zake zote. Nafasi za kazi zinapotangazwa ni Watanzania wachache sana wanaoomba nafasi hizo, maana yake ni kwamba, hatuna wawakilishi kwenye mashirika haya, sina hakika kama sasa hivi kwenye shirika hili la *the African Telecom Union* tuna mwakilishi au kwa maana ya mtumishi aliyeajiriwa na shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito tujitahidi kuwahimiza Watanzania kwamba nafasi za kazi zinapotangazwa na mashirika haya ambayo sisi ndiyo tunaomiliki, basi wajitahidi kuomba na kwa kuwa tunao wawakilishi kwenye vyombo hivyo vinavyoshughulikia ajira hizo, ni vizuri Watanzania wakaomba nafasi kwenye Shirika hili la *African Telecomm Union, Pan African Postal Union, ATU* pamoja na *UPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusirudi nyuma na mashirika mengine yote ya *AU* na yale ya Umoja wa Mataifa, tujitahidi kuomba nafasi za kazi, tuking'ang'ana kukaa huku nyumbani maana yake ni kwamba, sisi hatutapata fursa ya kutumikia Taifa letu kwa kuliwakilisha kwenye mashirika haya ambayo yanatengeneza sera pamoja na kanuni zinazosimamia sekta hizi za mawasiliano kwa Afrika na kwa Ulimwengu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, narudia tena kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na watendaji wote wa sekta hii pamoja na watoa huduma kwa maana ya *operators* wote ambao wamekuwa wakichangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Associate Membership, Associate Membership* linahusisha *operators* kwa maana ya watoa huduma, vyuo vya mafunzo yaani *training institutions* na *researchers* ndiyo wanaweza kujiunga kwa nanihii hiyo. Usipoomba mwenyewe kujiunga hutalazimishwa kujiunga, *Member States* ndiyo wanawakilisha hawa wote ikiwa hawa wanachama yaani *operators* au *Training Institute* hawajaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida wanazopata kwa kuomba kujiunga na nanihii hii, watashiriki katika *research*, watatumia takwimu na taarifa zitokanazo na utafiti huo na kwa maana hiyo zitawasaidia wao moja kwa moja kutumia takwimu hizo kuboresha huduma zao. Wasipoomba hawalazimiki kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona tu nitoe mchango wangu katika nanihii hiyo, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye kwa mchango wako na ufafanuzi ambao umeufanya. Sasa namwita mtoa hoja tukianza na Naibu Waziri Mheshimiwa January Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametolewa maoni mengi, lakini nitazungumza machache na Mheshimiwa Waziri atakuja kujibu mengi ambayo yamechangiwa na Kamati pamoja na Kambi ya Upinzani na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze tu na mchango wa Mheshimiwa Freeman Mbowe ambaye ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, amezungumza mambo mawili. Kwanza ni kwamba, mkataba huu uko *loose* au uko huru sana unatoa uhuru sana kwa nchi wanachama na hauelezi namna gani makubaliano hayo yatakuwa *enforced*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema tu ni kwamba, mikataba hii ipo ya aina mbili ya Kimataifa, kuna mikataba ambayo ni self *executor,* yaani mkataba wenyewe unasema utatekelezwa vipi na kuna mikataba ambayo siyo self *executory* na huu ni mmojawapo kwamba, nchi zinafanya makubaliano ya jumla, halafu zinapokutana zinatengeneza utaratibu wa kutekeleza yale makubaliano. Kwa hiyo, ndiyo maana mkataba huu Mheshimiwa Mbowe umeuona kama ulivyo, ni makusudi, ni aina ya mkataba ambao umekusudiwa kuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, amezungumza kwamba, Serikali haikujiandaa vizuri. Napenda nisikubaliane naye kwenye hilo.

Tumejiandaa vizuri kwa kina na sisi kama mnavyofahamu kwamba hizi Kamati zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge, sisi Serikali tumekaa na Kamati ya Miundombinu kwa siku mbili kwenye hili jambo, tumepitia ukurasa kwa ukurasa mikataba yote, tumejibu maswali yote waliyoyauliza, tumewaridhisha na ndiyo maana taarifa yao ya Kamati imesema kwamba, inaunga mkono turidhie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi imani yetu ni kwamba na kama unavyofahamu Mheshimiwa Mbowe na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye Mabunge mengine kwenye nchi zilizoendelea za kidemokrasia wakati mwingine hata haina haja kwa Bunge kukaa kama hivi wote baada ya kuwa Kamati imefanya kazi. Wabunge wanauliza tu kwamba, Kamati imesemaje? Wakisema Kamati imepita, kwa sababu Kamati tunakaa muda mrefu kwa mfano tumekaa siku mbili lakini leo tumekaa masaa machache ingekuwa si rahisi ku-*exhaust* kila kitu katika mkataba ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda tu nimhakikishie kwamba, Serikali iko makini, imefanya kazi yake na imefanya *homework* yake na imefanikiwa kuwaridhisha Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ambao mambo haya wana-*deal* nayo kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Mbowe kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki wataalam wa Wizara na taasisi ikiwemo Posta ambao wamekaa hapa muda mrefu, wameifanya hii kazi kwa kina na wametafuta majibu na wamefanya utafiti kwa kusema kwamba, hawako makini. Nadhani tutoe sifa pale inapostahili na kwa kweli Serikali imejitahidi kwenye hili jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbarouk amezungumza mambo mawili au matatu, lakini la kwanza amesema kwamba anategemea kwamba Prof. Lipumba atakapounda Serikali mwaka 2015 basi atatuchukua mimi na Mheshimiwa Waziri wangu. Kwanza nastaajabu kwamba wameshaamua kwamba Profesa Lipumba atakuwa mgombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nastaajabu kwamba, atakuwa anagombea mara ya ngapi, nadhani itakuwa ni mara ya saba! Lakini vile vile nafurahi kwamba, akigombea tena tutamshinda vile vile kama ambavyo tumekuwa tunamshinda. Lakini napenda kusema kwamba ni ndoto kwa Chama cha Mapinduzi kuondoka kwenye dola mwaka 2015. Tutaendelea kushinda na dalili zote zinaonesha kwamba, tutaendelea kuwepo madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa amezungumza jambo moja kwamba, mkataba huu umesema neno *OAU* badala ya *AU*, kitu ambacho nataka kusema ni kwamba, sisi Mheshimiwa Mbarouk tunacholeta hapa ni kwamba, tunawaletea mkataba kwa jinsi tulivyousaini hatubasilishi mkataba tukauleta hapa. Sasa utakumbuka kwamba mwaka 1999 hakukuwa na *AU, African Union* imeanzishwa Julai 9, 2002.

Kwa hiyo, naona umetumia muda mrefu sana kutulaumu kwamba mkataba ule hauna neno *AU* wakati ni dhahiri kwamba, mwaka 1999 hakukuwa na *AU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuwezi kusema kwamba, tubadilishe ule mkataba tuliosaini ili uoneshe *AU* wakati tulisaini ukiwa na *OAU*. Lakini kubwa ni kwamba, wanachama baada ya sisi kuridhia tutakwenda na ni uamuzi wa wanachama sasa kubadilisha kwa kulingana na mabadiliko yaliyotokea. Kwa hiyo, nataka tu nitoe elimu hiyo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo amezungumzia Mheshimiwa Mbarouk ni suala la ruksa anayotoa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa *delegations* kwenda kushiriki na kusaini hii mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa makubaliano ya uhusiano wa kidiplomasia Vienna ya mwaka 1961 na ndiyo utaratibu ambao unatumika kote duniani kwamba wenye mamlaka ya kusaini makubaliano ya nchi ni Waziri wa Mambo ya Nje na Rais na pale ambapo hawaendi basi wanatoa ile *accreditation* ili viongozi wengine wawakilishe na waseme kwa niaba ya Serikali na wasaini kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo, ni utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la *Associate Members* kwamba Tanzania yapo makampuni mengi ya mitandao na Wabunge wengine wamechangia vile vile. Lakini makampuni ambayo ni wanachama washiriki kwenye huu mkataba ni mawili tu yaani ni *Zantel* na *TTCL* na kwamba sasa hiyo ni lawama kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani siyo sahihi kutupia lawama kwa Serikali kwa sababu ushiriki kwa makampuni binafsi yaani *Associate Member* ni hiari. Kuna gharama ambazo makampuni yanaamua yenyewe kwamba yashiriki au yasishiriki na ukiangalia kwenye idadi ya wanachama ni wengi zaidi kuliko *Associate Members*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna nchi nyingi tena afadhali sisi angalau kwenye nchi yetu kuna makampuni ambayo yameamua kushiriki, lakini zipo nchi nyingi ambao ni wanachama ambapo hakuna hata kampuni moja imeamua kushiriki. Lakini ni vema na tutaendelea kuzungumza nao kwamba washiriki kwa sababu siyo jambo baya tukiwa na uwasilishi mkubwa hata kama ni wa *Associate Members.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kuchelewesha mkataba huu limezungumzwa sana na limezungumzwa na Wabunge wengi kwamba, mkataba huu umesainiwa mwaka 1999 na unaletwa kwa ajili ya *ratification* sasa. Tunakiri kwamba, ni tatizo na ni tatizo kubwa na mwaka 2008 Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alitoa agizo kwa Serikali nzima kwamba, mikataba yote na makubaliano yote ya Kimataifa ambayo yamelala na ambayo yanachelewa, kwa sababu hii ni michakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kusaini kule inakwenda kwenye *Cabinet Secretariat*, inakwenda kwenye *MTC*, inakwenda kwenye Baraza la Mawaziri, inakuja kwenye Kamati mpaka Bungeni. Kwa hiyo, ni mchakato ambao unachukua muda mrefu na likatolewa agizo kwamba mikataba yote hii sasa iletwe haraka na ipitishwe haraka ili tuweze kupata manufaa kamilifu katika ile mikataba ambayo tumesaini, bado hatujaipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, sisi Wizara yetu imeanzishwa mwaka 2008 na hili suala limekuwa katika Wizara mbalimbali katika kipindi kirefu. Mtakumbuka kuna kipindi suala hili lilikuwa kwenye Wizara ya Miundombinu na kama mnavyofahamu Wizara ya Miundombinu ina barabara, bandari na reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatimaye hili suala limekuja na sisi Wizara yetu tumefanya haraka, tumeamua kulileta ili tuweze kulipitisha. Lakini ni jambo ambalo tunakiri na tumeanza sasa kurekebisha na imani yetu ni kwamba, tutakuwa tunaharakisha, halitakuwa linatokea tena ila *concern* ya Wabunge tumeipata na ni *concern* ambayo ni ya kweli kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo baadhi ya mambo ambayo Kambi ya Upinzani imeyazungumza na nitaomba niyapitie haraka haraka. La kwanza ni kwamba hatua zipi zilichukuliwa na sasa hapa tunakwenda kwenye *PAPU*, zilichukuliwa na *PAPU* baada ya mkutano wa Cairo kuzingatia kuboresha na kuhakikisha Sekta ya Posta inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya makubaliano ya Cairo ya mwaka 2009 ambayo tunaomba Bunge hili liyaridhie, kazi nyingi zimefanyika kwa mfano, tumeweza kutengeneza dira, dhima na mpango mkakati wa kusaidia nchi zote wanachama na ili kuhakikisha kwamba nchi zote hizi zinakuwa na mtandao mmoja ulio imara katika kuwezesha huduma za Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kambi ya Upinzani imesema ni kwa kiasi gani nchi wanachama zinachangia kujenga jengo la Makao Makuu. Kama mnavyofahamu Makao Makuu ya Umoja wa Posta Afrika yapo Arusha Tanzania na imeamuliwa kwamba yajengwe Makao Makuu mapya pale pale Arusha na Serikali imetoa mchango wa kiwanja Arusha. Sasa Kambi ya Upinzani inauliza ni kiasi gani wanachama wanachangia kujenga jengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi ambao umechukuliwa kujenga jengo hili siyo michango ya wanachama bali sekretarieti pamoja na wanachama wameamua kwamba watumie utaratibu wa *PPP*, kiwanja kipo na kipo eneo zuri. Kwa hiyo, tushirikiane na wadau wa sekta binafsi ili nchi wanachama zisiingie gharama yoyote katika kujenga jengo hili lakini tuna jengo kubwa na la kudumu Arusha. Kwa hiyo, hakutakuwa na gharama kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kambi ya Upinzani imesema, ili kulikwamua Shirika la Posta haitoshi tu kujiunga na *PAPU* bali kuona changamoto ilizonazo katika mwelekeo wa soko lake. Ni kweli ushauri huu tumeuzingatia ni ushauri mzuri. Ni kweli kumekuwa na changamoto nyingi kutokana na maendeleo ya sekta ya mawasiliano, imetoa changamoto kwa Shirika letu la Posta na siyo Shirika la Posta Tanzania hata Mashirika ya Posta yote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, hata Shirika la Posta la *Royal Mail* Uingereza lina-*struggle* na sehemu nyinginezo. Lakini bado tunaamini kuhusu umuhimu wa Posta, bado Posta inahitajika, kuna huduma nyingine kama vifurushi na huduma nyinginezo ambazo ni muhimu Posta iendelee kutumika katika kuzikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama Serikali tumeendelea kutumia Posta kwa kiasi kikubwa ili kuliongezea nguvu na uwezo, mtakumbuka wakati wa Sensa ambayo ilikuwa ni shughuli kubwa, Shirika la Posta lilitumika vizuri, Baraza la Mitihani na shughuli nyingine kubwa za Serikali ambazo ni za kipato kikubwa ili kuendelea kuhakikisha kwamba Shirika letu la Posta linafanya vizuri na miaka inavyokwenda tunaongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge na ninyi mtumie Shirika la Posta kwani lina huduma za *DHL* na watu wengine wanazo, sasa hivi ukitaka kifurushi chako kitoke eneo moja kwenda lingine palepale mjini Dar es Salaam unaweza. Kwa hiyo, tunaomba na ninyi muwe wazalendo, mtumie huduma hizi za Shirika letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ni kufanya kile kituo cha Posta kuwa zaidi ya mahali pa kwenda kununua *stamp* na ku-*post* barua na kuchukua barua. Mambo mengi yanaweza kutokea Posta kikawa ni kituo kikubwa cha huduma zikiwemo huduma za *TEHAMA*, huduma za kuhamisha na kubadilisha fedha na vinginevyo na huo ndiyo mwelekeo mpya wa Posta kwamba siyo eneo lenye ma-*box* tu, unakwenda unanunua *stamp* na ku-*post* barua.

Waheshimiwa Wabunge, lakini vile vile kama mnavyofahamu kwamba, Serikali imefanya jambo kubwa, nadhani la kimapinduzi la kuanzisha mpango wa anuani za makazi na *symbol* za Posta. Utaratibu huu utaleta mapinduzi kwenye sekta ya mawasiliano nchini kwa sababu kuanzia sasa itawezekana siyo tu kupata barua pale unapokaa, kwa sababu kila mtaa na kila nyumba itatambulika na tayari namba hizi zimeshatengenezwa na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali na kwa sababu ni jambo mtambuka linalohusisha Serikali katika ujumla wake hasa Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba vibao vinawekwa kwenye mitaa na namba zinawekwa kwenye mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na mfumo huu, bado itahitajika kuwe na kituo cha kupokea na kusambazia barua kwa sababu hizi *symbol* za Posta zinaishia kwenye Kata yaani zile namba zinaishia kwenye Kata. Kwa hiyo, ni lazima pawe na kituo kwenye Kata ambacho kazi yake itakuwa ni kuchukua barua na kuzisambaza katika mitaa ya Kata ile. Tunaamini kwamba utekelezaji mzuri wa utaratibu huu utaimarisha Shirika letu la Posta na utalipa *relevance* mpya katika sekta ya Mawasiliano katika ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile limeulizwa swali juu ya kuchelewa kuridhia Katiba na mkataba wa *ATU*, nimeshalizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia yapo maoni ya Kamati ya Miundombinu ambayo ningependa kuyazungumzia kuhusu *ATU*. Ulisema ushauri umetolewa kuwe na mpango mahususi wa kuwaandaa Watanzania ili kunufaika na mafunzo yanayotolewa na umoja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunalifanya, Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu fursa za ajira na mafunzo yanayotolewa na umoja huu wa mawasiliano Afrika. Lakini vile vile nafasi zimekuwa zikitangazwa na tumekuwa tunajitahidi kuzitangaza kwa Watanzania wenye sifa ili kuomba nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa taarifa ni kwamba, wakati makao makuu yakiwa Kinshasa kabla hayajahamia Nairobi katika kipindi hicho Tanzania imepata kutoa Katibu Mtendaji wa Umoja huu, hayati Rajab Yusufu. Lakini vile vile ushauri huu wa Kamati tutauzingatia na tutaendelea kufuatilia kwa karibu kuona namna gani tunaweza kunufaika na fursa za ajira zinazotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la Kiswahili limeongelewa kwamba iwe ni lugha rasmi ya umoja huu wa *ATU*. Ni kweli kwamba, kama taasisi mama ya Umoja wa Afrika inacho Kiswahili kama lugha rasmi. Waheshimiwa Wabunge tumelaumu kidogo hapa, lakini napenda tuipongeze Serikali yetu.

Ukweli ni kwamba Kiswahili kimeingizwa kwenye lugha rasmi za Umoja wa Afrika, ni jitihada za Serikali hii. (*Makofi*)

Utakapotazama tofauti kati ya mkataba ule wa *AU* na *PAPU* ni kwamba, kwenye mkataba wa *PAPU* ambao umeingiwa mwaka 2009 ambapo tayari Kiswahili kilikuwa kimeshakubalika kama ni lugha rasmi, utaona mle kwamba Kiswahili ni lugha rasmi. Mwaka 1999 kwenye mkataba wa *ATU* kilikuwa bado Kiswahili hakijakubaliwa kwamba iwe lugha rasmi, ndiyo maana haipo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaomba mridhie mkataba huu ili tupate nguvu tukishirikiana na wenzetu wanaozungumza Kiswahili ili tuweze sasa kusema kwamba, Kiswahili na chenyewe kifanywe lugha rasmi kwenye *ATU*. Kwa hiyo, litategemea na sisi kuwa na uwezo wa kura, ushiriki na uwezo wa ushawishi kwenye umoja huu na itategemea na ninyi mtakaporidhia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshauri kwamba uwekwe muda maalum wa umoja huu ili kulipa nchi husika fedha zilizokopwa katika kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza. Ni kweli kwamba, kwenye moja ya vifungu vya mkataba kipo kipengele kinachosema kwamba, nchi mwenyeji inaweza kuchangia gharama fulani pale kunapokuwa kumejitokeza tatizo na baadaye itarudishiwa. Kwa hiyo, Kamati inasema tuweke muda maalum ambao tutarudishiwa zile fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu tutauzingatia na ambacho naweza kusema ni kwamba, katika miaka yote tangu umoja huu umeanzishwa mwaka 1988 haijatokea tumetoa fedha. Hivi vifungu vinawekwa mara nyingi kwenye mikataba ya aina hii kwa nchi ambazo ni wenyeji kwa sababu kuna manufaa ya kuwa mwenyeji, lakini vile vile kuna *obligations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza ikatokea dharura fulani na kwa sababu nyie mmepewa heshima ya kuwa wenyeji, basi muwe tayari kutoa mchango mdogo na mtarudishiwa pale dharura itakapokuwa imekwisha. Lakini tunakubali kwamba ni lazima kuweka muda ili kutokuwa na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine wa Kamati unasema kwamba, nchi iliyofanya utafiti ilipwe sehemu ya gharama iwapo matokeo ya utafiti yatakuwa na manufaa kwa umoja au nchi wanachama. Ushauri tumeuzingatia. Ni kweli kwamba, katika sekta yetu ya mawasiliano, utafiti ni sehemu muhimu sana katika kubuni mbinu za kuboresha huduma na utendaji wa kazi wa taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ulisema kwamba, kila nchi mwanachama ipendekeze mgombea wake kwenye nafasi za Baraza la Umoja kwani kanda hazipo kwenye muundo wa umoja huu. Ushauri huu tutauzingatia na tutazungumza na wenzetu tutakapokuwa tumepata fursa ya kuweza kupiga kura na kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna ushauri unasema *ATU* ifanye juhudi kuhakikisha kwamba mawasiliano yanaboreshwa katika nchi wanachama. Hili ataliongelea Mheshimiwa Waziri kwa kirefu. Lakini ni kweli kabisa kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Ole Medeye, moja ya misingi ya kuanzishwa kwa umoja huu:-

(i) Ni kuharakisha mawasiliano;

(ii) Kurahisisha mawasiliano; na

(iii) Kufanya mawasiliano yawe ya bei inayowezekana kwa watu wote na yawe mawasiliano bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunataka tushiriki ili tuweze kufikia azma hizo, lakini ninachoweza kusema ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Serukamba, nchi yetu inayo sifa kubwa sana katika nchi za Afrika ambazo zimefanya vizuri katika maeneo ya kusambaza mawasiliano. Bado changamoto zipo katika maeneo ya kurahisisha mawasiliano, ambazo pia zinaikabili nchi yetu. Tutaendelea kukabiliana na changamoto hizo, lakini tunaamini kwamba, tukishirikiana na wenzetu chini ya umoja huu tutafanikiwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kamati ilitaka kujua kama sera za mawasiliano zinafanana kwa nchi wanachama. Moja ya malengo ya umoja huu ni kuwianisha sera za mawasiliano barani Afrika. Jitihada zinaendelea katika kufanya hivyo katika masuala ya msingi, kwa mfano, masuala ya ufundi, viwango na udhibiti. Hiyo ndiyo nia halisi

na kwamba ushirikiano utakuwa rahisi zaidi na utakuwa wa manufaa zaidi kama tutakuwa tuna sera ambazo zimewiana au kukaribiana katika uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani haya ndiyo ambayo nimepewa kuyazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuwasihi Waheshimiwa Wabunge tukubali kuridhia mikataba hii miwili pamoja na Katiba hii ili tukafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Makamba. Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhitimisha majumuisho. Kabla ya kutoa hoja itabidi uyasome maazimio yote mawili ili Bunge lihoji kuyaridhia. Karibu!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwashukuru sana wataalam wote wa Wizara yangu nikianzia na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Kambi ya Upinzani na Wabunge wote waliochangia kwa mdomo na kwa maandishi. Napenda kuwathibitishia Wabunge wote kuwa maoni na michango yao tumeipokea na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja kwa kuzungumza ambao jumla yao ni 18. Waheshimiwa hao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Freeman Mbowe ambaye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni; Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Rajab Mbarouk, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa *Eng.* Mohammed Mnyaa, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Goodluck Ole- Medeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya waliochangia kwa maandishi ni 13. Waheshimiwa hao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Pinda Chana, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila...

**MWENYEKITI:** Anaitwa Pindi Chana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Augustino Maselle, Mheshimiwa *Eng.* Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Suleiman Jafo na Mheshimiwa Betty Machangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza michango yote iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ni mizuri na ina lengo la kuboresha maazimio haya yote mawili. Hoja zilizotolewa zimepokelewa na Wizara itaendelea kuzifanyia kazi kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka niwapitishe kwenye hoja, kwanza za Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amejibu hoja za Kamati ya Miundombinu kuhusu *ATU*. Mimi nitajielekeza zaidi kwenye masuala ya *PAPU*. Hoja ya kwanza ya Kamati ya Miundombinu ni ushauri kwamba kuwe na mpango mahususi wa kuandaa Watanzania ili kunufaika na mafunzo yanayotolewa na umoja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri umezingatiwa. Wizara yangu imekuwa ikifuatilia kwa karibu sana fursa za mafunzo zinazotolewa na *PAPU*. Aidha, nafasi hizo zimekuwa zikitangazwa na umoja na hadi sasa zimewanufaisha Watanzania mbalimbali waliopo katika sekta hii. Kwa mfano, wataalam sita kutoka kampuni ya Posta wamepata mafunzo huko India kupitia huu mpango wa *PAPU*.

Hivi ninavyoongea kuna wataalam wawili ambao wako India kwa ajili ya mafunzo kupitia huu umoja wa *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ya Kamati ya Miundombinu ambapo imeshauri kuwa uandaliwe mkakati mahususi kuona namna nchi yetu inavyonufaika kwa kupata ajira na masoko kutokana na kuwa mwenyeji wa umoja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umezingatiwa. Mpaka sasa nchi yetu imeendelea kunufaika kwa kuwa na wafanyakazi nane (8) katika jumla ya wafanyakazi 16 walioko ofisi za *PAPU* huko Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maamuzi ya nchi wanachama yaliyofanyika Julai mwaka huu kuwa mikutano yote ya umoja wa *PAPU* itafanyika kwenye Makao Makuu ya Umoja huo, sasa nchi yetu imepata fursa kubwa ya kuwa mwenyeji wa mikutano mbalimbali ya *PAPU* ambayo itafanyika hapa nchini. Fursa hii inatoa fursa kubwa kwa ajili ya biashara, utalii na mambo mengine ambayo yanaweza kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile imekuja na hoja na imeshauri kurejewa kwa ibara ya 15 ya mkataba inayotaka nchi mwenyeji kukopesha fedha kwa umoja huo inapobidi ikiwa ni pamoja na kuongeza kipengele cha kurejesha fedha ndani ya muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umezingatiwa. Kwa umuhimu wake jambo hili ni muhimu sana na tutaweza kulizungumza mara baada ya mkataba huu kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imetoa hoja ifuatayo: Kuwepo na Ibara inayoeleza ukomo wa muda wa kurejesha mkopo na hatua itakayochukuliwa iwapo *PAPU* itashindwa kurejesha mkopo huo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umezingatiwa. Jambo hili lina maslahi makubwa ikizingatiwa kuwa PAPU iko ndani ya nchi yetu, makao makuu ya PAPU yapo pale Arusha. Kwa hivyo suala hili tutalichukua kwenye mkutano wa wanachama wa PAPU ili kulizungumza na kuweza kuliweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ya Miundombinu imeshauri Serikali kutoa kipaumbele kwenye malipo na ada kwa wakati ili kuepuka kupoteza haki na kupata aibu ambayo nchi yetu inaweza kuipata hasa ukizingatia kuwa ndiyo makao makuu ya *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ni muhimu na Serikali imekuwa ikizingatia wakati wote na imeendelea kulipa michango hii kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeleta ushauri ufuatao: Mkataba kuwekwa wazi kuhusu hatima ya rasilimali zilizotolewa na nchi mwenyeji kwa ajili ya Makao Makuu pale ambapo itaondolewa uanachama kwa kuzingatia ibara ya 27 kuwa nchi yetu imekwishatoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu huko Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ni muhimu na unahusu maslahi ya moja kwa moja ambayo nchi yetu inayo. Kwa hivyo, tutalifanyia kazi mara moja, mara mkataba huu utakaporidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijikite kwenye hoja ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani. Kuhusu Kambi ya Upinzani nitajikita zaidi kwenye masuala ambayo yanahusiana na Katiba na mkataba wa *ATU* kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri ameangalia sana masuala ya *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ya Kambi ya Upinzani, kwanza wanaunga mkono hoja hii na wanaomba hoja hii iwe kwa Kiswahili kwani ni lugha muhimu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunashukuru sana Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono hoja na mchango wetu huu. Tutalichukua suala hili la lugha ya Kiswahili kwani ni muhimu sana katika kuendeleza lugha yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuridhia Katiba na Mkataba huu tutawashirikisha wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi nyingine jirani ili kuona jinsi gani tutakavyoweza kushawishi ili lugha ya Kiswahili iweze kutumika bila gharama zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya pili yalikuwa azimio hili lilianzishwa mwaka 1999 limeletwa ili kuridhiwa baada ya miaka 13. Napenda kukiri kuwa azimio hili limechelewa kuwasilishwa Bungeni na tunasikitika sana kwa hilo, lakini naomba nieleze yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ikumbukwe kuwa kabla ya kuundwa Wizara hii mwaka 2008 sekta ya mawasiliano kwanza ilikuwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, baadaye ilikuwa chini ya Wizara ya Miundombinu, wakati huo suala la mawasiliano lilikuwa limemezwa sana na sekta nyingine kama vile barabara, bandari na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuliona jambo hili ikaamua sasa iunde Wizara maalum ambayo itasimamia masuala ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano. Kwa kweli nchi nyingi wanatusifu kwa kuwa na Wizara kama hii kwa sababu mambo mengi yanaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukichukulia mradi wa mkongo wa Taifa ulikuwa umetegemewa uanze mwaka 2001, lakini kwa vile ulikuwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ulishindwa kuanza kwa wakati huo mpaka ulipoanza mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija tena kwa upande wa *UCAF*, kwa utaratibu *UCAF* ilitakiwa ianze mwaka 2006, lakini bahati mbaya ilishindwa kuanza kwa sababu ilikuwa kwenye Wizara hiyo na kipaumbele cha mawasiliano pale kilimezwa na sekta nyingine, lakini sasa mpango huu wa *UCAF* umeanza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine kwa nini mkataba umechelewa kuletwa hapa. Kwa utaratibu wa Serikali mkataba unapita kwenye mchakato mkubwa. Kwanza kabisa unaanzia kwenye *Cabinet Secretary* halafu unakwenda *MTC*, halafu ndiyo unakwenda kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mchakato mkubwa mpaka kufika hapo katika hatua zote hizo tunawashirikisha wadau mbalimbali wa sekta zote za mawasiliano ikiwemo *TCRA* na kampuni zote za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya Kambi ya Upinzani inayosema pamoja na ushirikiano na Mataifa na mwingiliano wa mawasiliano, ushauri unatolewa juu ya kulinda mila na desturi za Afrika. Ushauri umepokelewa na utazingatiwa. Aidha, Serikali inashirikisha wadau katika kutoa maoni wakati wa utayarishaji wa kanuni za maudhui kama ilivyoelezwa kwenye sheria yetu ya *EPOCA* ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine ambayo inazungumzia kuhusu wadau kushirikishwa katika mchakato wa kuridhia Katiba na mikataba ya Kimataifa. Maoni au maelezo kuhusu hoja hii katika Katiba na Mkataba wa *ATU,* wadau walishirikishwa ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Simu kama *TTCL, Zantel* na mengineyo pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imekuja na hoja nyingine inayosema kwamba, wanataka kujua utekelezaji wa Mfuko wa maendeleo ya huduma ya mawasiliano vijijini *UCAF* umefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyojibiwa katika Bunge la bajeti la mwaka huu, utekelezaji wa *UCAF* unaendelea vizuri na mwezi mmoja uliopita tulitangaza zabuni kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano kwenye vijiji 152 na zabuni hiyo itafunguliwa tarehe 14 mwezi Desemba mwaka huu ambapo tutapeleka mawasiliano kwenye vijiji 152.

Waheshimiwa Wabunge mkitaka maelezo kuhusu zabuni hiyo mnaweza mkatembelea tovuti ya *UCAF* ambayo ni *www.ucaf.go.tz* Aidha, lengo la *UCAF* ni kuhakikisha kwamba, vijiji vyote 3000 vinapata mawasiliano bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imekuja na hoja ya mwisho kwamba, ilitaka kujua ni lini sheria mpya itatungwa kulinda maslahi ya watumiaji na kuhakikisha matumizi mazuri ya mitandao ikiwemo ujumbe mfupi wa simu. Kwa kuanzia na utekelezaji wa Sheria ya Mawasiliano ya mwaka 2010 yaani *(UPOCA)* Serikali iliundwa Kamati ya Kushughulikia Usalama wa Matumizi ya Mitandao yaani *(SAT)* ambayo tunaita *Computer Emergencies Response Team* ambayo inashirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kushauri hatua zinazotakiwa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imepiga hatua nzuri na Mamlaka ya Mawasiliano ndio inaratibu shughuli hizi.

Aidha, Wizara yangu tangu mwezi Mei, 2012 imeanza kuchukua hatua za kuhusisha Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 ambapo suala la usalama wa mitandao ni hoja ya msingi mkuu wa sera hiyo ambapo inategemea kufika mwezi Aprili mwakani sera hiyo itakuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kutoa maoni yao kuhusu sera hiyo ambayo unaweza kutoa maoni yako kupitia tovuti ya Wizara yetu *www.mst.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo zilikuwa ni hoja za Kambi ya Upinzani, sasa naomba niende kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge walizozitoa. Hoja ya kwanza, nianze kwa Mheshimiwa Ezekia Wenje, yeye alikuwa amesema kwamba, bei za simu nchini hazishuki ingawaje tumewekeza kwenye pesa nyingi kwenye mkongo wa Taifa. Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 wakati unapiga simu kwenye *On-net, on-net* ni kupiga simu ndani ya mtandao mmoja *Airtel to Airtel or Zantel to Zantel.* Mwaka 2009 bei ilikuwa shilingi 147. Mwaka 2010 bei ilishuka mpaka ikafikia shilingi 93 ambayo hiyo ni asilimia 36. Mwaka 2011 bei ilishuka mpaka kufikia shilingi 59 ambayo ni asilimia 37. Hizi ni bei za wastani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia mpango wa *Off-net* ni kupiga simu kutoka kwenye *Airtel* kwenda *Zantel, Tigo* au *Vodacom*. Mwaka 2009 bei ilikuwa shilingi 292, mwaka 2010 ilikuwa shilingi 263, bei ilishuka kwa asilimia 10 na mwaka 2011 bei ilikuwa ni shilingi 187 bei ilishuka kwa asilimia 29. Ukija kwenye mkongo wa Taifa kabla ya mkongo wa Taifa kujengwa mwaka 2009 kifurushi cha *internet* cha *two gigabyte* kilikuwa kinauzwa shilingi laki moja. Leo hii kifurushi cha two *gigabyte* kinauzwa shilingi 30,000 ambayo hiyo ni punguzo la asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kifurushi cha *gigabyte* 40 ambazo mara nyingi kinatumiwa kwenye Makampuni kabla ya mkongo wa Taifa wa mwaka 2009 ilikuwa ni shilingi milioni moja. Leo hii ni shilingi 360,000. Vile vile kusafirisha mawasiliano kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine bei imeshuka kutoka kilomita 450 mpaka kilomita 500 kwa *speed* ya *two gigabyte per second* imeshuka kutoka dola 9,410 kabla ya mkongo na leo hii ni dola 158.7 ambayo ni punguzo la asilimia 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa pia alisema kwamba, kwa nini hatuigi kwa wenzetu kama Ghana na nchi nyingine ambazo ameweka mtambo maalum kwa ajili ya kuangalia mapato ya simu. Sisi hilo tumelitambua na tulishatangaza zabuni na Makampuni 24 kwanza yaliomba na tukafanya mchakato yakaja Makampuni sita, sasa hivi tayari tumeshachagua kampuni ambayo tutafunga mtambo pale *TCRA* kwa ajili ya kuangalia mapato ya simu zote hizi nchini. Tunategemea Mungu akipenda ifikapo mwisho wa mwezi Desemba mtambo huo utakuwa unafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nije kwenye hoja yetu ya msingi, nijibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, kwa kutumia njia ya maandishi, Mheshimiwa Ritta Kabati ametoa hoja hiyo, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa David Sillinde na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wamezungumzia suala kuwa Azimio hili lilianzishwa mwaka 1999, limeletwa baada ya miaka 13 na wakati huo nchi yetu imekuwa ikilipa ada. Ni kweli kama nilivyosema mwanzo, suala hili limechukua muda mrefu, lakini kama nilivyoeleza miaka ya nyuma kulikuwa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na ilikuwa na mambo mengi, halafu ikaja Wizara ya Miundombinu ambayo vile vile ilikuwa na mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona kwamba mambo ya mawasiliano kule hayaendi vizuri ndio Mheshimiwa Rais akaunda Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na tokea kuundwa Wizara hii mnaona kwamba, mambo mengi yanakwenda vizuri kwa mfano, kama *UCAF* na mambo ya mkongo wa Taifa yanakwenda vizuri na nyote mmeshuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja ambayo inahusu maoni kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Ignas Malocha, *Engineer* Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Pindi Chana na Waheshimiwa wengine wote wamechangia kuhusu hili, wakasema maoni kuhusu

matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa nini isitumike lugha ya Kiswahili katika Mikataba ya Umoja wa *PAPU* na *ATU* na kisiwe na alama inapotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyojibu, ni kweli suala hili tunalijua na sisi mara baada ya kuridhia Mikataba hii tutakaa na wenzetu nchi wanachama kuona jinsi gani tutaweza kuingiza Kiswahili iwe ni lugha ambayo inatumika bila gharama yoyote. Hili ni jambo muhimu kwa nchi yetu na tutaendelea kulipigania kuhakikisha kwamba tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja kuhusu suala la kulipa ada, kwa nini Tanzania inalipa ada kabla ya kuridhiwa. Suala hili limeulizwa na watu wengi, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Godfrey Zambi. Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja huu ambapo ni sehemu na ni wajibu wa kila nchi mwanachama kulipa ada hiyo. Kwa vile Tanzania ilisaini Mkataba ni lazima ilipe ada hiyo na tutaendelea kulipa ada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na suala ambalo linasema je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa Watanzania wananufaika na Mikataba hii kuona vijana wananufaika na mafunzo pia kuanzisha fidia, faida na changamoto. Suala hili limechangiwa sana na Mheshimiwa Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Ignas Malocho, Mheshimiwa Ritta Kabati na wengine. Maoni yamezingatiwa na Serikali itaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ningependa kutoa taarifa kuwa Tanzania imekuwa ikinufaika na fursa mbalimbali ikiwemo na mafunzo kama nilivyosema, kuna wataalam saba wameweza kupelekwa kusoma huko India kwa kutumia huu Umoja wa *PAPU*. Vile vile kuna miradi mingi ambayo Tanzania imeweza kufaidika kwa kupitia huu mpango au Umoja wa *PAPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kubadilishana uzoefu baina ya nchi yetu na nchi wanachama, kama vile, Shirika la Posta lilijifunza kutoka Zambia uanzishwaji wa huduma za *Bureua De Change* zinazoendeshwa na Shirika hivi sasa. Mradi huu ulipitia kwenye *PAPU* na tukajifunza kwa wenzetu huko Zambia na mradi huu unaendeshwa vizuri na Shirika la Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine mzuri ni ule mfano ambao tunauzungumzia anwani za makazi. Mradi ule ulianzia *UPU* ukaenda *PAPU* na Tanzania tukaanza *Pilot Project* kwa kutumia Umoja huu wa *PAPU*. Pia kuna mradi mwingine wa Kikanda kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo utumiaji wa pesa Kimataifa kupitia Posta (*International Financial System)* ambapo mradi wa majaribio wa Kanda ya Afrika ya Mashariki umefanywa hapa Tanzania ambao unasimamiwa na Mtanzania ambaye anafanya kazi pale *PAPU* na Shirika la Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *PAPU* Shirika limefaidika na mazoezi ya kupima ubora wa huduma za Posta. Kama mnavyokumbuka au kama mlivyoona kwenye mitandao katika Mkutano uliopita wa *UPU,* Shirika la Posta lilipata tuzo maalum kwa kuwa kati ya moja ya Shirika bora la Posta hapa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine ambayo imetoka kwa Mheshimiwa *Eng.* Athumani Mfutakamba, Wizara kuhamasisha na kuzielimisha Kampuni binafsi kujiunga na Umoja wa *ATU* ili kupata fursa ya kutoa mchango na mawazo ya kuboresha zaidi huduma za mawasiliano hapo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu tumeupokea, Wizara itaendelea kuelimisha Makampuni yote ya Simu hapa nchini na watoa huduma wote kuhakikisha kwamba wanajiunga na Umoja wa *ATU* na *UPU* ili waweze kuendelea kutoa huduma mpaka maeneo ya vijijini na kupunguza gharama za mawasiliano.

Suala la kulipa ada kabla ya kuridhiwa hili nimeshalisoma. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Felix Mkosamali na wengineo. Pia kuna suala lingine ambalo Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed alizungumzia hapa kuhusu PAPU, alisema, Serikali imejipangaje kulipa fedha za awali za mkopo kama ibara 15, hii nimeshaisoma nafikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed ameuliza kuhusu Mikataba ya *ATU* na *PAPU* kutomtaja bayana Mheshimiwa Rais au Waziri mwenye dhamana. Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu hili vizuri, sipendi nirejee tena kwa sababu ameshalijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Hussein Amar ametoa hoja Mkataba wa *ATU* uwezeshe uboreshaji kwa huduma za mawasiliano na ametoa mfano wa Kata 11 za jimbo lake kule. Aidha, tunamwambia moja ya faida ya Umoja wa ATU ni kuboresha mawasiliano Afrika. Huu mpango wa *UCAF* kwanza ulianzia huko *ATU* na sisi kama tunavyojua tumeshatangaza zabuni kwa ajili ya kupeleka mawasiliano kwenye vijiji na naamini kabisa vijiji vya Mheshimiwa Mbunge na yeye vimo kwenye ile zabuni tuliyoitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja nyingine ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Pindi Chana. Yeye amezungumzia kuhusu *PAPU* na *ATU,* suala la changamoto za utandawazi katika TEHAMA, matumizi ya simu *internet* na Posta. Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge umezingatiwa, taratibu za kutunga sheria matumizi ya *Cyber Security* inaendelea vizuri na tayari imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yote haya ya mambo ya mitandao yataangaliwa vizuri kuhakikisha kwamba tunalinda maadili ya watoto wetu na wananchi wetu kwa ujumla.

Aidha, Wizara yangu tangu mwezi Mei, 2012 imeanza kuchukua hatua kuhuisha Sera ya TEHAMA ambayo masuala ya usalama na maadili yataangaliwa vizuri ili kuhakikisha kwamba hapa nchini mambo ya TEHAMA hayatumiki vibaya badala yake yanatumika kwa kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala mengine ambayo yameulizwa na masuala mengine ambayo yanarejearejea, kwa mfano, yaliyoulizwa na Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Diana Chilolo kuhusu *PAPU* na *ATU*. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa Watanzania wananufaika na Mikataba hii kama nilivyoonesha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida kubwa imeshapata na tutaendelea kuhamasisha Umoja huu ambao tutaendelea kupigana kwenye Jumuiya hizi kuhakikisha kwamba tunapata faida kubwa kwa ajili ya nchi yetu. Kuna vijana wananufaika kwenye mafunzo haya ni kweli Wizara yangu imekuwa ikifuatilia kwa karibu fursa za ajira na mafunzo zinazotolewa na *ATU*. Aidha, nafasi za ajira zimekuwa zikitangazwa na Umoja kwa kila nchi na sisi kama Wizara inayosimamia sekta hii tutaendelea kuhamasisha wananchi wengi waweze kuomba nafasi hizi ili nchi yetu iweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakati wa uendeshaji wa Makao Makuu ya Umoja yakiwa Kinshasa ambako ndiko Makao Makuu Kikatiba. Mtanzania wa kwanza alikuwa ni Mtendaji Mkuu ambaye sasa hivi amekuwa marehemu, tunamwita Hayati Rajab Yusuph yeye alikuwa ni Mtendaji wa mwanzo kwenye Umoja huo. Tutahakikisha kwamba tunaendelea kuhamasisha wengine waombe nafasi hizi ili nao sisi tuweze kutangaza jina letu huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala bado ni mengi kidogo na naomba niendelee na masuala machache, je nchi imenufaikaje na masuala hayo, pia nimeshalijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya kuwa, Posta ina hali mbaya, manufaa ya moja kwa moja yatakuwaje kwa ajili ya hii. Kwa kweli Shirika la Posta watu wengi wanafikiri lina hali mbaya, lakini Shirika la Posta lina changamoto nyingi tunajua, lakini vile vile Shirika la Posta lina faida kubwa kama litatumia vizuri rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaanza kuweka anwani za makazi katika maeneo mbalimbali kupitia kwenye biashara ya mtandao, huwezi kuifanya biashara ya mtandao bila ya Posta. Unaweza kununua vitu kwa kutumia *internet,* lakini kuipeleka kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine lazima upate Posta. Kwa hiyo, sisi tunaamini Shirika la Posta lina uwezo mkubwa isipokuwa linatakiwa liendelezwe vizuri na linaweza kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna masuala ambayo Serikali imejipangaje kuboresha Posta nimejibu. Kusaini Mkataba wakati Shirika la Posta liko hai. Kama tunavyosema tutaendelea kudumisha Shirika la Posta kwa sababu ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yote yanaendelea na yanarejearejea, kwa hivyo naomba niishie hapo.

**MWENYEKITI:** Nakuomba uyasome Maazimio yote mawili kabla ya kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nitumie fursa hii kwa mara nyingine kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri mliyotupa. Kipekee niishukuru Kamati ya Miundombinu kwa ushirikiano mkubwa ambao imetupatia katika suala hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao niliwasahau waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa *Eng.*Athumani Mfutakamba na Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani. Samahani kwa kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limepitia Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika wa mwaka 2009, Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano wa Afrika wa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba uyasome Maazimio haya, Azimio la kwanza ambalo ni Azimio kuhusu Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta zile kwa kuwa zote uzirudie na moja. Halafu hii ya pili kwa kuwa zote zisome baada ya hapo utoe hoja halafu nitalihoji Bunge. Tafadhali!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ngoja niangalie hii.

**MWENYEKITI:** Anza na hii ya kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta wa Afrika wa mwaka 2009, halafu uje kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano wa Afrika.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika (*Instrumental of Pan African Postal Union)* wa mwaka 2009.

Na kwa kuwa kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano wa Afrika (*Constitutional and Convention of African Telecommunication Union (ATU)*) wa mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unatakiwa uzisome hizi taarifa kwa kuwa Umoja huu uko hivi, hizo hapo zisome zote. Usome Azimio la kwanza na usome Azimio la Pili. Azimio la kwanza linazungumzia kuridhia Mkataba wa Umoja wa Posta Afrika na Azimio namba mbili linazungumzia sema kuridhia Katiba na Mkataba.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** KWA KUWA Umoja wa Mawasiliano Afrika ulianzishwa kwa lengo la kusimamia maendeleo ya miundombinu na huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Bara la Afrika;

KWA KUWA Tanzania kama nchi mwanachama haijaridhia Katiba na Mkataba wa *ATU* ingawa inaendelea kutimiza masharti mengine ya uanachama ikiwemo kulipia ada na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimaamuzi ya Umoja huo;

KWA KUWA baada ya kuridhia Katiba na Mkataba wa *ATU,* Tanzania itaweza kushirikiana kikamilifu na nchi nyingine wanachama katika kukuza ushirikiano katika masuala ya utafiti na maendeleo, kujenga uwezo wa kitalaam na kuweka mikakati madhubuti ya kuendeleza miundombinu na huduma za TEHAMA ikiwemo ya kuliunganisha Bara la Afrika na Dunia kupitia huduma za mtandao wenye ubora na kwa gharama nafuu;

KWA KUWA Sera ya Taifa ya Mawasiliano *National Telecommunication Policy* ya mwaka 1997 inaagiza kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika sekta ya mawasiliano ili nchi yetu iweze kunufaika ipasavyo na TEHAMA;

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina jukumu la kuridhia Katiba na mikataba inayohitaji kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; "Kwa madhumuni ya Utekelezaji wa majukumu yake, Bunge laweza kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa";

KWA KUWAhakutakuwa na gharama ya ziada kwa Tanzania kuridhia Katiba na Mkataba huu zaidi ya kulipa ada ya uanachama ya kila mwaka kiasi cha shilingi milioni 40 ambayo Tanzania imeendelea kulipa;

HIVYO BASI naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika (*Constitution and Convention of the African Telecommunication Union).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, haya soma la pili.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** KWA KUWAUmoja wa Posta Afrika *(The Instrumental of the Pan African Postal Union (PAPU))* umeanzishwa kwa lengo la kujenga uwezo wa kitaalam, kuongoza na kusimamia maendeleo ya huduma za maendeleo katika Bara la Afrika.

KWA KUWA kwa mujibu wa Mkutano wa Mkuu wa Umoja wa Posta uliofanyika mwezi Juni, 2009 mjini Cairo, Misri kulifanyika na kupitisha marekebisho katika mkataba wa awali ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika Sekta ya Posta ili kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

KWA KUWA Tanzania kama nchi mwanachama bado haijaridhia Mkataba mpya wa Umoja wa Posta *(PAPU)* ingawa imeendelea kutimiza masharti mengine ya Uanachama ikiwemo kulipa ada ya uanachama na kushiriki katika mikutano ya umoja huo.

KWA KUWA nchi zote za wanachama zilizosaini mkataba mpya zinatakiwa kuridhia kulingana na utaratibu wa nchi zao na hadi sasa idadi ya nchi zilizoridhia mkataba huu ni tano ambapo mkataba huu utaanza kufanya kazi endapo asilimia 51 ya wanachama wa umoja watakuwa wameridhia mkataba.

KWA KUWA Tanzania ni mwenyeji wa Umoja huu uko umuhimu wa kuridhia mkataba huu na kushawishi nchi nyingine kuridhia ili mkataba uweze kutambulika kisheria na kuanza kufanya kazi. Ikizingatiwa kuwa, kutoridhia mkataba kutahatarisha heshima ambayo Tanzania imepewa ya kuwa mwenyeji wa *PAPU* kwani fursa hiyo inaweza kunyang'anywa na kupewa nchi nyingine zinazohitaji nafasi hiyo na hivyo kupoteza manufaa yanayotokana na kuwa mwenyeji wa Umoja wa Posta Afrika.

KWA KUWA kuridhiwa kwa mkataba huu kutaiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kushirikiana na nchi nyingine za Bara la Afrika katika kubuni sera na mikakati madhubuti ya kuendeleza Sekta ya Posta kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi.

KWA KUWA kuridhiwa kwa mkataba huu ni kutekeleza sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 inayoeleza kuhusu kuendeleza ushirikiano wa Kimataifa katika Sekta ya Posta.

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina jukumu la kuridhia mkataba kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 naomba kunukuu:

"Kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, Bunge laweza kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa." Mwisho wa kunukuu.

KWA KUWA madhumuni ya Azimio hili ni kuliomba Bunge lako Tukufu kukubali mapendekezo ya kuridhia mkataba wa *PAPU* kwa mujibu wa Ibara ya 29 ya mkataba huu ili nchi yetu iweze kunufaika katika kubadilishana wataalam, mafunzo, ufundi na tafiti mbalimbali zitakazoongeza tija pamoja na kuendeleza kupata manufaa yanayotokana na Umoja huu kuwa na Makao Makuu yake hapa nchini.

KWA KUWA Tanzania kama mwenyeji tayari imetoa jengo la ofisi za muda na hivi imetoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu na mchakato wa ujenzi wa ofisi za kudumu za Makao Makuu ya Umoja unaendelea, fursa ambayo Tanzania inaweza kuipoteza kwa kushindwa kuridhia mkataba mpya wa Umoja wa Posta Afrika.

KWA KUWA kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama inavyofanyiwa marekebisho na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndilo lenye mamlaka ya kuridhia mkataba huu na baada ya kuridhiwa hati ya kuridhia itaandaliwa na kuwasilishwa kwa mhifadhi ambaye ni Katibu Mtendaji wa Umoja wa Posta Afrika kama inavyoonyesha katika ibara ya 17(1)(2) ya mkataba huu.

HIVYO BASI naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia mkataba wa Umoja wa Posta Afrika *Instruments of Pan African Postal Union* ili Tanzania iweze kushirikiana na nchi nyingine za umoja huu katika kukuza maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba Mpya wa Umoja wa Posta Afrika, 2009 na Azimio la Bunge la Kuridhia Katiba na Mkataba wa Umoja wa Mawasiliano Afrika wa Mwaka 1999 Yaliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakupongeza, Naibu Waziri na watendaji wote na ninyi waheshimiwa Wabunge kwa kujadili maazimio haya na hatimaye kuyaridhia. Kazi nzuri mmefanya, basi niwatakie jioni njema.

Baada ya hapa naomba kuahirisha kazi hizi za siku hii ya leo hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.30 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 7 Novemba, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*